# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## Kikao cha Nane – Tarehe 5 Septemba, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Hiki ni Kikao cha nane cha Mkutano wetu wa kumi na mbili. Nawakaribisheni nyote, Katibu.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina orodha ya Wabunge 15 kama ambavyo nimekuwa nikisisitiza ni vizuri yeyote atakayepata nafasi kuuliza swali aulize kwa kifupi iwezekanavyo, kama kuna la nyongeza vile vile kwa kifupi iwezekanavyo ili kuwapa nafasi Wabunge wengine wenye nia ya kuuliza maswali. Kama ilivyo ada tunaanza na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni endapo ana swali.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu nchi yetu sasa iko katika kipindi kigumu ambapo Taifa linashiriki mchakato wa kuipata Katiba mpya ya Taifa letu. Ni dhahiri kwamba mchakato wa kuipata Katiba mpya unahitaji ustahimilivu, ushirikiano, uwazi, ukweli, dhamira njema na kipekee sisi ambao ni Wabunge ndani ya Bunge hili tunatambua na tunastahili kutambua kwamba wako wadau wengi sana nje ya Bunge hili ambao nao ni wadau kama sisi katika mustakabali mzima wa Katiba.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa matukio ambayo yalitokea juana ndani ya Bunge lako, panaonekana kuwepo ufa mkubwa ambao unaweza ukafanya dhamira njema ya kuiandika upya Katiba ya Taifa letu ikapata ufa mkubwa katika hatua hii ya kutunga na kurekebisha Sheria hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu Mkuu, wewe kama kiongozi wa Serikali Bungeni, ambayo Serikali yako ndiyo imeleta Muswada ulioleta sintomfahamu iliyotokea jana. Unatoa kauli gani kwa Watanzania kuhusiana na sintomfahamu hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba utulivu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili ndiyo limepewa mamlaka ya kutunga Sheria. Serikali

inacholeta ni mapendekezo. Yanaweza kuwa ni mapendekezo yanayohusu Sheria, yanaweza kuwa ni mapendekezo yanayohusu Marekebisho ya Sheria.

Mapendekezo hayo ndiyo maana yanapita kwenye hatua mbalimbali. Kuna hatua ya ushirikishwaji wa wananchi kwa kupitia *Public Hearing* lakini kubwa tunapokuja hapa matarajio ya wananchi ni kwamba Wabunge tuliyomo humo ndani tutaujadili Muswada huo kikamilifu na maeneo yote ambayo yanadhaniwa yanaweza yasiwe na tija au neema kwa nchi yetu ni jukumu letu sisi Wabunge kujadili kwa uwazi, kwa uaminifu, kiukweli na kazi kubwa ya Serikali katika mjadala ule ni kuona mahali gani inawezekana kweli tulipitiwa. Hili tunalikubali, sehemu gani tunadhani Waheshimiwa Wabunge hapa tunadhani bado msimamo wa Serikali ni sahihi. Lakini hatimaye tunafikia maamuzi ya pamoja yanayoonyesha nini hasa kinatakiwa kuwemo katika Sheria hiyo. *(Makofi)*

Niseme tu Mheshimiwa Mbowe, kilichotokea jana mimi nasema *it is very unfortunate situation, very unfortunate.* Nimejiuliza sana kumetokea nini hasa. Mambo gani ambayo yasingeweza kujadiliwa ndani ya Bunge hili na tukafikia muafaka. Suluhu ikaonekana badala ya Wabunge kutoka nje. Mimi nimepata taabu nalo sana. Sasa kama kwa kufanya hivyo ndiyo kuwakilisha watu kikamilifu mimi nafikiri hapana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niombe sana tutumie fursa hii ya kuwa Wabunge ndani ya Bunge kikamilifu. Hakuna Sheria

hapa itakayotungwa ambayo haitakuwa imejadiliwa kwa kiasi cha kuweza kuridhiana. Mara ngapi tumekubali baadhi ya mawazo kutoka kwa Wabunge, mara nyingi tu.

Kwa hiyo mimi sikuona kwamba ilikuwa kuna jambo kubwa sana pale la kutufanya mpaka Wabunge wote mtoke. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu kwa kweli tujaribu kuzingatia taratibu za Bunge na kwa kweli tujadili kikamilifu kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali fupi la nyongeza Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili jambo la Katiba, naomba niweke wazi siyo jepesi kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaopiga makofi wanavyotaka kuliona. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kweli kwamba yako matukio ya kibabe, ya kejeli, ya matusi, ya dharau, ambayo yana-*delay process* nzima ya kutafuta muafaka katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na rai uliyotoa, sisi tunaamini kwamba yako maeneo mengi yasiyo na tija ambayo yanafanya msingi wa Sheria au wa Muswada wa marekebisho ulioletwa jana uwe kwamba hauna tija kwa mchakato huu hauna tija kwa Taifa na sisi tunaamini kwamba kwa sababu kuna lengo jema na kwa sababu unasema kuna dhamira njema upande wa Serikali ni muafaka kwako na Serikali

yako kuuondoa Muswada huu mkaurejesha katika maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumsikilize Mheshimiwa anapouliza swali ili tuwe na ufuatiliaji wa pamoja. Huyu ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni mpeni heshima yake asikike anauliza swali gani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani endelea.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu narudia, maadamu umedai kwamba kuna dhamira njema kutoka upande wa Serikali na Chama kinachoongoza nchi. Ni ushauri rasmi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Muswada huu kama ulivyoletwa jana una maeneo makubwa ambayo utaweka ufa mkubwa kwenye Taifa hili kuliko mnavyofikiria.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumia Mamlaka yako ondoeni Muswada huu ukafanyiwe kazi za msingi mapema kabla, kafanyeni *Political Management* kwenye *process* hii kisha muulete Muswada ambao una muafaka wa pande mbili za Muungano kisha tutakwenda pamoja. Unatoa kauli gani kuhusu kuondoa Muswada huu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mbowe anasema Muswada una mambo mengi ambayo anafikiri si kwa maslahi ya nchi. Hivi kweli Mheshimiwa Mbowe

unangoja mpaka kweli Muswada unafika ndani ya Bunge ndipo unakuja na hoja ya namna hiyo wakati tulikuwa na fursa kubwa kwenye Kamati ndiyo, ndiyo utaratibu ndiyo. *(Makofi)*

Tulikuwa na fursa kwenye *Public Hearing*, kwenye Kamati yenyewe ya Bunge ndiyo, ni utaratibu tu. Ni utaratibu. Lakini mimi nasema katika mambo ambayo nimeelezwa jana kwamba ndiyo yaliyojiri na kusababisha mkatoka nje, hakuna mtu ambaye ataona umuhimu wa kuondoa Muswada huu hata kidogo. Kwa sababu ni vitu ambavyo ndani ya Bunge hili hili vinazungumzika na vinaweza kubadilishwa kulingana na mamlaka mliyopewa. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na *Montevideo Convention* ya tarehe 26 Desemba, 1933 imeleza tabia kuu nne za dola ikiwekwa upande wa ardhi, watu, utawala pamoja na ushirikiano wa mambo ya nje. Mfumo wetu wa kiutawala au wa dola ni mgumu *is a complex state* uki-*compare* na wenzetu ambao wana *simple state.* Tendo la kuunda dola ni tendo la kisiasa ambapo mfano Mwalimu Nyerere na Karume mwaka 1964 tarehe 22 Aprili, 1964 walisaini Mkataba wa Muungano.

Mfano mwingine Mwaka 2009 Maalimu Seif na Rais wa Zanzibar wakati huo Mheshimiwa Amani Karume walizungumza kisiasa kwanza, tendo la kisiasa, Sheria ikafuata baadaye.

Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Hatuoni kwamba ni busara majadiliano ya kisiasa yakafanyika kwanza na kwa uwazi kwa kushirikiana zaidi badala ya kuanza kwa Sheria zaidi tukaji-*engage* zaidi kwenye masuala ya kisiasa ya mazungumzo ambapo yatatusaidia, dhana halisi ya kuunda dola, dhana halisi ya kuunda Katiba ambayo ni tendo la kisiasa na Sheria inafuata baadaye? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo na ushauri wa Mheshimiwa James Mbatia, hata kidogo. Ni jema tu, tatizo tu ni kwamba kwa sababu nimeshindwa kuelewa ushauri huu unaunganishwa na nini hasa. Kwa sababu kama unazungumza Sheria hii ambayo tumeleta mabadiliko, mapendekezo ya marekebisho fulani fulani, kulikuwepo na mashauriano makubwa ndani ya Vyama kwanza, lakini hata baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Ndiyo maana hata huu Muswada mwingine wa pili tumeuondoa kwa dhana hiyo hiyo, tulikutana kwenye ngazi za Viongozi wa Vyama, kura ya maoni hiyo. Baadaye tukaja na mapendekezo. Tulipokwenda kuona wenzetu wa Zanzibar wakasema tunahitaji muda zaidi wa mashauriano. Tumekubali na tuliondoa Muswada ili wapate muda zaidi wa kushauriana.

Kwa hiyo, unalolisema ni la msingi na lazima liendelee kujengewa misingi imara zaidi katika hatua zake zote. Sasa pengine kwa hilo ulilolishauri kama kuna

namna ambayo unalitazama kwa maana ya suala lenyewe kwa upana wake kwamba pengine mambo mengine yote yawe *suspended* yaahirishwe kwanza, kwanza tuzungumze kwa ujumla jumla hivi ni jambo jema tu mimi sioni kama lina tatizo hata kidogo. Tutategemea sasa tunataka kuzungumza katika mfumo gani na kwa kujaribu kuzingatia mambo gani halafu tunaweza tukatoka pale tukaelewana tukaona sasa tunakwenda namna gani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Labda nifafanue kwamba kusudio langu ni kwamba ukiona kura ya maoni iliyofanyika Zanzibar tarehe 31 Julai, 2010 siku ya Jumamosi, ambapo asilimia 66.4 ya Wazanzibar waliamua kufanya kurejea au Toleo la 10 au mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar na kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar ni sehemu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kiasi kikubwa Katiba ya Zanzibar imechukua Mamlaka ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo kwa lugha nyingine niseme kuna Mgororo wa Kikatiba sasa hivi tunapozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mfano Rais wa Zanzibar amechukua Mamlaka ya kukagawa Tanzania Zanzibar kimikoa na kiwilaya, ni hatua nzuri wakati ni mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano. Hata

inaonekana kwamba mtoto amemzaa mama badala ya mama kumzaa mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa kutokana na mambo haya huko mbeleni tunakokwenda ambapo tunaona *crisis* itakuwa ni kubwa. Huoni tukiji-*engage* zaidi katika meza ya mazungumzo itatuvusha, badala ya kusema funika kombe mwana haramu apite? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, analolisema Mheshimiwa Mbatia kwa maoni yangu ingekuwa ni hoja ya msingi sana kama tusingekuwa katika hatua tuliyopo sasa ya kuandaa Katiba Mpya ambayo itatuongoza kwa muda unaokuja.

Katiba hii mpya inameza yote yaliyomo kwenye Katiba hizo mbili kuyafutilia mbali kuja na mawazo mengine ambayo tunafikiri yatatuongoza katika kipindi kinachokuja. Ndiyo maana nasema kama tusingekuwa na utaratibu huu pengine hoja hiyo ingekuwa nzuri sana. Lakini katika mazingira ninayoyaona sasa ninataka 2015 tuwe na Katiba mpya.

Mimi nadhani juhudi kubwa ziwekwe katika kuona Katiba hii hiyo mpya sasa iweje ili kuondoa hayo yote pamoja na hayo unayoyasema. Mimi nadhani ingekuwa ndiyo mtazamo sahihi zaidi katika jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali mawili yameshachukua dakika 15. Tunaendelea na dakika 15 zilizobaki. Swali tatu Mheshimiwa Weston Zambi.

**MHE. GOFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali kwa Waziri Mkuu. Lakini jina langu ni Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, moja ya sekta ambazo ziko kwenye mpango wa Matokeo ya Haraka (*Big Result Now)*, ni Kilimo. Lakini pia iko dhana muhimu sana kwenye sekta ya kilimo ambayo inasema Kilimo Kwanza.

Sasa nataka kujua Mheshimiwa Waziri Mkuu kama iko dhamira ya kweli kwa upande wa Serikali wa kutekeleza matokeo ya haraka kwa sekta ya kilimo lakini na dhana yenyewe ya kilimo, Kilimo Kwanza katika mazingira ambayo mbolea na pembejeo za kilimo kwa ujumla zimekuwa zinatoka kwa kuchelewa. Lakini pia zinakuwa chache kwa wakulima wa nchi hii ambao wanahitaji mbolea ya ruzuku ya Serikali. Nini dhamira ya Serikali katika kutekeleza hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kabla ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu niseme tu kwamba kila Mbunge ana majina rasmi matatu. Kwa hiyo, Kiti kikikuita katika jina mojawapo lolote katika hayo matatu bado ni sahihi ni ya kwako wewe mwenyewe. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mheshimiwa Zambi kwa kweli ni mtazamo wa Watanzania tulio wengi. Wengi tunatamani kilimo kipewe nafasi kubwa zaidi pengine kuliko hata sekta nyingine zote.

Lakini katika mazingira ambayo tuna mambo mengi ambayo yote ni muhimu lazima tukubali vile vile kwamba kwa kiwango cha fedha au kwa Bajeti tunazokuwa nazo ni lazima kuna baadhi ya maeneo hayawezi kulingana.

Tunachojaribu kufanya ni kuendelea kusisitiza sana juu ya umuhimu wa eneo hili ili Watanzania hasa mmoja mmoja ambao wanaweza kuwa na uwezo wajaribu kutoa msukumo zaidi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejitahidi kama Serikali, kuja na wazo hili la kutoa ruzuku kwa ajili ya pembejeo, lakini kama anavyosema Mheshimiwa Zambi, si kwa Watanzania wote wakulima kwa sababu, uwezo wa kufanya hivyo kwa watanzania wote bado hatuna, ndio maana tulikwenda hatua kwa hatua mwaka huu watu 7,500 uliofuata tukafika 1,000,000 tukalenga tukafika 2,000,000 na lengo ni kufika wakulima angalao 4,000,000.

Lakini bado utaona hata katika dhamira hiyo nzuri tumeshindwa kutoa pembejeo kwa 100% yaani kwa maana ya mahitaji ya kila mkulima anavyohitaji. Kwa hiyo, tukaona tutumie ekari ile moja kumfanya aelewe

umuhimu wa matumizi ya pembejeo, ili yeye mwenyewe afike mahali akishatambua aone anavyoweza kutumia uwezo alionao mdogo kuongeza kile ambacho Serikali, imemwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Zambi, nakubaliana na wewe kwamba, bado tuna safari ndefu, lakini matumaini yangu ni kwamba, kadiri uwezo wa kibajeti utakavyokuwa unaongezeka tutazidi kuongeza kasi katika eneo hili.

Sasa hivi tumeweka uzito mkubwa sana katika maeneo ya miundombinu, umeme na barabara. Tumetoa nafasi kubwa sana kwa ajili ya kusukuma elimu, lakini tumeweka msisitizo vilevile mkubwa sana katika sekta ya afya na maji. Lakini ni katika hatua zile za mwanzo kwa sababu mambo yote tunayahitaji. Kwa hiyo, mimi nadhani muda mzuri ukifika, basi anayoyasema Mheshimiwa Zambi, yatazidi kupewa nafasi kubwa zaidi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni nini Kauli yako kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, kuhusu upatikanaji wa mbolea ya ruzuku mwaka huu kwa sababu, moja ya kilio cha watanzania, hasa hawa wanaofaidika na mbolea ya ruzuku, ni kupata mbolea wakati msimu hasa wa kilimo umeshapita. Ni nini Kauli yako kwa msimu wa kilimo wa mwaka huu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, imejipanga kuhakikisha kwamba, mbolea inapatikana

mapema inavyowezekana na tuweze kuisambaza na kuifikisha kwa wakulima kabla ya msimu wa mvua haujaanza. Sasa Wizara ya Kilimo ilichofanya, imejaribu kuja na njia mbili kwa hiyo, tutakuwa na utaratibu huu wa sasa katika baadhi ya maeneo, utaendelea, lakini tumeona katika sehemu ya pili tutumie vikundi mahsusi kwa ajili ya kutoa hiyo pembejeo kwa njia ya mkopo. Kwa hiyo, tutakwenda na yote mawili, matumaini yangu ni kwamba, Wizara inafanya kazi kubwa kuhakikisha hatucheleweshi mbolea hata kama itakuwa ni katika mazingira ya kuhitaji zaidi msukumo kwa ajili ya kuwezesha jambo hili liweze kukamilika mapema. Kwa hiyo, tutajitahidi kwa kadiri tutakavvyoweza.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sera ya Idadi ya Watu na Makazi, ilirekebishwa mara ya mwisho mwaka 2006, yaani miaka 7 kutoka wakati huo. Tafiti za mwaka 2010 za Mama na Mtoto zinaonesha kuwa watoto 6 kwa kila mwanamke mwenye umri wa kuzaa na 42% ya watoto walio chini ya miaka 5 wana utapiamlo na 67% ya watoto walio chini ya miaka 5 wana upungufu wa damu. Lakini Sensa ya Makazi ya mwaka jana inaonesha *Birth Rate* inakuwa kwa kasi – 2.6% na wakati huohuo uchumi wetu unakuwa kwa 6% mpaka 7%.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa, tangu mwaka 2006 kumefanyika mabadiliko makubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa, Serikali, haioni kuna haja ya

kufanya tathmini ya Sera hii kwa ajili, ya kuona kama inaendana na ongezeko la watu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Machangu na Serikali tumeshaanza kulitazama hilo eneo. Kwa kweli, kilichofanya tukafikia uamuzi ule ilitokana hasa na ongezeko la watu ambalo linakuwa kwa kasi kubwa. Kwa hiyo, tumeomba vyombo pamoja na Taasisi yetu ya Takwimu, washirikiane kufanya tathmini juu ya Sera ile, ili tuweze kuwa na uhakika kwamba, tunakwenda sambamba na mahitaji ya nchi yetu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bajeti ya Wizara ya Afya tangu mwaka 2011/2012 mpaka leo haijaongezeka na bado iko 10%, lakini Azimio la Abuja la nchi za Umoja wa Afrika pamoja na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* mwaka 2001 walikuabaliana Bajeti za Wizara za Afya zifikie 15% itakapofika 2015 kwa ajili ya kuondoa vifo vya watoto na akinamama wanaotaka kujifungua kwa nchi za *Sub-Sahara.*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unatoa Tamko gani kuhusu utekelezaji wa hili Azimio la Abuja kwa Tanzania?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza swali lenyewe sina hakika kama ni la nyongeza au ni jipya kabisa, lakini ninachoweza kusema tu ni kwamba, ni kweli Tamko hilo lipo, lakini tunayo Matamko mengi kwenye Kilimo yapo, kwenye elimu yapo. Sasa jitihada

za kila nchi kulingana na uwezo wake wa kibajeti ni kulenga kweli kufikia viwango hivyo ambavyo vimewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa upande wa Tanzania tunachoweza kusema ni kwamba, tunajitahidi kufika huko, lakini tunakwenda hatua kwa hatua.

Ni kweli kwa maana ya bajeti ya nchi inawezekana ikaonekana bado ni ndogo, lakini bado tumepata sisi misaada mingi kutoka kwa wadau mbalimbali na ndio maana unaona hata takwimu sasa zinaonesha dalili nzuri kwamba, vifo vinaendelea kupungua kwa watoto wachanga, watoto chini ya miaka mitano, hata kwa akinamama kuna *improvement* kidogo kuliko ilivyokuwa hapo mwanzoni.

Kwa hiyo, mimi nadhani ni kuendelesa kuchanganya wadau wote pamoja na jitihada zetu za ndani, ili tuweze kufikia lengo hilo. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kumwuliza Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa sasa ni dhahiri kabisa kwamba, pengo kati ya masikini na matajiri Tanzania linazidi kukua siku hadi siku. Na kwa kuwa, ki-historia ulimwenguni pengo kama hili ndio chanzo cha nchi kuingia katika vurugu na kupoteza amani ya nchi.

Je, Serikali, haioni tatizo la pengi hili? Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la Mama Kilango ni pana ni kubwa na linahitaji kulitafakari kwa kina kabla hujapata majibu ya uhakika sana. Lakini labda niseme kwa ujumla tu kwamba, jitihada za Serikali kwa sasa ni kutafuta kila njia inayowezekana ya kumwezesha mwananchi wa kawaida, ili kuweza kumwongezea uwezo wake wa kupambana na hiyo hali ya umasikini.

Sasa tumekuja na njia mbalimbali ambazo tumejaribu kuzitumia katika kumwezesha kufanya hivyo na juzi hapa itakuwa mliona, tumejaribu kuja na mpango mwingine wa kujaribu sasa kuona ni namna gani tunaweza tukawasaidia hasa wale wananchi ambao wana umasikini uliokithiri kwa kujaribu kutoa fedha, ili kuwawezesha waweze kutoka pale walipo, kama njia ya kujaribu kupunguza hilo eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado ni lazima tukiri kwamba, kazi ni kubwa kwa sababu, ni lazima tuhakikishe kwamba, hili kundi kubwa ambalo ni karibu 70% ni lazima liwezeshwe zaidi kuliko makundi yale mengine. Lakini kwa sehemu kubwa itategemea vilevile mambo mawili. Uwezo wa nchi, lakini kubwa na jitihada za kila mwananchi katika kujaribu kutatua hilo tatizo kwa pamoja. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MUHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na utafiti wa Benki ya Dunia kuhusiana na Bandari ya Dar-es-Salaam kwamba, ikiwa itaboreshwa ki-miundombinu, ki-ufanisi,

pato linaweza likaongezeka likafikia hadi dola bilioni 1.8 kama itafanyiwa maboresho kama vile Bandari ya Mombasa, Kenya ambayo itakuwa *almost* ni kama 7% ya pato la Taifa. Mbali na yale tuliyopitisha katika Bajeti kuhusu Gate Number 13 na 14 ambayo itafanyiwa maboresho na kampuni ya *China Harbour (CCC).* Je, Serikali, ina mpango gani wa kuiboresha Bandari hii kiutafiti, ili kufikia lengo hilo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana kwanza Mheshimiwa Eng. Mnyaa, kwa sababu, anauliza jambo ambalo ni la msingi sana.

Kwa upande wa Tanzania, linakuwa ni la msingi zaidi kwa sababu, tuna uwezo mkubwa sana wa kuweza kutumia bandari hii kwa kuwahudumia majirani zetu ambao kwa kweli, hawana sehemu nyingine ya mlango wa kutokea, isipokuwa hapa au Mombasa. Kwa hiyo, tukiimarisha hapa tuna uhakika kabisa unalolisema linawezekana kabisa.

Kwa hiyo, kwetu sisi Bandari, imepewa kipaumbele kikubwa na kama siyo kwa sababu ya yaliyojiri kwenye Bajeti ile iliyopita mwaka jana. Wewe mwenyewe utakumbuka tulikuwa tumepanga vizuri kujaribu kuiboresha bandari ile, lakini ilionekana kuna matatizo ikabidi tukubali kulitazama tena upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, limetazamwa, tumeshafikia maamuzi. Kwa hiyo, ujenzi wa ile Bandari ni sehemu ya mkakati wa kujaribu kuongeza uchumi wetu wa nchi. Kwa hiyo, mpango upo, tunachofanya

sasa ni zile taratibu tu, ili paweze kutengenezwa, pajengwe, tuongeze gati, ili tuweze kufanya Dar-es-Salaam sasa iwe ni Bandari nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hiyo peke yake haitatosha, ndio maana katika mpango ule tunaangalia vilevile tunafanya nini na reli, ambayo ndio inatoka pale Bandarini na kusafirisha mizigo kwenda Bara, lakini vilevile na kwenda nchi jirani. Kwa hiyo, reli kwetu vilevile ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha ubora wa Bandari yetu na vinakwenda pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni *Container Terminals* kwa sababu nalo hili limeonekena ni jambo la msingi sana. Sasa maeneo ya kuegesha makasha sasa hivi yaliyopo ni kidogo sana, hayatoshi kama tutajipanga vizuri na ukuaji huu wa haraka.

Ndiyo maana tumeingia sasa katika wazo jipya la kuona ni namna gani Sekta Binafsi na yenyewe inaweza ikajiingiza katika eneo hili kwa nguvu, ili tuweze kuwa na maeneo makubwa zaidi kwa ajili ya uhifadhi wa makasha haya, kwa hiyo, kurahisisha na kuondoa mlundikano ambao unapatikana kwa sasa pale Bandarini.

Kwa hiyo, kwa kweli, mkakati upo na ninafikiri Waziri wa Uchukuzi kama atapata nafasi, anaweza akalifafanua vizuri zaidi katika siku zijazo, ili muweze kupata uelewa mpana zaidi. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mhehimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri, lakini bado nina swali dogo la nyongeza. Kutokana na Ripoti ya Benki ya Dunia pia ya Mwaka 2012, Tanzania imekuwa *ranked* kwamba ni nchi ya 127 kufanya *business.*

Pamoja na maelezo uliyotoa ya reli na *Container Terminal,* lakini yako matatizo mengine sugu. Kwa mfanoni suala la barabara ambayo usafirishaji mizigo na bidhaa kupitia Tanzania kwa hizo nchi za jirani inasimamishwa njiani, vituoni, mara 38 na inawezekana ndio lililosababisha majirani zetu kufanya vikao ambavyo vina-*exclude* Tanzania sasa hivi ambavyo vinaleta *effect* mpaka kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Je, ni nini Tanzania sasa itafanya baada ya kugundua hayo na kuona wenzetu wanatuacha mkono pamoja na mambo mengine, lakini kwa sababu za miundombinu yetu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika sana kwamba, kama kweli, majirani hawa wanaokutana-kutana moja ya ajenda yao ni kutokana na vikwazo vya barabara, hapana. Hilo sina hakika nalo sana. Mimi nadhani jambo la msingi hapa ambalo umelisema ni Serikali inafanya jitihada gani kupunguza vikwazo hivi vya barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa limekuwa ni jambo moja kubwa ambalo tumelizungumza sana, tumefika

mahali tukaanza kulitekeleza. Kulikuwa na vituo vingi sana, tikajitahidi kupunguza mpaka karibu 40, ikaonekana bado ni vingi, tukachukua hatua nyingine zaidi, nadhani viko kwenye kumi na sasa hivi.

Lakini tatizo ambalo bado linalojitokeza Mheshimiwa Mnyaa. Oh! nchi hizi masikini zinazoendelea tabu kwa sababu, suala la usalama kwetu na lenyewe linakuwa ni jambo jingine ambalo muda wote linaturudisha nyuma. Kwa hiyo, unakuta wakati mwingine kunalazimika kuweka tena vizingiti barabarani kwa sababu tu za kiusalama kutokana na taarifa mbalimbali zinazopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajaribu kuliangalia nalo hili tuone tutafanyaje, ili vingine visije vikawa visingizio tu kwa ajili ya watu kutaka kujinufaisha kwa kisingizio hicho. Lakini kwa kweli, tumeshapiga hatua nzuri, tulikuwa tunakwenda vizuri na mimi naamini baada ya muda si mrefu, tutafika mahali tutaelewana vizuri sana juu ya jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkitizama muda wetu mtaona nusu saa yetu imeisha. Naomba tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu mazuri kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunasema ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Tulikuwa na waliokuwa wameonesha nia ya kuuliza Maswali kwa Waziri Mkuu 15, tumeweza kuwapata watano. Tunaendelea, Katibu! *(Makofi)*

## MASWALI YA KAWAIDA

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya Kawaida; Swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini. Mheshimiwa Kigola, kwa niaba yake Mheshimiwa Ritta Kabati?

Na. 96

### Kituo cha Afya Mgololo Kupatiwa Gari

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. MENDRAD L. KIGOLA)** aliuliza:-

Kata ya Mgololo ina Vijiji vikubwa ambavyo vinategemea Kituo cha Afya cha Mgololo, ambacho hakina gari na pia kinahudumia Wananchi wa Kata ya Kiyowela:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa kupeleka gari la wagonjwa katika kituo hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inavyo vituo vya afya sita vya Serikali, ambavyo ni Kasanga, Mgololo, Ifwagi, Sadani, Malangali na Ihongole. Aidha, vituo vya afya vya Serikali, vyenye magari ni Kasanga na Malangali, gari jingine la Wagonjwa lipo katika Hospitali ya Wilaya ya Mufindi iliyopo Mjini Mafinga. Kwa hiyo, Halmashauri ina jumla ya magari ya wagonjwa matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa, kituo cha afya cha Mgololo, kinahudumia vijiji vikubwa na hakina gari. Serikali kwa kulitambua hilo, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2013/2014, Halmshauri ya Wilaya ya Mufindi, imetenga fedha kupitia maombi maalum kiasi cha shilingi milioni 150 za ununuzi wa gari la wagonjwa. Gari hili litakaponunuliwa litapelekwa kituo cha afya cha Mgololo, hivyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge, avute subira wakati tukisubiri upatikanaji wa fedha hizo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na niseme ukweli kabisa, vijiji hivi ambavyo vimezunguka Kituo hiki, akinamama wamekuwa wakipata shida sana, hasa wajawazito kutokana na miundombinu mibovu, wamekuwa wakitumia mpaka Boda-Boda kupelekwa katika Hospitali ya Wilaya.

Sasa ninaomba tu labda kujua, ili wanawake wale wa Mufindi au wananchi wa Mufindi waendelee kuwa na matumaini; ni mikakati gani hasa imeshafikia mpaka sasahivi, ili kuweza kupatiwa hilo gari?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Tatizo la magari ya wagonjwa liko katika maeneo mengi sana, ikiwemo hata katika hospitali yetu ya Wilaya ya Iringa Mjini katika Manispaa ya Iringa, Jimbo la Iringa Mjini.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri, hospitali hii imefunguliwa muda sasa, lakini wagonjwa wale wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana na hasa kutokana na kwamba, Hospitali yetu ya Mkoa pia, ina gari moja tu. Ningependa kujua ni lini pia Hospitali hii ya Iringa itapatiwa gari?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu langu la msingi nimesema tumeweka kwenye Bajeti fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari la kituo cha Afya cha Mgololo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi tunasubiri hizo fedha magari yaliyopo katika vituo vile viwili pia yanasaidia kutoa huduma katika vituo vinavyozunguka na lile gari ambalo lipo katika Hospitali ya Wilaya pia inahudumia vituo vya afya ambavyo havina magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lini watapata gari la wagonjwa ni pale ambapo Wizara ya Fedha ambayo na yenyewe pia ni Serikali itakapotoa fedha

za kuweza kununua hilo lakini kwa maana ya Bajeti tumetenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile swali la pili kwamba ni lini Hospitali ya Wilaya ya Iringa itapata gari ya naomba suala hilo aniachie nilifuatilie kwa sababu kama alivyosema ni mpya imefunguliwa karibuni. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana swali langu kwa kuwa Wilaya na jimbo la Kishapu hatuna Hospitali ya Wilaya na huduma za afya hasa kwa kina mama na watoto zinategemea sana vituo vichache vya afya tulivyonavyo wakati tukiendelea na jitihada nyingine za kujenga vituo vya afya.

Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara alikuta tuna *ambulance* mbili nilimuomba *ambulance* nne na baada ya muda kweli *ambulance* hizo zilifika namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu kwa kuwa huduma hii ya afya hasa kwa majimbo ama Wilaya zisizokuwa na Hospitali za Wilaya zina tabu nyingi sana kwa kina mama na watoto kusafiri kutafuta huduma hizi.

Je, Mheshimiwa Waziri ananihakikishiaje kuniongezea gari za wagonjwa *at least* nne wakati tukiendelea na jitihada za kujenga Hospitali ya Wilaya

ili akina mama wenzako wasipate tabu pamoja na watoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi, ukipata magari manne peke yako Kongwa na sisi tutapata chochote kweli? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nchambi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka huu sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hatukuweka Bajeti ya ununuzi wa magari isipokuwa tumezielekeza Halmashauri moja moja kutenga katika Bajeti zao kwa mujibu wa *ceiling* zao walizopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama tatizo la magari ya wagonjwa katika Wilaya yake ni kubwa sana basi ajitahidi sana kuhakikisha yeye pamoja na Halmashauri wanaweka katika Bajeti ya Halmashauri husika ili kuhakikisha wanapata magari ya wagonjwa. *(Makofi)*

Na. 97

## Fedha za Mradi wa MKUHUMI

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Wahisani wa maendeleo wanatoa fedha nyingi kwa ajili ya mradi wa MKUHUMI ambao unakusudia kuhifadhi mazingira.

Je, wananchi wanafaidika vipi na fedha hizo katika kuhifadhi mazingira ili kuhimili mabadiliko ya tabia nchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabia nchi yaani *climate change* ni changamoto inayoikabili dunia kutokana na ongezeko la gesi joto *(green house gases)* angani hususani gesi au hewa ukaa yaani *carbon dioxide*. Nchi zilizoendelea zinachangia uzalishaji wa gesi joto hewa ukaa angani kutokana na uzalishaji viwandani kwa zaidi ya 60%. Nchi za ukanda wa tropiki ikiwemo Tanzania zinachangia ongezeko la hewa ukaa kwa asilimia kati ya 18 mpaka 20 kutokana na ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa unaosababishwa na uharibifu wa misitu mpango maalum wa MKUHUMI yaani mkakati wa kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na kuhifadhi miti na misitu ulianzishwa duniani mwaka

2007. Nchini Tanzania ulianza kutekelezwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi tisa ya majaribio ya MKUHUMI inatekelezwa kupitia asasi zisizo za Serikali katika Wilaya za Kondoa, Kigoma, Kilosa, Kilwa, Lindi Vijijini, Rungwe, Muheza, Kisarawe, Shinyanga Vijijini na Kahama, kwa upande wa Tanzania Bara.

Katika Wilaya za chakechake, Wete, Mkoani, Micheweni, Kusini Unguja, Kati na Kaskazini B kwa upande wa Tanzania Visiwani. Miradi hii inalenga kuhifadhi misitu ya asili, kupanda miti kwa ajili ya matumizi ya wananchi hususani nishati, kilimo bora, matumizi ya majiko banifu na mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya vijiji vya majaribio vimefaidika na miradi ya MKUHUMI kutokana na uuzaji wa hewa ukaa. Vijiji hivyo ni pamoja na kijiji cha Mkanga Lindi vijijini, Likwaya Lindi vijijini, Isanga Dodoma na Kijiji cha Chamiba Kilosa. Aidha baadhi ya vijiji vimeanzisha miradi midogo midogo inayowaongezea kipato wananchi na vile vile kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kutoka kwenye misitu ya asili. Mfano kijiji cha Chololo Wilaya ya Dodoma wananchi wameweza kuongeza mazao ya chakula na biashara kwa kulima mazao yanayostahili ukame, kijiji cha Muyuni C Kusini Unguja kikundi cha kina mama kinatengeneza majiko banifu na kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Shirika la *African Wildlife Foundation (AWF)* huko Kondoa limeanzisha mipango ya matumizi bora ya ardhi na upandaji wa miti. Kwa upande wa kujengea uwezo Watanzania 16 wa Shahada za Uzamivu *(Ph.D.)* na 50 wa shahada za Uzamili katika Sayansi *(M.Sc.)* walipata ufadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa MKUHUMI unakuja na fursa anuai *(diversity)* ambazo zinawanufaisha wananchi wengi moja kwa moja kwa kuongeza kipato, kuhifadhi mazingira na kupunguza uharibifu wa misitu, vyanzo vya maji na pia fursa ya kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuweka ulinganifu katika matumizi ya rasilimali.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jibu la Mheshimiwa Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la Mheshimiwa Waziri imedhihirika kuwa mradi wa MKUHUMI upo katika sehemu zote mbili za Muungano.

Je, namwuliza sasa kuna zile nafasi za masomo ambazo 16 wa Uzamivu *Ph.D.* na 50 za *Master Degree* Wazanzibari wangapi wamepata nafasi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili imedhihirika Mheshimiwa kuwa mradi huu unapata ufadhili wa moja kwa moja kutoka nje.

Je, Serikali imejiandaa vipi ufadhili huu utakapokoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nafasi za masomo kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba fedha hizi za MKUHUMI zinakwenda moja kwa moja kwa asasi zisizo za Kiserikali. Ofisi ya Makamu wa Rais ni mratibu tu, nafasi za masomo fedha zile zinakwenda moja kwa moja *SUA* na zinaenda moja kwa moja *University of* Dar es Salaam.

Kwa hiyo, wanatumia vigezo vya kitaifa vya kufaulu kwa hiyo ukitaka kujua Wazanzibari wangapi wamekwenda naomba uje ofisini tutaenda *University of* Dar es Salaam na SUA tukajue Wazanzibari wangapi walikidhi vigezo kwa kupata Shahada ya Pili *(M.A.)* na ya tatu *(Ph.D.).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali ina mpango gani mpango wa Serikali upo na ndiyo maana tunahamasisha kwa sababu bado Baraza la Mikopo linatoa mikopo kwa fani zote zilizopo vyuo vikuu.

Kwa hiyo, bado tuna nafasi mbalimbali kwa sababu *University of* Dar es Salaam kama mnavyojua imeshaanzisha *degree* za *Climate Change* kwa hiyo Serikali imeshajidhatiti na wale wanafunzi wote

wanaoingia kwenye *degree* za *Climate Change* wanapata mkopo kutoka kwenye bodi ya mikopo. Kwa hiyo huo ndiyo mkakati wa Serikali na bado tunaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 98

**Hewa Chafu Kutoka Kwenye Matanki ya Mafuta**

**MHE. ABIA M. NYABAKARI (K.n.y. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Wananchi wa Kigamboni ambao wamezungukwa na matanki ya mafuta wanapata hewa chafu yenye harufu mbaya mara matanki hayo yanapokuwa yanasafishwa.

Je, hewa na harufu zinazotoka kwenye matanki hayo ni salama kwa maisha ya binadamu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA** alijibu**:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta yanayohifadhiwa kwenye matanki baada ya muda mrefu hutengeneza tope sehemu ya chini ya matanki hayo. Tope la mafuta huwa na kiasi kikubwa cha kemikali za aina mbalimbali ambazo kwa ujumla huitwa *hydro carbons.*

Kwa kuwa si rahisi kupima kiwango cha kila aina ya kemikali iliyoko katika hewa kipimo kinachotumika kuelezea uwingi wa kemikali hizo kinajulikana kama *total petroleum hydro carbons.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa kemikali hizo zinaweza kuleta madhara kwa binadamu iwapo zitakuwa hewani kwa kiasi kikubwa na kwa muda mrefu.

Madhara yanayoweza kusababishwa ni pamoja na maumivu ya kichwa na kusikia kizungu zungu kwa sababu ya mfumo wa damu kuwa na kemikali, kuwasha macho, pua, madhara kwenye mapafu na maini kama binadamu atakuwa kwenye mazingira hayo kwa muda mrefu.

Kwa maana hiyo watu wanaoweza kuathirika zaidi na hewa ya *hydro carbon* ni wafanyakazi wanaohusika na usafishaji wa matanki hayo endapo hawatatumia vitendea kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti mbalimbali zilizofanywa zinaonyesha kuwa viwango vya kemikali yaani *Total Petroleum Hydro carbon* katika hewa nje ya

matanki viko chini sana kiasi ambacho hakiwezi kuleta madhara kwa wakazi karibu na matanki hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana mwezi wa tano Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilifuatilia suala hili na hakuna madhara yoyote yaliyobainika. Hata hivyo kwa ajili ya tahadhari Serikali itaendelea kiufanya uchunguzi wa mara kwa mara yaani *monitoring* ili kuona kama kuna tatizo lolote litakalojitokeza.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Wananchi wa Vijibweni na Kigamboni kufuatana na majibu ya Waziri naamini wanaamini kwamba wanaishi katika maisha hatarishi ya kuvuta hewa chafu.

Je, Serikali inaweza kuwaambia kwamba waliokwisha kuathirika na hali hiyo ni wangapi ya kutokana na madhara ya hiyo *air pollution* na Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi hao kwamba ni lini itakomesha sasa harufu chafu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matanki ya mafuta yanasafishwa na meli nazo tunaamini kwamba huwa zinabeba mafuta na mafuta machafu yakiwepo.

Je, ni meli ngapi ambazo zimefanyiwa usafi katika bandari yetu ya Dar es Salaam mwaka 2012 na yalitupwa katika eneo gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyabakari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameuliza kuhusu wananchi wa Vijibweni na Kigamboni kama wamepata athari kiasi gani? Lakini jibu langu la msingi nimesema Wizara ya Afya kwa sababu tuliandikiwa barua Ofisi ya Makamu wa Rais tukaipeleka Wizara ya Afya na wataalamu wa Wizara ya Afya walienda sehemu hizo za matanki kupima kama kuna athari zozote zile na baada ya kupima waliona kiasi kilichopo hewani ni kidogo sana kiasi ambacho hakiwezi kuathiri maisha ya binadamu.

Waheshimiwa Wabunge labda niwaeleze tu hizo *hydro carbon petroleum* hata sisi tunazivuta kwenye magari yetu. Kwa hiyo, hata sisi kama tunataka kuacha kabisa tuache matumizi ya magari ili tuwe salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango kilichoko kwenye magari kwa sababu ni *petroleum* na kiwango kilichopo hewani, hewani ni kiasi kidogo sana ambacho hakileti madhara.

Tamko ninalolitoa ni kwamba matanki yale yanasafishwa kwa utaalamu mkubwa na wataalamu wanakuwepo wakati wa kusafisha kwa hiyo hakuna athari kubwa athari kubwa inayoweza kuwadhuru wananchi wa Kijibweni au Kigamboni na hata sisi wenyewe kwenye magari yetu hakuna athari tunayoweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ameuliza kwamba matanki haya yakisafishwa labda mvua inaweza kuchukua na kupeleka kwenye vyanzo mbalimbali vya maji na maeneo chepechepe.

Ninachoweza kusema ni kwamba utaalamu unatumika katika kusafisha kwa hiyo wanaposafisha yale matanki siyo maana yake lile tope lililoganda chini litawekwa tu kwenye sehemu ambayo ni kwenye mazingira halafu likaenda kwenye bahari au kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, matope yale yanakusanywa vizuri na yanahifadhiwa vizuri na hayaendi kwenye mazingira ambako wananchi wanaishi.

Lakini kwa ziada ni kwamba sehemu ile yote yenye matanki sasa hivi mnajua kuna mradi mkubwa wa kuendeleza sehemu ile ya Kurasini kwa hiyo watu watahama kwa hiyo lile eneo lote litakuwa la bandari.

Na. 99

**Ofisi kwa Wawekezaji Bandarini**

**MHE. JAKU HASHIM AYUBU** aliuliza:-

Pamoja na Serikali kuhamisha na kukaribisha wawekezaji kwenye sekta mbalimbali bado kwa muda

mrefu wawekezaji hao hawapewi ofisi kama vile ilivyo katika majengo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania.

(a) Je, ni vigezo gani vinatumika kuwapa ofisi wafanyabiashara wa ndani wanaouza nguo na mikate na kuwaacha wawekezaji wakubwa ambao huhitaji ofisi kwa ajili ya kuimarisha uwekezaji mkubwa?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa kitendo hicho kwa kuwa wawekezaji hao ambao ni walipa kodi wakubwa wamekuwa wakiomba kupatiwa ofisi bila mafanikio kwa muda mrefu na kuacha ofisi hizo kutumiwa na biashara za kawaida za ndani?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayub, Mbunge toka Baraza la Wawakilishi (B.L.W.), lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la bandari ya Dar es Salaam kwa sasa ni finyu kutokana na kuongezeka kwa shehena ipitayo katika bandari hiyo mwaka hadi mwaka. Katika kukabiliana na changamoto na ufinyu wa eneo na kuzingatia kanuni bora za uendeshaji wa bandari *TPA* inashirikiana na wadau wa bandari kuhamishia sehemu ya shehena inayoshuka nje ya bandari na kuhamisha ofisi za wadau kutoka ndani ya bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha taarifa ya awali ya mshauri muelekezi wa *TPA* kwenye mradi wa kuifanya bandari ya Dar es Salaam kuwa ya kisasa yaani *Port Modernization* inapendekeza majengo ya Ofisi na baadhi ya maghala ya kuhifadhia mizigo ambayo kwa sasa yako ndani ya bandari yavunjwe ili kuongeza eneo bandarini. Taarifa hiyo inaonyesha umuhimu wa ofisi za wadau na maghala ya kuhifadhi mizigo kuwa nje ya bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo *TPA* itaendelea kuwapa ofisi wadau wachache ambao uwepo wao ndani ya bandari ni wa lazima kwa utendaji wa kazi zao na ufanisi wa shughuli za bandari. Tunaomba ieleweke kwamba hatua hii inalenga kuinua ubora wa bandari na huduma zinazotolewa kwa wawekezaji na wateja kwa ujumla na wala haimaanishi kutothamini wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) wawekezaji na wadau wa bandari ya Dar es Salaam wanaombwa kuvuta subira mpaka hapo jengo jipya la *One Stop Center* litakapokamilika mwaka 2015 ili wapate nafasi za kupanga kwenye jengo hilo kwa ajili ya ofisi zao kuwa karibu kabisa na bandari.

**MHE. JAKU HASHIM AYUBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante pamoja na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ya kutokidhi swali la msingi nililouliza naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Hii ni kawaida yake Naibu Waziri kuwa

makini katika maswali ya nyongeza kwa ufuatiliaji wake makini.

Hatua gani za dharura zitakachukuliwa hivi sasa wawekezaji hao na walipa kodi wakubwa nchi hii hadi hapo 2015 jengo hilo litakapomalizika? Kuna sababu gani za kuwaondosha wawekezaji hao katika eneo lile na hakuna hatua yoyote iliyofanywa karibu miaka mitatu? Haoni hii ni sawa sawa na nyoka wa mdimu kukaa kwenye mdimu, ndimu hana kazi nazo unakwenda kuchuma anakurukia?

Pili, Serikali inachukua hatua gani ya kuondoa urasimu katika eneo hilo kwa wawekezaji, wakati kuna eneo hilo mwekezaji mmoja tayari anataka kukabidhiwa eneo hilo, lakini mpaka sasa kuna urasimu wa kutokabidhiwa eneo hilo. Ni sababu gani eneo hilo kutokabidhiwa mtu huyo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi kwamba ushauri uliotolewa na mshauri mwelekezi kuhusu kuboresha bandari ya Dar es Salaam ni kwamba maghala na ofisi ambazo si za muhimu kubaki katika bandari zivunjwe ili kutoa nafasi kwa ajili ya kupata nafasi kwa matumizi yenye umuhimu zaidi ndani ya bandari.

Kwa hivyo, Mamlaka ya Bandari imeondoa ofisi zote ambazo inadhani kwamba ili kukidhi haja hazipaswi kuwa ndani ya eneo la bandari. Nimesema pia kwamba zile ofisi ambazo ni lazima zibaki ndani ya

eneo la bandari hizo pekee ndizo zitakazoachwa kubaki ndani ya eneo la bandari.

Kwa hivyo, kama mtu anaamini kwamba anaingia ndani ya hilo kundi la ofisi zenye kulazimika kubaki ndani ya eneo la bandari, basi mamlaka haiwezi kutokumpa ofisi kwa sababu pia na yenyewe pia inamhitaji awepo ndani ya eneo la bandari.

Kuhusu hatua gani zinachukuliwa kwa sasa kwa wale ambao watakuwa ofisi zao zimevunjwa na maghala kuvunjwa, kila jambo jema lina gharama yake hatuwezi tukala mkate halafu tukabaki kuwa nao. Kwa hivyo ndiyo maana tunawaomba wawe wavumilivu tujenge hilo jengo wote watapata ofisi pale watafanya shughuli zao.

Kwa hivi sasa wanaombwa tu watafute maeneo nje kidogo ya bandari waweze kuendesha shughuli zao na jengo hili litakapokamilika basi watakuja watapewa nafasi katika jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari ya urasimu nadhani hakuna asiye shahidi kwamba tunapambana nao kadiri inavyowezekana, tumejitahidi sana urasimu hauko kabisa sasa hivi na ikibainika kwamba yuko mrasimu bado pale bandarini Mheshimiwa Jaku ofisi zetu ziko wazi. *(Makofi)*

Na. 100

## Ujenzi wa Mwalo wa Ikola

**MHE. MOSI S. KAKOSO** aliuliza:-

Mradi wa Mwalo katika kijiji cha Ikola umekwama kwa muda mrefu sasa:-

(a) Je, ni shughuli gani zilizofanya mrafi huo ukwame?

(b) Je, wananchi wameshirikishwa vipi katika utekelezaji wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza *program* shirikishi ya uwiano wa usimamizi wa *program* ya kikanda na maendeleo ya Ziwa Tanganyika *The Lake* Tanganyika *Integrated Regional Development Programme (PRODAP)* amb ayo imeanza 2004 na inatarajiwa kukamilika 2013, *program* yenye lengo la kuboresha usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi na kuimarisha miundombinu ya uvuvi katika ukanda wa Ziwa Tanganyika kwa mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa ili kuinua hali ya maisha ya jamii.

Mojawapo ya kazi zilizo ainishwa katika *program* hiyo ni ujenzi wa Mwalo wa kisasa wa kupokelea samaki katika kijiji cha Ikola, kwenye Halmashauri ya Wilaya Mpanda Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa Mwalo wa kupokelea samaki wa Ikola haujakwama. Hadi hivi sasa, michoro ya Mwalo huo imekamilika na mzabuni wa ujenzi wa Mwalo huo ameshapatikana kupitia zabuni iliyofanyiwa tathmini na kupitishwa na mfadhili kwa maana Benki ya Maendeleo ya Afrika tarehe 24 Februari, 2013.

Aidha, tayari mkandarasi ameshakabidhiwa eneo la ujenzi wa Mwalo wa Ikola na kazi ya ujenzi imeshaanza kazi itakayogharimu jumla ya shilingi milioni 791,319,400 na wameshaanza ambapo kiwango cha ujenzi kimefikia asilimia 25.

Kazi iliyofanyika ni kumwaga jamvi na mkandarasi anasubiri jamvi hilo likauke huku akiendelea kufyatua matofali, ambapo idadi ya matofali imeshafikia takribani nusu ya idadi inayohitajika kwa ajili ya ujenzi huo. Mkataba wa ujenzi wa Mwalo huo ni mkataba wa miezi sita na ujenzi unatarajia kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2013.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa walengwa na watumiaji wa Mwalo ni wananchi, wananchi na viongozi wa halmashauri hushirikishwa kikamilifu katika mchakato mzima wa Mwalo kwamba

uboreshwe katika wilaya tarafa na kata, mchakato huo huzingatia vigezo maalum ama *criteria* katika uteuzi wa mwalo.

Halmashauri ya Mpanda Vijijini na wananchi wa Ikola wamekuwa wakikishirikishwa kikamilifu katika hatua zote za awali. Aidha, halmashauri na wananchi ndiyo watakuwa wasimamizi na waendeshaji wa shughuli za Mwalo huu kupitia utaratibu wa Halmashauri ya Mpanda Vijijini.

**MHE. MOSI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mzabuni aliyepewa ujenzi wa Mwalo katika kijiji cha Ikola ndiye huyo huyo aliyepewa tenda ya kujenga Mialo mingine katika mkoa wa Rukwa na Kigoma. Kwa nini Serikali isiweze kutofautisha kuwapa tenda ili waweze kumaliza miradi katika muda uliopangwa?

Mbili, kwa kuwa mradi wa *PRODAP* ulikuwa sambamba na kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo katika maeneo ya kijiji cha Ikola na Karema, hasa kuwawezesha kuwapa nyenzo za uvuvi, wavuvi wadogo wadogo kupitia vikundi vyao.

Je, Serikali imejipanga vipi kuwawezesha wavuvi hao wadogo wadogo ili waweze kumudu na kutumia fursa itakayokuwa imepatikana kwa ajili ya kukamilika ujenzi wa Mwalo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Nyongeza ya Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

(a) Mialo inayojengwa ni minne, miwili ipo kwenye Mkoa wa Kigoma na huo mmoja uliopo Mpanda Vijijini na Mwalo mwingine upo Nkasi. Wakandarasi waliopewa kazi hizi ni wakandarasi wanne tofauti. Kwa hiyo, Mwalo wa Kirando uliopo Nkasi ni Sukson *Building Construction*, huo wa Ikola mkandarasi ni Mwizobe *Builders* na kwa hiyo, ya Kigoma Kandarasi ni tofauti.

Kwa hiyo, tunatarajia kwamba mkandarasi aliyepewa kazi hiyo hatachukua muda mrefu maana *contract* aliyonayo ni hiyo tu peke yake wa Mwalo wa Ikola.

(b) Kuhusu mradi huu kuwezesha wavuvi wadogo wadogo naomba tu nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba vitu vilivyopangwa ni miundombinu zaidi maana kuna barabara, kuna ujenzi katika shule Zahanati na miradi mingine ya miundombinu lakini kwa upande wa kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo, *component* iliyokuwa kwenye mradi ni moja tu ambayo ni ya mafunzo ama *training.*

Jitihada nyingine za kuwajengea uwezo zitapangwa ki-Wizara kwa kuwa mradi huu haukuwa na *component* hiyo.

Na. 101

## Uhimilishaji Mifugo (Ng'ombe)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais amekuwa akihimiza mara nyingi uhimilishaji wa mifugo (ng'ombe) ili kupata mifugo bora ya kisasa itakayoweza kumuongezea mwananchi kipato na Taifa kwa ujumla:-

Je, ni kwa nini zoezi hilo linasuasua?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele kuhimiza uhamilishaji wa mifugo hapa nchini ili kuongeza tija kwa mifugo yetu na kuwaongezea wafugaji na nchi kipato.

Katika kutekeleza maagizo hayo Wizara yangu imeimarisha kituo cha *NAIC* kilichopo Arusha ambapo idadi ya madume imeongezwa kutoka 22 mwaka 2005 hadi madume 30 mwaka 2013 na hivyo kuwezesha

kituo kuzalisha dozi 168,000 za mbegu kwa mwaka 2012/2013.

Aidha, hali hiyo imewezesha kuongezeka kwa ng'ombe waliopandishwa kwa njia ya uhamilishaji kutoka ng'ombe 46,530 mwaka 2005/2006 hadi ng'ombe 98,340 mwaka 2012/2013.

Wizara yangu pia imeanzisha vituo vya kanda vya uhamilishaji vya Kibaha kwa ukanda wa Mashariki uliopo mkoani Pwani, Nzuguni iliyopo Dodoma, Mwanza pia kuna kituo cha Kanda, Uyole Mbeya na Lindi.

Pia, vituo viwili vidogo vya uhamilishaji moja kimefunguliwa Tanga na nyingine Tabora ambavyo vimeanzishwa ili kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhamilishaji. Vituo hivyo vya kanda na vituo vya *NAIC – Usa River* vinaendelea kuimarishwa kwa kuvipatia vifaa vya kuhifadhi na kusambaza mbegu bora.

Katika mwaka 2012/2013 Wizara imeanza ujenzi wa kituo kikubwa cha pili kule *Sao Hill,* Mufindi – Mkoani Iringa, ili kusaidiana na kile cha *NAIC* kilichopo Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba wataalam wa kutoa huduma hii wanapatikana kwa wingi nchini Wizara yangu imeanzisha Chuo cha Uhamilishaji *NAIC* Arusha ili kutoa mafunzo kwa wataalam kutoka kwenye halmashauri zetu na sekta

zetu na watu binafsi. Hadi Juni, mwaka huu 2013 jumla ya wataalam 622 walipatiwa mafunzo.

Aidha, hadi sasa jumla ya halmashauri za wilaya 129 nchini zimeweza kupata vifaa vya Uhamilishaji ikiwemo mitungi ya kuhifadhi mbegu na kimiminika cha naitrojeni, vifaa vya kupandishia ambavyo ni *pistollets, gloves* na *sheaths* na vyombo vya usafiri. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini lengo la Serikali ilikuwa ni kuwafikia wafugaji wadogo ambako vijijini ambao wanafuga ng'ombe wa kienyeji ambao ni kama asilimia 95 ya ng'ombe wote ambao tunao hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi ninavyozungumza hakuna mfugaji ambaye anajua habari ya *NAIC* hana elimu, na hajafikiwa hata kidogo. Lakini tunao maafisa mifugo kila kata.

Je, Serikali kwanini isiwapalekee mbegu hizi na vifaa maafisa wa kata hapa nchini ili kuwasaidia wafugaji wadogo wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kituo cha *NAIC* kimeonyesha kutokutoa mbegu ambazo hazina ubora hata kidogo, na hiyo ni kutokana na kwamba hawana mitambo ya kisasa, wananchi wanawajibika kuagiza mbegu nje ya nchi ikiwemo Kenya, Uholanzi, Afrika ya

Kusini, ambayo gharama yake uanzia 20,000 na kuendelea.

Je, Serikali inasemaje, ni kwanini isitoe ruzuku kwa wafugaji wadogo wadogo wa Kongwa na wa Karagwe na sehemu zingine ili waweze kupata mbegu zilizo bora kutoka nje ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa swali nzuri sana, Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ole-Nangoro, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja nimetoa katika majibu yangu ya msingi idadi ya wataalam waliofundishwa kutoka kwenye halmashauri zetu ambao nimesema jumla yake 622.

Unachosema Mheshimiwa Mbunge ni sahihi, lakini ni matarajio yetu kama Wizara kwamba hawa waliofundishwa kutoka halmashauri wao ndiyo watakuwa walimu watakaofundisha hawa maafisa wengine waliopo kwenye ngazi za kata ili na hao nao waweze kutoa huduma hiyo ya uhamilishaji katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili hakuna haja kwa wafugaji kuagiza mbegu kutoka nje, kwa sababu madume tunayoyatumia ya mbegu yaliyoko *NAIC* manane ni aina ya *frajion* yaliyotoka Afrika ya Kusini kuna yaliyotoka Kenya, aina ya Asia, madume nane na madume na wawili kutoka Iringa, lakini pia kuna *Borani,*

*Sahiwal, Jese* na *Sementori* ambao hawa tumewaagiza kutoka Kenya.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa sasa mbegu zinazopatikana kwa kweli tayari Wizara imefanya kazi kubwa ya kuleta mbegu hizi karibu na wafugaji.

Lakini niseme pia teknolojia inazidi kubadilika na kama Wizara tunajaribu kujipanga kwenda katika hatua nyingine *endrio transfer* lakini pia sex sea men kama teknolojia ambayo itakuwa ni nzuri zaidi tuweze hata mfugaji hata anapopandisha aweze kuamua kwamba atawazalisha ama madume tupu ama ni mitamba kwa mtindo huu wa *sex sea men*.

Na. 102

**Kuwezesha wanamichezo wenye Ulemavu**

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA** aliuliza:-

Wanamichezo wenye ulemavu hasa michezo ya *Para-Olimpic* wamekuwa wakifanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa licha ya changamoto nyingi zinazokabili timu zao wakati wa maandalizi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwawezesha wananchi hao ili kuondokana na changamoto hizo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba timu ya wanamichezo walemavu pamoja na vikundi vya michezo mingine vimekuwa vikikabiliwa na changamoto wakati wa maandalizi kutokana na uwezo mdogo wa fedha.

Pia ni kweli kwamba timu za wanamichezo zenye ulemavu zimekuwa zikifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Aidha, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali nayo imekuwa vigumu kusaidia kikamilifu maandalizi na ushiriki wa timu zetu katika michezo ya kimataifa.

Pamoja na changamoto hizo, Wizara yangu imeendelea kufanya jitihada za kukabiliana nazo kama ifuatavyo:-

(i) Kusaidia fursa za mafunzo kwa Watanzania ili wawe Makocha, viongozi na waamuzi bora wa michezo ya watu wenye ulemavu.

(ii) Kusaidia upatikanaji wa fursa za miradi ya maendeleo ambayo husaidia rasilimali ambazo hupunguza changamoto ambazo watu wenye mahitaji maalum wanakutana nazo katika kushiriki michezo ya Kitaifa na Kimataifa.

(iii) Kuwashirikisha katika *program* mbalimbali za maendeleo ya michezo ambazo zinalenga katika kujenga uwezo wa Watanzania kwa ujumla katika kujiendesha kimichezo katika ngazi zote za kitaifa na kimataifa.

(iv) Kulipia gharama za usafiri na mahitaji mengine ya msingi ya timu hizo zinaposhiriki kwenye michezo ya Afrika, Jumuiya ya Madola na ile ya Olimpiki.

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi pamojan a majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali ya kuuliza.

Je, fursa ngapi mpaka sasa hivi za miradi ya maendeleo ambayo timu hizi zimepewa ili ziweze kusaidia kupata hizo rasilimali kama alivyosema?

Je, Serikali haioni haja ya kuwaenzi wachezaji hawa kila wanapofanikiwa kwa njia yoyote ile ili kuendelea kuwapa moyo kwa sababu mwenye ulemavu si sawa na mzima na anapo-*perform* vizuri angalau anajisikia na yeye yumo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA NA UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, ni kwamba Serikali inafanya jitihada za upatikanaji wa fursa za miradi ya maendeleo ikiwemo kushirikiana na sekta

binafsi, Serikali yenyewe, wafadhili na vyama vya michezo. Hili nataka niwathibitishie kwamba, mafunzo mbalimbali kama nilivyosema ya Walimu yatatolewa ili kuwaendeleza wanamichezo wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali inapokea ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge ya kuwaenzi wanamichezo hawa ambao ni walemavu. Kwa takwimu zilizopo ni kwamba, kwa michezo ya *Para-Olympic* iliyofanyika mwaka jana, Tanzania ilipata mshiriki mmoja wa kurusha mkuki na kisahani na hatukuweza kupata medali yoyote, lakini ushauri wake tumeuzingatia.

Na. 103

## Mauaji ya Wanafunzi Mbeya

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI** aliuliza:-

Mwaka 2000 Jeshi la Polisi Mkoani Mbeya lilihusika na mauaji ya mwanafunzi wa sekondari ya Iyunga, Ndugu Michael Sikupya na hili lilithibitishwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa kwa Hukumu – *Inquest* Na. 152/2003:-

(a) Je, ni nani alichukuliwa hatua katika kesi hiyo?

(b) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kwa mauaji hayo?

(c) Je, Seriklai inasemaje kuhusu kuilipa fidia familia ya Mzee Sikupya ambaye ni Baba Mzazi wa Marehemu aliyehangaika na suala hili zaidi ya miaka 10 bila msaada wowote?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 26 Novemba, 2000 majira ya saa 1.30 usiku, wanafunzi wa shule ya sekondari Iyunga walifanya vurugu na kusababisha uharibifu mkubwa wa majengo na mali za shule kwa kuzichoma moto na kupiga mawe. Kufuatia vurugu hizo, jumla ya wanafunzi 53 walikamatwa na Polisi usiku huo akiwemo Michael Sikupya kwa mahojiano. Akiwa Polisi, gafla hali yake ilibadilika na kuanza kuumwa ambapo alikimbizwa hospitali na kulazwa. Tarehe 3 Desemba, 2000 majira ya saa 5.20 asubuhi alifariki dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uchunguzi wa awali uliyofanywa juu ya kifo hicho ukihusisha jopo la Madaktari, hakuna mtu yeyote aliyechukuliwa hatua za kisheria. Aidha, upelelzi uliendelea ikiwa ni pamoja na Shauri hili kufunguliwa *Inquest* Na. 152/2003 Mahakamani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 14 Aprili, 2011, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya ilitoa maamuzi ya Shauri Na. 152/2003. Kufuatia maamuzi hayo, Timu Maalum ya Uchunguzi ikishirikisha vyombo vitano vya upelelezi iliundwa na tayari imekamilisha upelelezi wake. Kwa sasa taarifa ya uchunguzi huo inaandaliwa na mara itakapokamilika itatolewa hadharani. Aidha, hatua stahiki kwa mujibu wa mapendekezo ya Tume hiyo zitachukuliwa kwa wale wote watakaobainika kuhusika na mauaji haya.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haiwezi kusema lolote juu ya fidia. Suala hili ni la kisheria ambalo ni vema likasubiri maamuzi ya Mahakama kwa watuhumiwa watakaokamatwa na kufikishwa Mahakamani kwa kesi ya mauaji.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naibu Waziri anasema kwamba, suala hili limeshughulikiwa ikiwemo kwenda Mahakamani utafikiri kwamba Serikali ilihusika kwenda Mahakamani na wakati familia ndiyo ilipeleka suala hili Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Mahakama iliamua kwamba Jeshi la Polisi lilihusika na mauaji ya

Michael Sikupya, maana yake uchunguzi ulifanyika na ushahidi ulikuwepo. Sasa kwa nini mpaka leo hakuna hata Askari mmoja aliyehusika ambaye amekamatwa na kufunguliwa mashtaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa vile Mahakama ilithibitisha kuhusika kwa Serikali kupitia Askari ambao ni waajiriwa wake katika suala la kifo cha Michael Sikupya, ni sheria ipi inayowezesha Serikali kukwepa wajibu wa kuilipa fidia familia ya marehemu Michael Sikupya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, *Inquest* ilisema Jeshi la Polisi lilaumiwe lakini hiyo haikuwa toshelevu kwa sababu haikuweza ku-*point* nani achukuliwe hatua. Uundwaji wa hili jopo ambalo limefanya uchunguzi ndilo ambalo litasema nani na nani na kwa vipi anahusika ili kurahisisha hatua kumwendea yule hasa anayehusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fidia, ni kwamba kwa sababu lengo ni kuwachukulia hatua hawa watu kwa kuwafikisha Mahakamani na Mahakama inaweza kusema pamoja na mambo mengine walipwe fidia, kwa hiyo, ni kheri tukasubiri Mahakama itamuaje, halafu ndiyo tuanze kuzungumza haja ya fidia kama ipo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa sababu swali langu ni la msingi

sana ningeomba kama ungenisaidia kumwambia Waziri Mkuu anisikilize.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Askari kuuwa raia, ni suala *serious* na vifo ambavyo vimetokana na Askari kuuwa raia siyo kimoja, viwili au vitatu. Jana nilimwuliza Naibu Waziri swali la msingi, ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi cha kuunda Tume Huru ya Mahakama, kuchunguza na hatimaye kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaohusika na mauaji haya? Jambo ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwa lugha nyepesi sana, tena ya kejeli, kwamba Serikali haijaona umuhimu wa kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, raia wanauwawa, Serikali haioni kwamba kuna sababu za kuunda Tume Huru wakati raia wanakufa, vifo vinatokea na vinaendelea kutokea? Awali nilishawahi kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili, naye alitoa ahadi ya Serikali kuunda Tume Huru za Kimahakama ili zichunguze vifo hivi vyenye utata ambavyo vimekuwepo vingi, vya muda mrefu na vinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, Mheshimiwa Waziri, ni mpaka watakapouwawa ndugu zenu viongozi wa Serikali na Mawazri, watoto wenu pengine, ndiyo mtaona kwamba hili suala ni *serious* na linatakiwa kuchukuliwa hatua? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna

matukio mengi sasa hivi yanajitokeza ya mauaji ya raia yanayotokea kwenye mapambano au kwenye vurugu ambazo zinasababishwa na raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mambo ambayo tumeyaeleza mara nyingi ni kwamba kila linapotokea, tunaunda *Task Force* ya kuchunguza pamoja na kufukuzwa kazi pale ambapo tutajua mtu aliyehusika. Zaidi ya kuwafukuza kazi, watu hawa tunawapeleka Mahakamani ambavyo ndiyo vyombo vyetu tulivyoviweka Kikatiba vitoe haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtu tumempata, tumemjua, tumemfukuza kazi, tukampeleka Mahakamani, hapa kuna tatizo gani la haki ambayo haijatendeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kwamba vyombo hivi vya uchunguzi vinaweza vikaundwa na Serikali, wakati Serikali bado ina imani na vyombo vyake, bado pia upande wa raia wanaweza kuunda vyombo kama wanahisi haki haikutendeka ipasavyo. *(Makofi)*

Na. 104

## Utafiti wa Dhahabu Kwenye Maeneo Mbalimbali Mbongwe

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwepo na utafiti wa Madini ya Dhahabu maeneo mbalimbali katika Wilaya

ya Mbogwe hususani maeneo ya Nyakafuru, Lugunga na Bukandwe:-

(a) Je, ni lini Kampuni zinazofanya utafiti kwenye maeneo husika zitafungua Migodi kwa uzalishaji rasmi?

(b) Kama Kampuni husika hazina mpango wa kufungua Migodi katika maeneo hayo; je, ni lini Serikali itapunguza maeneo yanayofanyiwa utafiti na kuyagawa kwa wachimbaji wadogo wadogo waweze kuendesha shughuli za uchimbaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino M. Masele, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa maeneo ya Nyakafuru, Lugunga na Bukandwe yaliyopo katika Wilaya ya Bukombe na Kahama, yanajulikana kuwa na madini ya dhahabu. Hadi sasa Kampuni za *Mabangu Mining Limited*, *Resolute* (T) *Limited* na *Vulcan Resources (T) Limited* zinaendelea na shughuli za utafutaji wa madini katika maeneo hayo. Leseni za utafutaji wa madini katika maeneo hayo zilitolewa kwa vipindi mbalimbali kuanzia mwezi Julai mwaka 2005, hadi mwezi Februari mwaka 2013. Utafutaji wa madini unahitaji muda wa kutosha kuweza kubainisha mashapo ya kutosha kabla ya kufikia hatua za upembuzi yakinifu na hatimaye kuanzisha mgodi. Shughuli hizo za utafutaji ni muhimu ili kukusanya

takwimu za kijiolojia, kihaidrojia, kijioteknolojia na pia kufanya upembuzi wa masuala ya uchumi, mazingira na masuala ya jamii kuhusu mradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa na kampuni husika hapo juu, takwimu zilizopatikana hazijitoshelezi kuweza kufungua mgodi. Hata hivyo, kampuni ya *Mabangu Mining Limited* imefikia hatua ya upembuzi yakinifu wa awali, yaani (*pre-feasibility study*) katika eneo la Nyakafuru liloko Wilaya ya Bukombe ambapo kuna takribani wakia 700,000 za mashapo ya adhabu. Kiasi hicho bado ni kidogo na kampuni inahitaji kuendelea na utafutaji wa kina wa madini katika eneo hilo ili kugundua mashapo zaidi. Iwapo mashapo zaidi yatagunduliwa, hadi kufikia wakia 1,000,000, upo uwezekano wa kampuni hyo kuanzisha mgodi katika eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Mabangu Mining Limited* inayoendesha shughuli za utafutaji wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Nyakafuru, inaendelea nautafutaji wa kina wa madini hayo ili kukamilisha upembuzi yakinifu kwa kufanya uchorongaji zaidi wa miamba. Lengo ni kuongeza kiwango cha mashapo katika eneo hilo. Kutokana na malengo hayo, kampuni hiyo imeomba kuongezewa muda yaani *extension* wa leseni yake ya Nyakafuru yenye ukubwa wa kilometa za mraba 4.38 kwa kipindi cha miaka miwili hadi mwaka 2014. Mradi huo unajumuisha pia leseni nyingine zenye ukubwa unaokaribiana na leseni ya Nyakafuru. Iwapo ndani ya kipindi hicho, kampuni haitapata mashapo zaidi

kuiwezesha kuanzisha mgodi, itaachia maeneo hayo ili kuweza kupewa wawekezaji wengine hasa wachimbaji wadogo na wa kati.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wamekuwa wakichimba dhahabu katika nchi hii kwa muda mrefu. Naomba kujua Serikali inawasaidiaje wachimbaji hawa wadogo kupata masoko ya bidhaa zao hapahapa nchini na nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa madini ya dhahabu yana mchango mkubwa katika ukuzaji wa uchumi na kustahamilisha sarafu ya nchi. Serikali ina mpango gani sasa wa kununua dhahabu na kuiweka katika Hazina ya Serikali, ili kuweza kuwa na akiba ya kutosha katika nchi yetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la masoko kwa wachimbaji wadogo, ni kweli kwamba Serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kwamba kunakuwa na masoko rasmi kwa ajili ya wachimbaji wadogo ndani ya nchi, lakini wote tunatambua kwamba namna ya ku-*control* hawa wachimbaji wadogo ni kazi kweli. Tumejitahidi na tumekuwa tukifanya semina mbalimbali nao na tumekuwa tukiita maonyesho makubwa nchini hata maonyesho ya Kimataifa kuwaita wanunuaji wa madini

wanaotoka duniani kote, iliwaweze kupata *contact* nao. Hii imesaidia wao kupata *contact* kwa maana ya soko la nje. Kwa soko la ndani, tutajitahidi na tunafanya jitihada kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanakuwa na soko linaloeleweka na hii jitihada inaonekana inaweza ikazaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kununua madini, itakumbukwa kwamba tumewahi kufanya hivyo siku za nyuma nchini na wote tunatambua matatizo yaliyotokea. Wazo ni zuri, tunalichukua tuone ni namna gani tunaweza tukafanya hivyo, kwa sababu pia ni kweli kwamba ni rasilimali muhimu inayoweza ikafanya sarafu yetu ikapanda kwa sababu tutakuwa tuna thamani hizo katika mabenki yetu.

Na. 105

**Gharama za Uunganishaji wa Umeme**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Ili kupanua wigo kwa wananchi kuunganishiwa umeme kwa haraka ni muhimu kuwa na vyanzo mbadala vya fedha za kugharamia miradi ya umeme zaidi ya bajeti ya Serikali ambayo hutegemea kodi na misaada ya kibajeti:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuweka mfumo ambao utawezesha wateja kugharamia nguzo na vifaa vingine wakati wa kuvuta umeme fedha hizo zihesabike kama kiwango walicholipia umeme *(pre-paid electricity*) ili

kufidia gharama hizo kwani miundombinu hiyo hubaki kuwa mali ya *TANESCO*?

(b) Je, kwa nini kusiwepo utaratibu wa kutoa mikopo kwa ajili ya kuunganisha umeme na kuweka mfumo wa kurejesha sehemu ya gharama kupitia malipo ya wateja wengine watakaojiunga na mtandao husika?

(c) Je, Serikali itatekeleza lini maelezo yaliyotolewa tarehe 1/4/2011 kuhusu *TANESCO* kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wateja na kuingiza gharama kwenye ankara kidogo kidogo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John J. Mnyika, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, gharama anazolipa mteja katika kuunganishiwa umeme, huwezesha *TANESCO* kurejesha gharama zilizotumika kununua vifaa pamoja na nguvu kazi yaani *labour charge* na utunzaji yaani *maintenance* kwa vifaa hivyo katika kipindi chote cha uhai wa njia ya umeme. Hivyo, wateja wataendelea kuchangia gharama za kuunganishiwa umeme ili kuliwezesha Shirika kumudu kuunganisha wateja wapya wengi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* imeingia mkataba na Benki ya Akiba yaani *ACB* kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wateja wanaotaka kuunganishiwa umeme. Mpango huu ujulikanao kama *ACB Umeme Loan,* ulizinduliwa rasmi tarehe 2 Juni 2011. Aidha, huduma hii ya mikopo ilibuniwa na benki ya Akiba kwa kushirikiana na *TANESCO*, inalenga kutoa mikopo ya kuunganishiwa umeme itakayorudishwa kati ya miezi sita hadi miezi 24. Mpango huu pia unatoa mikopo kwa Wakandarasi wa kazi za umeme wa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia Mikoa itakayonufaika na mikopo hii ni ile yenye matawi ya benki ya *Akiba Commercial Bank*. Mipango inaendelea kufanywa ili kuingia mikataba na benki nyingine na kuwezesha wateja wengi zaidi kupata mikopo hiyo. Aidha, suala la kurejeshewa sehemu za gharama kupitia malipo ya wateja watakaojiunga na mtandao husika, linaendelea kufanyiwa kazi kwa kuwahusisha wadau mbalimbali kwa kuzingatia Kanuni za Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijijini yaani *REA* ilianza kutekeleza mpango wa kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wateja, kuanzia mwezi Januari mwaka 2013, kama ilivyotangazwa. Kwa mfano, gharama za kuunganisha umeme kwa umbali usiozidi mita 30 kwa maana ya njia ya *single fence* bila kuhitaji nguzo, imeshuka kutoka Sh.455,108/- hadi

Sh.177,000/- kwa vijijini na Sh.320,960/- kwa mjini. Aidha, kwa wateja wanaohitaji nguzo moja kuunganishwa umeme, gharama imeshuka kutoka Sh.1,351,884/- hadi Sh.337,740 kwa vijijini na Sh.515,618/- kwa mjini.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la kuingiza gharama kwenye Ankara kidogo kidogo, litawezekana tu pale ambapo mfumo wa utoaji bili za umeme utawezesha mpango huo. Baada ya Shirika kupunguza gharama za umeme kwa asilimia zaidi ya hamsini, wateja wamepewa unafuu wa kulipa gharama hizo kwa awamu tatu kabla ya kuunganishiwa umeme.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni kati ya Wizara zilizoko kwenye orodha ya Wizara za Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Suala la kuunganisha umeme, ni kati ya malengo ambayo Wizara ndani ya mikataba imewekewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili utaona kwenye swali la msingi, nimeanza kulihoji mwaka 2011. Imechukua miaka miwili mpaka Januari 2013, kwa jambo moja tu la kushusha gharama za umeme. Mambo mengine yote ya kuingiza bili taratibu kwenye ankara na kubadili mfumo hayajatekelezwa. Aidha, jambo la kulipia gharama kidogokidogo kwa wateja waliounganisha nguzo kwa wengine tunaahidiwa ahadi mpya mpaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Wizara hii inapaswa kutekeleza mpango chini ya Matokeo

Makubwa Sasa. Je, Wizara iko tayari kuleta Bungeni, mkataba ambao Wizara imeingia juu ya masuala haya na mengine ili kukiwa na ucheleweshaji kama huu Bunge liweze kuchukua hatua kwa niaba ya wananchi kwa kuiwajibisha Wizara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pamoja na tangazo la kupunguza gharama za kuunganisha umeme, ukweli ni kwamba katika Mikoa mbalimbali ambayo nimezungukia na hata katika Jimbo la Ubungo ambalo ni jirani kabisa na Makao Makuu ya *TANESCO*, ukienda maeneo ya King'azi, Malambamawili, Msigwa, Matosa, Kulangwa na maeneo mengine mengi ya pembezoni, tatizo kubwa lililopo ni kwamba hakuna vifaa. Kuna uhaba wa nguzo, uhaba wa nyaya na *transformer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari pamoja na kwamba matatizo haya ni ya nchi nzima, kuongozana na mimi katika Jimbo la Ubungo kufuatilia ili hayo matokeo makubwa ya haraka yaonekane kwa haraka kwa wananchi kupata umeme, siyo Ubungo tu bali na maeneo mengine nchini?

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo, wote mpo Dar es Salaam, mpo tayari kuongozana?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara yetu ipo kwenye kundi la Wizara ambazo zinatakiwa kutoa matokeo ya haraka

na kwamba katika mpango wa kuwaunganishia umeme wananchi kwa idadi kubwa ni sehemu ya matokeo hayo. Nichukue nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba tunaendelea vizuri sana na tumekuwa kwa kweli tukipambana kwa kiasi kikubwa kutatua hii changamoto ya upungufu wa vifaa na changamoto nyingine katika kuhakikisha kwamba tunawafungia umeme wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa hapa ni kwamba kutoka mwezi Januari 2011 hadi sasa, tumewafungia wateja wengi umeme kuliko wakati mwingine wowote tangu tumepata uhuru wa nchi yetu. Kutoka mwaka 2012 mwezi Mei hadi sasa tumewafungia umeme wateja zaidi ya 150,000 kitu ambacho hakijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kweli kwamba matokeo ya haraka yatakuja na kubwa tu hapa ni changamoto zilizopo kwamba baada ya kupunguza bei, tumepata wateja wengi na kwamba uwezo wa *TANESCO* ulikuwa bado haujawa vizuri lakini kubwa ambalo tumelifanya katika bajeti tuliyoipitisha juzi, ni kwamba tumejaribu kujenga uwezo mkubwa wa *TANESCO* na kwamba sasa watajitahidi kadri inavyowezekana kuanzia mwezi huu, upungufu unaousema Mheshimiwa Mnyika kwamba umeonekana katika maeneo mbalimbali ya nchi na sisi tunaufahamu wala hatuhitaji kuleta mkataba hapa Bungeni tuje tueleze tena, hapa kinachotakiwa ni kutekeleza tu yale ambayo ni changamoto za kila siku

kwa sababu wanajitokeza wateja wengi na hili ni soko na sisi tunajitahidi na ndiyo maana tunafikiria hata kuweza kutenga *TANESCO* ili iweze kuwa na kampuni nyingine kwa ajili ya *distribution*. Hii yote ni katika ku-*mitigate* ule mzigo ambao upo unaielemea *TANESCO*. Nichukue nafasi hii kueleza kwamba tumefanya makubwa katika muda huu kuwaunganishia wateja wengi kuliko kipindi chochote kile tangu tumepata uhuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkitazama muda wetu, mtaona hauko upande wetu na kwa jinsi hiyo tunaendelea na matangazo.

Tangazo la kwanza ni wanafunzi 67 kutoka shule ya sekondari ya Hagafilo, Njombe, pale mlipo wanafunzi simameni. Karibuni sana wanafunzi kutoka Njombe, karibuni sana wanafunzi pamoja na Walimu wenu, mnapendeza sana na tunawakaribisha mjifunze masuala ya Bunge. Karibuni sana kutoka Njombe. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 80 kutoka shule ya sekondari ya Kitungwa, natumaini *gallery* zimejaa hivyo wanaweza wakawa wako *basement*.

Tuna wanafunzi 24 na viongozi 18 kutoka shule ya msingi Chiligati, Manyoni Singida. Wapo wanafunzi wa darasa la saba 24, Walimu 11 na viongozi wa Kamati ya Shule saba. Shule hii ya msingi kule Manyoni Singida inaitwa shule ya msingi Chiligati. Karibuni sana na

Mheshimiwa Chiligati anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. (*Makofi*)

Wapo wanachama wa Chama cha Waigizaji Mkoa wa Dodoma, karibuni sana waigizaji Mkoa wa Dodoma, tunashukuru kuwaona na karibuni Kongwa pia. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo 31 ambao ni wageni wa Mheshimiwa Anne K. Malecela, kutoka Jimbo la Same Mashariki, wakiongozwa na Katibu Msaidizi CCM Wilaya Marisha Salim ambao ni Makatibu Kata 30 kutoka Same Mashariki kuja kutembelea Bunge. Karibuni sana ndugu zetu wa Same Mashariki, Mheshimiwa Anne Kilango ni mpiganaji, anafanya kazi kubwa sana hapa Bungeni na sisi tunaamini kama Makatibu Kata 30 katika Jimbo hilo basi hakuna wasiwasi kabisa. Kwa hiyo, mwaka 2015 ni kama amesimama tu, tupelekeeni salamu Same Mashariki! *(Makofi)*

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mwenyekiti wa *TAPAFE* ambaye anaitwa Dkt. Wilson Matekenya. Nafikiri ni yule aliyesimama, yeye ni *Sub Saharan Region Director for Climate Parliament*, anatoka Zimbabwe lakini anafanya kazi *South Africa. Climate Parliament* ni mtandao wa Wabunge wenye lengo la kudhibiti athari ya mabadiliko ya tabia nchi na kuongeza nishati kupitia *renewable energy.* Amekuja kukutana na Chama cha Wabunge Marafiki wa Mazingira ambao Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Hilda Ngoye. *(Makofi)*

Sasa naomba kuwatambulisha watu wawili muhimu sana kipekee, kwanza ni Bwana Francis Cheka pale alipo. *(Makofi)*

Huyo ndiye Bwana Francis Cheka, Bingwa wa Shirikisho la Ngumi Duniani yaani *World Boxing Federation,* uzito wa kati. *(Makofi)*

Karibu sana pamoja na mama watoto, naomba asimame na yeye hapo karibu yako, ahsante sana mama, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Francis Cheka alimshinda Mmarekani Phill Williams katika pambano la *rounds* 12 na kutwaa ubingwa huo wa *Word Boxing Federation* uzito wa kati. *(Makofi)*

Nakushukuru sana kwa niaba ya Watanzania wote kwani tunajivunia mafanikio haya na kwa kweli mnatubeba katika nyanja hii ya michezo. Tunasema ahsante sana na uendelee zaidi kwani tunategemea mataji zaidi kutoka kwako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimtambulishe mpiganaji mwingine wa *Boxing*, Ndugu Francis Miyeyusho. *(Makofi)*

Karibu sana na mama pia kama yupo. Ahsante sana na tunashukuru sana. Yeye ni Bingwa wa Mabara wa *WBF,* uzito wa *Bantam*. Wote wapo pamoja na mapromota wao na kampuni zinazohusika na

mapambano hayo, Bwana Bawazir na Ndugu Katherine Mitiri. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Baada ya hayo, sasa naomba nitoe matangazo ya kazi. Mheshimiwa James Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba saa 7.15 mchana Kamati hiyo ikutane katika ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 7.15 mchana katika ukumbi wa *basement*.

Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane katika ukumbi wa Pius Msekwa C, saa 7.15 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa naangalia kumbukumbu zangu hapa, nikaona kuna Mbunge leo ni *happy birthday* yake, naye si mwingine isipokuwa ni Mheshimiwa Ummy Mwalim. *(Makofi)*

Tunakupongeza sana Mheshimiwa, leo ni siku yako. Kwa hiyo, Mbunge atakayeweza baadaye kipande cha keki siyo mbaya kwa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, niseme tu kwamba kuna baadhi ya Miongozo ambayo ilitolewa jana, nitaitolea ufafanuzi wake baadaye

kidogo kabla ya kuahirisha Bunge mchana wa leo. Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013 *[The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2013]*

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MWONGOZO WA SPIKA

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama kuomba Mwongozo wa Kiti)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu, kabla hujaendelea, subiri kidogo, kuna Waheshimiwa wamesimama kuomba Miongozo nao ni Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Waziri wa Nchi na Mheshimiwa Jenista. Kuna ambaye sijamtaja? Ahsante sana. Tuanze na Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1) na Kanuni ya 87(1).

**NAIBU SPIKA:** Tusomee.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya

hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo imeshapitishwa, wakati wa mchakato wake ililazimika watoa maoni au wadau waende sehemu mbalimbali ikiwemo Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kuna wakati ilionekana kama kwenda Zanzibar ni kosa, lakini ikafika mahali, ikaenda ikapata maoni na matokeo yake tukapata Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Kwa hiyo, ilipaswa Sheria hiihii inapotaka kufanyiwa mabadiliko iende kulekule Zanzibar kwa sababu Sheria ni ileile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha, Kamati inayohusika na Katiba, Sheria na Utawala, Zanzibar haikwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayezungumza hapa ni Mjumbe wa Kamati hiyo na Kamati ilikuwa na utashi wa kwenda, ukichukua historia ya Mabadiliko ya Katiba utaona Wajumbe waliounda Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba ilikuwa ina watu saba kutoka sehemu zote mbili za Jamhuri. Kwa hiyo, Kamati iliona umuhimu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kamati tuliitwa Dar es Salaam tarehe 27, ratiba ambayo tumeikuta,

iliyotayarishwa, halikuwepo kabisa suala la Kamati kwenda Zanzibar na ratiba ni hii hapa. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Ali Khamis Seif alionyesha Ratiba ya Kamati aliyokuwa anaizungumzia)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukahoji...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kwa heshima kubwa, kwanza hoja yako nimeipokea…

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**WABUNGE FULANI:** Bado hajamaliza.

**NAIBU SPIKA:** Nitaifanyia kazi.

**MBUNGE FULANI:** Tabia gani hii?

**NAIBU SPIKA:** Ni katika upungufu mkubwa sana. Jambo hili limetolewa jana, ni katika yale mambo ambayo nimesema ninayo nitayatolea maelezo baadaye, lakini kwa hoja yako ya kusema kwamba, maana hoja yako ni kutaka mjadala huu uahirishwe, kwa lile la kwenda Zanzibar au kutokwenda Zanzibar limetolewa jana ni katika yale ambayo nitayatolea maamuzi. (*Makofi*)

Kwa hii hoja yako kwamba Bunge hili liahirishwe, hilo nitalifanyia kazi na nimeshalipokea, nitalifanyia kazi

sasa hivi. Labda kama una lingine zaidi ya kuahirishwa? Endelea Mheshimiwa Ali Khamis Seif!

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachokisema ni kuwa, sisi tulipofika pale kuona ratiba hakuna habari ya Zanzibar tukasema tupendekeze...

**NAIBU SPIKA:** Hoja yako ni nini Mheshimiwa?

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Hoja yangu ni kuonyesha kuwa Kamati nayo ilitaka iende Zanzibar na ratiba ikatayarishwa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, hoja ni Kamati ilitaka kwenda Zanzibar?

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Bunge lako liahirishe mjadala huu ili Kamati iende Zanzibar na mjadala huu uahirishwe mpaka Bunge la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hapa Wabunge wa Upinzani walisimama kuunga mkono Hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Ali Khamis Seif)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba mkae.

Mheshimiwa Ali Khamis Seif, ndiyo maana nikasema, hoja yako nimeielewa na ninaiheshimu sana

na nitaifanyia kazi. Hoja yako ni kwamba shughuli za Bunge ziahirishwe kwa sababu ulizozitoa kwa kutumia Kanuni ya 69(1). Kanuni ya 69(1), kwa vile nchi nzima inatufuatilia basi ni vizuri twende pamoja, inasema, Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba mjadala huo sasa uahirishwe, kama alivyofanya Mheshimiwa Ali Khamis Seif, ni sahihi kabisa. Aidha, atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani, sikumsikia akisema.

**WABUNGE FULANI:** Amesema.

**NAIBU SPIKA:** Pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala huo uahirishwe na ametoa sababu zake.

Kanuni ya 69(2) inasema, kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, atakataa kuitoa ili iamuliwe, vinginevyo papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hoja hiyo kadri atakavyoona inafaa. Kwa hiyo, hoja ya namna hii haikuwa na sababu ya ninyi kusimama kuunga mkono bali ni maamuzi ya Kiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Kanuni ya 69(3) inasema, endapo hoja iliyowasilishwa haitapata kibali cha Bunge, mjadala kuhusu hoja hiyo iliyopo mbele ya Bunge utaendelea. *(Makofi)*

Kanuni ya 69(4) inasema, Mbunge yeyote, hii haina uhusiano sana.

Kwa hiyo, nimesema nitaifanyia kazi muda si mrefu, tunaendelea na wengine halafu nitahoji.

**WABUNGE FULANI:** Hoji.

**NAIBU SPIKA:** Nitaifanyia kazi sasa hivi.

Wa pili kati ya waliokuwa wamesimama, tuzichukue hoja zote ili tuzifanyie kazi kwa wakati mmoja. Wa pili ni Mheshimiwa Mkosamali na atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista. Sasa namwita Mheshimiwa Mkosamali!

**WABUNGE FULANI:** Wapo wengine nao walisimama.

**NAIBU SPIKA:** Jamani, nina orodha ya wote waliosimama, hakuna ambaye alisimama hatapata nafasi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 90 pamoja na Kanuni ya 8 na Kanuni ya 5.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnapo-*refer* Makanuni mengi basi twende pamoja taratibu na Wabunge wote wenye Kanuni ni vizuri tukaenda pamoja. *(Kicheko)*

Haya anza na Kanuni ya kwanza kwa kuisoma.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 90 inasema, mtoa hoja anayewasilisha Muswada wa Sheria anaweza kuuondoa Muswada wakati wowote...

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Kanuni ya 90.

**NAIBU SPIKA:** Tisa sifuri? Endelea Kaka.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Wakati wowote kabla ya Bunge kuhojiwa kutoa uamuzi wake, baada ya kutoa taarifa kwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni nyingine ninayoisoma pamoja na hiyo nimesema ni Kanuni ya 8 lakini naomba Kanuni ya 68(7) nisiisome ni ya kuomba Mwongozo najua inafahamika. Kanuni ya 8 inasema, kwa kuzingatia matakwa ya masharti yaliyotolewa na kiapo cha kazi zake, yaani kiongozi anayeongoza Bunge kwa maana ya Spika, Naibu Spika au Mwenyekiti na kwa madhumuni ya utoaji wa uamuzi na uendeshaji wa shughuli za Bunge na kwa haki bila upendeleo, Spika:- (a) ataendesha shughuli za Bunge na kutoa maamuzi kwa haki, uadilifu bila chuki wala upendeleo wowote...*(Makofi)*

Kwa kuongozwa na Katiba, Sheria za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, Maamuzi ya Maspika wa Bunge waliotangulia na pia kwa kuzingatia uzoefu pamoja na desturi za Mabunge mengine yanayofanana na utaratibu wa Kibunge unaofanana na unaofuatwa na Bunge Tanzania. *(Makofi)*

Kipengele (b) kinasema, hatafungwa na msimamo unaowekwa na makubaliano yanayofikiwa na Kamati yoyote ya Chama cha Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kifungu hiki kinakutaka wewe na mtu yeyote atakayekaa hapo kuendesha Bunge kwa uadilifu na siyo kishabikishabiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wangu nakuomba, kwa kuwa wewe uliapa na tumekuweka hapo uwe muadilifu, usiburuzwe na Chama chako, uzingatie Miongozo yote inayotolewa na Vyama vyote, uitoe kwa wakati kwa sababu unavyoi-*prolong,* unakiuka Kanuni hii, unafanya mambo kinyume na uadilifu. Kwa nini usitumie mamlaka uliyopewa kwenye Kanuni ya 5, ukamwagiza mto hoja aondoe hoja kama ambavyo Kanuni ya 90 inasema ili vyama vyote tuweze kuridhika na Watanzania wa pande zote mbili za Muungano waweze kuridhia kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, yako mambo ambayo hayahitaji hata kusubiri au kufikiri sana lakini yako mambo ni mazito yanayohitaji usubiri kidogo, upate ushauri na ndiyo uongozi. Nilisema yale ambayo nilikuwa ninahitaji ushauri, nitayatolea maamuzi muda si mrefu, kwa vile yalikuwa ni mazito yanahitaji kupata ushauri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Binadamu mwenye akili timamu na anayejipenda, hupenda ushauri, hutakurupuka kutaka kutoa majibu ya saa hiyohiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Felix Mkosamali, amesoma Kanuni ya 90, kwamba mtoa hoja anayewasilisha Muswada wa Sheria anaweza kuuondoa Muswada wakati wowote kabla ya Bunge kuhojiwa kutoa uamuzi wake baada ya kutoa taarifa kwa Spika. Mtoa hoja anaweza kuondoa Muswada. Sasa ananitaka mimi niuondoe Muswada na anasema kwa kufanya hivyo ndiyo ninafanya sasa kazi yangu vizuri, kwa hiyo hilo halikubaliki. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji wa tatu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nitatumia

Kanuni hiyohiyo ya 68(7) lakini nitaomba Mwongozo wako kwa hili lifuatalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mjadala unaoendelea Bungeni toka asubuhi, ni kuhusu Sheria ambayo imewekwa Mezani kwa mujibu wa Kanuni na kwa kuwa mtoa hoja ambaye pia ni Serikali, alishatoa taarifa ya kukamilika kwa shughuli hii na ikaingizwa Bungeni tayari kwa kujadiliwa; na kwa kuwa bado kuna malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba majadiliano haya hayajafanyika ingawa Serikali tayari inathibitisha majadiliano haya yamekwishakufanyika, je, Bunge lako, halioni kwamba ni vema ikaipa nafasi Serikali yetu ili kuthibitisha kwamba majadiliano haya yamekwisha kufanyika...*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kuwapa nafasi Watanzania kufahamu kwamba mashauriano hayo yanayodaiwa kwamba hayakufanyika, yamekwisha kufanyika, ili hoja hii iweze kuendelea na hitimisho la hoja hii liweze kufanyika bila kupoteza muda wa shughuli za Bunge katika kujadili mambo ambayo wakati mwingine majibu yako ndani ya Bunge hilihili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hilo pia nalo tutalifanyia kazi baada ya muda si mrefu hapahapa asubuhi ya leo.

Kwa hatua hii na kwa Watanzania wanaofuatilia, mmewasikia baadhi ya Wajumbe wa Kamati iliyochambua Muswada huu, wakisema hiki na kile. Taratibu zetu za Bunge, ni kwamba jambo haliingii hapa kwenye Bunge zima hili ispokuwa limepita kwenye Kamati na Mwenyekiti wa Kamati amemjulisha Spika kwamba kazi ya Kamati imekamilika. Kamati imejiridhisha na kazi yake na ndiyo inapangiwa ratiba hapa. *(Makofi)*

Nilitaka tu Watanzania waelewe kwamba kupangwa kwa shughuli hii ni kutokana na taarifa niliyonayo tena kimaandishi kwamba Kamati imekwishafanya kazi yake, imejiridhisha sasa ni hatua ya Bunge zima kushuhulikia jambo hili. *(Makofi)*

Anayefuata ni Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 63(1)(3)(4)(5) pamoja na Kanuni ya 64(1)(a) za Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachoombea Mwongozo ni kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Naomba zisomwe zote ili twende pamoja.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7) ni ya kuombea Mwongozo inajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(1) inasema, bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(a) inasema, bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kikao cha Bunge cha jana cha tarehe 4 Septemba, 2013, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge lako Tukufu ya Katiba Sheria …

**NAIBU SPIKA:** Bado Kanuni ya 63(3)(4)(5).

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(3) inasema, Mbunge mwingine yeyote anaweza

kusimama mahali pake na kutamka “kuhusu utaratibu” na baada ya kuruhusiwa na Spika, kudai kwamba, Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(4) inasema, Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(5) inasema, bila ya kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala amesema mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, wadau wa Zanzibar, *namely*, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, ilishirikishwa katika kutoa maoni yake juu ya Muswada ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu. Kauli hiyo ni ya uongo na uongo mtupu. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Taarifa!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Taarifa! Taarifa!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Taarifa gani, kuna taarifa gani wakati naomba Mwongozo? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kaa chini.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote mliosimama, naomba mkae chini.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote mliosimama, naomba mkae chini.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwahakikishieni kwamba ninao uwezo mkubwa sana wa kutenda haki. Niko tayari kumsikiliza kila mmoja lakini tujue tu hakuna kinacholala hapa... *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sawasawa.

**NAIBU SPIKA:** Labda ninyi muamue hivyo maana mwisho wa siku wanaoamua siyo Kiti, mimi ni mwongozaji tu, wanaoamua ni ninyi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tupeane nafasi, tusikilizane, la muhimu tulipe nafasi, lisilo la muhimu halina sababu. Tunachoona hapa ni watu wa Kamati fulani kutuchanganya tu kwa mambo ya kwao wao wenyewe. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**NAIBU SPIKA:** Lakini kwa vile wameamua hilo, sasa tuendelee na Mheshimiwa Tundu Lissu, baadaye kidogo uipokee taarifa hiyo kwa sababu imetolewa wakati ukiongea. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema, kauli aliyoitoa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala jana, ilikuwa ni kauli ya uongo. Hakuna Mzanzibar hata mmoja aliyetoa maoni yake kwenye Kamati kuhusiana na Muswada wowote ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nawajibika kutoa ushahidi, ushahidi ni ratiba ya Kamati. Ratiba tuliyokutana nayo siku ya kwanza tulipokaa, ina majina ya wadau 22, wote ni Watanzania Bara. Hakuna mdau hata mmoja wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ratiba hii ya kwanza inaonyesha kwamba tulikuwa na safari ya kwenda Zanzibar, siyo kwenda kupokea maoni ya wadau,

kwenda kutembelea miradi ya *TASAF-Zanzibar*, kutembelea Ofisi ya Makamu wa Rais na kutembelea Ofisi ndogo ya Bunge, siyo kwenda kuzungumza na wadau wa Zanzibar. Hii ni ratiba ya kwanza tuliyokutana nayo. *(Makofi)*

*(Hapa Ratiba ya Kwanza ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilioneshwa Ndani ya Bunge)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ratiba ya pili, baada ya Wajumbe wa Kamati kulalamika kwamba Wazanzibari wako wapi kwenye ratiba hii, tukatengeneza ratiba nyingine hii hapa.

*(Hapa Ratiba ya Pili ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilioneshwa Ndani ya Bunge)*

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ratiba hii iliongeza wadau wengine wa Tanzania Bara saba. Ikaweka wadau wa Zanzibar nane, wako hapa. Ratiba hii inasema tarehe 14 – 16, Kamati ingekwenda Zanzibar kukutana na wadau wa Zanzibar, hatukwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wote waliotajwa kwenye ratiba hizi, hakuna mdau anayeitwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Katika maoni yote iliyopokea Kamati, hakuna Mzanzibari hata mmoja. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Taarifa!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Kaa chini, kaa chini. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu...

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo…

**NAIBU SPIKA:** Kwa heshima zote, utaongea na Kiti.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Na hutawagombeza wala kuwakemea Wabunge wengine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke kuwa kila tunachokifanya Bungeni hapa, tutawajibika nacho kesho.

**WABUNGE FULANI:** Sawa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nchi nzima inaona utovu wa nidhamu wa hali ya juu unaotokea humu ndani.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**NAIBU SPIKA:** Na muwajue Wabunge wenu hivyo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nimewaambia siahirishi kitu hapa, hapa kila mmoja wenu anasomeka katika nchi nzima.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**NAIBU SPIKA:** Kila mmoja wenu anasomeka, eleza hoja yako, heshimu wengine na wengine wakifuata Kanuni, uwe tayari kuwasikiliza, huo ndio utaratibu wetu humu ndani. Hatuwezi kuwa na Bunge la mtu mmoja kusema. Yeye akisema ni sahihi, wakisema wengine si sahihi, Bunge la namna hiyo halipo, siyo Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tundu Lissu, malizia kwa dakika ya mwisho, ulishapewa taarifa, kwa utaratibu wa kawaida ungekaa lakini nimekuheshimu umalizie ili mwenzio akupe taarifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu haya masuala ni ya msingi sana...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Ratiba ya pili kama nilivyosema, ilikuwa na Taasisi za Zanzibar ambazo Kamati ingekwenda kuonana nazo Zanzibar kati ya tarehe 14/8/2013 – 16/8/2013, kwa mujibu wa ratiba hii.

Nao ni Profesa Abdul Shariff, Zanzibar *Law Society,* Zanzibar *Female Lawyers Association, Association of NGOs in Zanzibar*, Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, *State University of Zanzibar* na *Zanzibar University* Tunguu. Hatukuonana nao kwa sababu *some how* tukaambiwa safari ya Zanzibar haipo kwamba Kamati haiwezi kwenda Zanzibar kwa sababu za kiusalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii kauli ya Mwenyekiti wa Kamati kwamba tulisikiliza wadau wa Zanzibar wa Tume ya Uchaguzi ni ya uongo. Naomba Mwongozo wako...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hiyo ndiyo ilikuwa hoja yako tangu mwanzo.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Hatua gani inachukuliwa dhidi ya mwongo huyu.

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana, taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, naomba tuheshimiane na tusikilizane, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitatumia kile kifungu cha taarifa, Kanuni ya 68(7) lakini baada ya hicho na mimi natumia Kanuni ya 64(1)(a) kinachosema kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka Mwongozo wako endapo Mbunge ametoa taarifa zisizo na ukweli, kuwadanganya Watanzania wote na ambazo amezitoa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza. Jana tarehe 4 Septemba, 2013, nilisema hapa kwamba wadau wa Zanzibar waliitwa na wakati ninaendelea kuongea, kuna watu waliondoka kabla sijamaliza. Baada ya kumaliza, wadau wale hawakuwemo humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema kwamba Tume ya Tume ya Uchaguzi tulikuwa nao wakati tunachambua lakini pia nikasema Vyama vya Siasa, Jahazi Asilia, ni chama kilichosajiliwa katika Muungano na walikuja kutoa maoni. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge Walikuwa Wakishangilia kwa Sauti za Juu)*

**NAIBU SPIKA:** *Order, order.*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kilikuja chama cha *ADC*, kikiwakilishwa na Mheshimiwa Shoka, ni miongoni mwa watu...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Nakuomba Mheshimiwa Mnyika ukae chini. Ninaomba nidhamu katika jambo hili, tafadhali sana. Endelea Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna chama cha *ADC*, Mheshimiwa Shoka alikuja kutoa taarifa. Kuna Wabunge wakati wa vikao wanakwepa, wanaenda Mwanza kufanya shughuli zao, Kamati inaendelea na kazi. Hawapo wakati wa kazi ndani ya Bunge. Kamati inachambua, akirudi anawarudisha nyuma, muanzia pale, mbona hukuwepo, si tunakuona kwenye *TV* huko Mwanza unafanya shughuli zako binafsi wakati kazi za Bunge zinaendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni zetu zinasema Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Kuna Mbunge amesimama hapa ametoa taarifa ambazo hazina ukweli. Wakati jana ninaongea, waliondoka na kuacha kusikiliza. Kwa utaratibu, unatakiwa usikilize, utoe hoja na nikasema na naendelea kusema, Jahazi Asilia wamekuja, *ADC* wamekuja mbele ya Kamti kutoa maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo, naomba Meza ipokee taarifa hii hapa ya maoni ya wadau waliokuja mbele ya Kamati na naomba Meza ipokee ratiba tuliyoalika vyama vya siasa vyote vije mbele ya Kamati, naomba mje mpokee. *(Makofi)*

*(Hapa Nyaraka zilizotajwa ziliwasilishwa Mezani)*

**WABUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Naomba Waheshimiwa Wabunge, mkae chini. Orodha yangu ya wachangiaji bado Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

Niseme tu katika hatua hii na katika utendaji wetu wa kazi na kufuatana na Kanuni, taarifa rasmi za Kamati, Meza hii inazipata kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati na hizo ndizo taarifa ambazo tumezipata kwenye Meza. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Sasa tumskilize Waziri wa Nchi ili nifanyie kazi baadhi ya Miongozo ambayo ilikuwa imetoka hapa ili tuweze kusogea hatua ya pili.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nijikite kwenye Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo lakini Kanuni hii nataka isomwe pamoja na Kanuni ya 63(1) na Kanuni …

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Aliyoisoma Mheshimiwa Tundu Lissu ya 64(1)(a) na (d).

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda nirudie kusoma Kanuni ya 63(1) inasema, bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo Mbunge yeyote atakayekuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo tu la kubuni au la kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nisome tena kwa faida ya Bunge lako Kanuni ya 64(1)(a) na (d). Kanuni ya 64(1) inasema, bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:- (a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli lakini (d) hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Masuala ya Sheria na Katiba, Mheshimiwa Tundu Lissu, katika hotuba yake ambayo ilijaribu kuwashawishi baadhi ya wengine hata wakatoka nje na Watanzania wakashawishika

kwamba anayoyasema ni kweli mojawapo ni hili lifuatalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa saba wa hotuba yake alisema kwamba uteuzi wa Wajumbe wa Tume uliofanywa na Rais na ambao unatumiwa kama mfano yaani hapa alikuwa anataka ku-*justify* kwamba Rais huyu asiaminike tena kuteua Wajumbe katika Bunge la Katiba kwa mujibu wa Sheria. Uteuzi wa Wajumbe wa Tume uliofanywa na Rais na ambao unatumiwa kama mfano, wenyewe ulikuwa na walakini mkubwa. Katika hili, kuna ushahidi wa Wawakilishi wa Baraza la Maaskofu Katoliki (*TEC),* Baraza la Kikristo *(CCT)* na Asasi mbalimbali za kiraia zikiwemo za walemavu waliowasilisha maoni ya taasisi zao kwa Kamati ya Muswada huu. Wawakilishi hao waliiambia Kamati kwamba ijapokuwa waliandikiwa na Rais kuwasilisha majina kwa mujibu wa Sheria, Sheria ilitaka kila Taasisi hizi iwasilishe majina matatu siyo uteuzi bali ni majina matatu halafu Rais ateue mmoja kati ya majina hayo.

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kuwasilisha majina ya Wajumbe hao kwa ajili ya kuteuliwa kwenye Tume na walifanya hivyo. Hakuna hata moja, kwa mujibu wa Mheshimiwa Lissu, ya majina yaliyopendekezwa aliyeteuliwa na Rais kuwa Mjumbe wa Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ni kwamba majina haya yalitakiwa yatolewa kwa Mheshimiwa Rais kwa barua...

**MJUMBE FULANI:** Zisome!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Si nimepewa nafasi?

**MBUNGE FULANI:** Wewe endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Badala yake, tena nazungumza kwa lugha ya kistaarabu, sijanywa hata chai wala sina ghadhabu, subirini tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, badala yake Rais aliteua watu aliowaona yeye na washauri wake kuwa wanafaa, hakuzingatia yale majina. Kama taarifa za wadau hao ni za kweli maana yake ni kwamba Rais na Mwenyekiti huyu wa CCM Taifa hawezi kuaminika tena kuteua Wajumbe halisi wa Taasisi hizi katika Bunge Maalum ambalo ndilo litakalojadili na kuipitisha au kuikataa Rasimu ya Katiba Mpya ambayo tayari CCM na wapambe wao wametamka wazi wanaikataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukweli ni huu ninaousema mimi. Sheria ilisema, Rais ataalika na alifanya hivyo, makundi haya yataandika majina matatu, yalifanya na Rais kwa kuzingatia Sheria atateua jina moja katika yale majina matatu yaliyowasilishwa na makundi. Makundi hayakualikwa

kupendekeza majina matatu, hayo yalifanywa na makundi vizuri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Sasa kilichotokea, Mheshimiwa Rais alichokifanya kwa kutimiza wajibu wa sheria na kwa mifano aliyoisema, ndiyo maana nataka kuomba Mwongozo kwamba katika Wajumbe wa Tume waliopo hivi sasa, hiki anachosema *TEC*, kwa barua ya *TEC*, Mama Maria Kashonda, huyu ni miongoni mwa wajumbe watatu walioletwa na *TEC* kwa barua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CCT,* Mama Mkuchu, ni miongoni mwa majina matatu yaliyoletwa kwa barua ya *CCT* kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Barua iko wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Sema tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, *Civil Society*, kwanza niwaambie Wabunge mlitunga Sheria ya kiungwana sana kwa sababu mngeainisha kama wanavyotaka kwamba kila chama cha hiari kilete mjumbe, hata uwanja wa mpira ule wa Dar es Salaam usingetosha. Kwa taarifa nilizonazo leo kutoka kwa Wasajili maana vyama vya hiari nchini vinasajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Leo, Wizara ya Mambo ya Ndani ina vyama vilivyosajiliwa 8,116, kati ya hivyo, vya kidini ni 928 na vya kawaida ni 7,180 na Wizara ya Maendeleo ya Jamii vipo 6,000. Sasa, taasisi hizi kwa barua, *Civil Society* ilileta majina matatu na akateuliwa Ndugu Humphrey Polepole ambaye ni *Chairman* wa *Civil Society. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasomi walileta majina mengi, hayo matatu, lakini Ndugu Kabudi akateuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, BAKWATA, katika barua yao ya majina matatu, Mama Mwantumu Malale aliteuliwa kuwa mwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ile mjue iliwataka Marais hawa wawili kuzingatia uwiano wa kijinsia. Nataka niwapongeze sana hawa akina mama, akina mama hawa niliowataja wame-*shine* katika makundi mengi sana lakini pamoja na makundi haya, majina haya yameonekana kwenye taasisi hizi nilizozisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuishia hapo, asimame mtu mmoja hapa mwakilishi wa chama chochote cha siasa aliyemo humu ndani ambaye kwa barua waliyoleta chama hicho Rais hakuzingatia. CHADEMA, yupo msomi aliyebobea Profesa Baregu ingawa katika barua yao CHADEMA walimweka na Mheshimiwa Tundu Lissu lakini Profesa Baregu ndiye aliyeteuliwa kwa sababu ya sifa zake. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** *Shame, shame!*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha NCCR – Mageuzi, Dkt. Mvungi ameteuliwa na aliletwa na NCCR – Mageuzi. *TLP* yupo na hata *CUF* pia wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kusema ni kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Walemavu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Walemavu ambao wametajwa humu, Mheshimiwa Kwegyir yupo humu ndani, ameletwa kwa barua na Muungano wa Walemavu. Zanzibar, sitaki kusema majina ya Zanzibar lakini Mheshimiwa Kwegyir anawakilisha watu wenye ulemavu wa ngozi lakini Zanzibar wamemleta mama ambaye ana ulemavu wa viungo...

**WABUNGE FULANI:** Haya sasa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Aah, simsemei maana haya nasema ya kwangu Bara, yale ya Zanzibar siwasemei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nachotaka kusema ni kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Mambo ya uwongo, anaongopa, apewe adhabu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Hapa kuna mambo mawili, kwanza taarifa alizozitoa Mheshimiwa Tundu Lissu hapa ndani ...

**WABUNGE FULANI:** Za uwongo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Za kumwaminisha...

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali, naomba ukae chini amalizie.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nitaomba nipewe nafasi ya kumpa taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Za kuwaaminisha Watanzania kwamba Rais Kikwete ni mtu asiyejali sheria, asiyejali

utaratibu, hawezi kusoma wala hawezi kutafakari ni za uongo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo yangu haya na wao walioandika hizo barua wanajua ni barua walipeleka kwa Mheshimiwa Rais na mimi ni kiongozi wa Serikali vilevile najua, barua walizozipeleka kwa Mheshimiwa Rais wanajua, wakatae leo hapa kwamba *TEC* hawakumchagua huyo, *CCT* hawakupeleka jina hilo, BAKWATA hawakupeleka jina hilo, CHADEMA hamkupeleka Profesa, kataeni hapa na mkikataa nitaleta hizi barua ili adhabu iwe kali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, je, kwa kiongozi kama huyu, mwenzangu, rafiki yangu, mwenzetu, msomi, anayetumia fursa ya kalamu yake kudanganya Watanzania na kufitinisha taasisi hizi na Mheshimiwa Rais au na uendeshaji mzima ambao umezingatia sheria, sasa mawili naomba Mwongozo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, taarifa hizi si za kweli …

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MBUNGE FULANI:** Zijibiwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** La pili kwa kutumia jina la Mheshimiwa Rais kwa dhihaka kwa sababu sheria

ilimtaka Mheshimiwa Rais tu azingatie yale majina matatu yanayoletwa kutoka kwenye taasisi, azingatie, ametekeleza, amezingatia na hakuna hata mtu mmoja aliyewekwa kwenye Tume bila kuwa na mwanvuli wenye barua iliyokwenda kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, hatua gani kali zichukuliwe, kali, kwa sababu siyo kosa la kwanza...

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Sawa, safi.

**MBUNGE FULANI:** Siyo la kwanza!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kwa taarifa kama hizi zinazoletwa Bungeni, hazina uhakika, zinazotaka kufitinisha wananchi na Bunge kwa jambo ambalo limetendwa kwa mujibu wa sheria na limesababisha hata majirani wengine, hata jana wengine kutoka nje, kwa taarifa ambazo hawazijui kwa sababu imeandikwa na mtu mmoja, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesimama kutaka kupewa nafasi ya kuongea)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba wote mliosimama mkae chini. Naomba sana mkae chini na niwaombe sana leo kila mmoja ajitahidi kuwa na nidhamu, nawaomba sana.

Sasa Miongozo ya wale waliokuwa wamesimama mwanzo na niliuliza, jamani ni hawa tu?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ni hawa tu, nikawaorodhesha, tumefikia hapo. Sasa kufuatia Miongozo yao, naanza kuifanyia kazi, wale watano na ipo miwili hasa ambayo inahitaji niifanyie kazi kwa haraka.

**MBUNGE FULANI:** Sawa.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Waziri wa Nchi, nitautolea maelezo kabla ya saa saba kufika. Mwongozo wa Mheshimiwa Jenista, nakuomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama una cha kusema kuhusu ushiriki wa Zanzibar halafu tutakwenda na Mwongozo wa Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Muswada huu ambao uko mbele ya Bunge na ushiriki wa Serikali ya Zanzibar…

**MBUNGE FULANI:** Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona Waheshimiwa Wabunge wanataka nizungumze vitu vingine, ninaweza kuvizungumza lakini najielekeza tu kwenye Serikali lakini kwenye tafsiri ya Ibara tutafika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliiandikia Serikali ya Zanzibar na kupeleka Muswada huu kwao na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alituletea mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba mwezi Mei na mimi nikakiri barua nikimjulisha Mheshimiwa Waziri Mkuu na kukiri barua kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa heshima na unyenyekevu, nikimjulisha kwamba tumepokea mawazo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mawazo yaliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilikuwa ni kuhusu uteuzi wa Wajumbe 166. Maoni ya upande wa Zanzibar yalikuwa kwamba uteuzi huu unafanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, ufanyike baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar. Kama utakavyoona kwenye Muswada, pendekezo hili limezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili, lilikuwa linahusu marekebisho katika Ibara ya 3 ya Muswada, kifungu kipya cha 22B kwenye Muswada kinachohusu mambo ambayo Rais atazingatia katika kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum. Walipendekeza

maneno jinsia yatoke kutokana na kwamba inaweza kuwa ni vigumu kufikia uwiano wa kijinsia kwa 50% kwa 50% na wakasema kwamba izingatiwe jinsia pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili limezingatiwa katika Muswada isipokuwa sisi tulishauri kwamba kifungu hicho kibaki kama kilivyo na tumekileta hapa Bungeni kwa sababu kazi ya kutunga sheria si ya wadau bali ni kazi ya Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme sasa kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba kwa asili na kwa asilia, kwa asili na kwa asilia na kwa mujibu wa Katiba ya nchi, mamlaka ya kutunga sheria na kupitisha Miswada ya Serikali kuwa sheria, ni kazi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, yamkini Waheshimiwa Wabunge wanaowawakilisha wananchi katika Majimbo yao ya Uchaguzi, katika uwakilishi huo, inategemewa Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa Tanzania mnaonisikiliza, fanyeni uamuzi wa busara. Kazi ya uwakilishi, inategemewa Mbunge anapokuja hapa kujadili Muswada atakuwa ameshaongea na wale waliomchagua. Kama Wabunge hawafanyi hivyo, Watanzania wenzangu msiokuwa na vyama na wenye vyama, fanyeni uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nategemea kwamba, Wabunge wanachofanya hapa, kama kutoka nje au kujadili Muswada kwa makini, hiyo ni ridhaa ya wananchi wao

waliowachagua. Nategemea kwamba Wabunge bila kubishana, Wabunge wanaotoka Tanzania Zanzibar, pande zote mbili yaani nyuma yangu huku na mbele yangu huku, nyuma ya binadamu, nategemea kwamba na wenyewe walifuata utaratibu huo. Kwa hiyo, Bunge lisinyimwe nafasi ya kusikiliza kupitia kwa Wabunge maoni ya wanaowawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa pia pendekezo la tatu linalohusu Ibara ya 6 ya Muswada linalohusu Baraza la Katiba na walipendekeza kuwa iwapo Baraza la Katiba linashindwa kukamilisha kazi yake katika muda uliopangwa au endapo kuna mazingira yasiyotabirika ambayo yanaweza kukwamisha ukamilishaji wa kazi za Baraza katika muda uliopangwa wa siku sabini, basi Mwenyekiti apewe mamlaka kwa kushauriana na Naibu wake na kwa ridhaa ya Rais, kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar kuongeza muda huo usiozidi siku tisini. Muswada tulionao umezingatia pendekezo hilo la Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nipo hapa, nilipata nafasi na mimi kwenda kwenye Kamati na namshukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Tundu Lissu kwenye Kamati, walitoa mawazo mazuri sana...

**MBUNGE FULANI:** Hawakuwepo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Safi kabisa, kuhusiana na mapendekezo mawili tuliyofanya.

Pendekezo la kwanza, sisi tulikuwa tumeshauri kwenye Muswada wa Asili kwamba Spika ndiye awe Mwenyekiti wa hatua ya kwanza ya kuchagua Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, kusimamia ule utaratibu wa mwanzo. Wakatoa mapendekezo mazuri na yamekubalika kwenye Muswada. *(Makofi)*

La pili, hili alilisema Mheshimiwa Halima Mdee na nikamshika mkono kwamba ametumia kichwa chake kufikiri. Ndivyo nilivyosema! Tulikuwa tumesema kwamba kama watu watazungumza, wazungumze wasielewane, mwisho pale kwenye Bunge la Katiba, tunafanya nini? Yeye akasema, tuwape Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Katiba nafasi za ku-*negotiate* kujadiliana na kupatana, yaani kujenga *consensus* mpaka mwisho. Ikishindikana, basi tufanye *simple majority ya* pande zote mbili ya Tanzania Bara na ya Tanzania Zanzibar. Hii ni hoja ambayo tuliileta Bungeni tukitegemea kwamba itaboreshwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

La tatu, nilisemee tu ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba baadhi ya mambo tuliyoweka humu pamoja na hilo ambalo lilikuwa kwenye Kamati la namna ya kumaliza *stalemate* kama Bunge la Katiba halielewani, akasema jambo hilo halikuwemo kwenye Muswada wa awali, kwa hiyo, ni haramu kulileta kwenye Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika tunasoma Kanuni vizuri, na nina hakika tunafanya mambo haya

kwa nia njema. Kama tulivyozungumza kwenye Muswada wa Vyama vya Ushirika, kufanya kazi kwa nia njema. *(Makofi)*

Ibara ya 86 (7) inasema hivi: "Mjadala wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili, utahusu ubora na misingi ya Muswada huo tu." Sawa? Kanuni za Bunge ni nyingi sana. Kanuni za Bunge, ukiacha majedwali zipo 157. Nafahamu ndugu yangu Mheshimiwa Tundu Lissu anafahamu misingi ya kufanya tafsiri na Wachungaji pamoja na Mapadri mliomo humu ndani na wale ambao tulipitia Seminari lakini tukadanganywa, tukaacha; huwezi kusoma mstari moja ukasimamia hapo hapo. Ni lazima kama unasoma *Quran* katika aya fulani au Biblia, kwa mfano, "Ole walao nyama ya nguruwe na michuzi inichukizayo" Mambo ya Walawi 11:7-13. Ukasema basi, ole walao nyama ya nguruwe na michuzi inichukizayo, watakoma! Basi! Lazima uende mahali pengine. "Sikuja kuitengua Torati, ila kuikamilisha. Kimtiacho mtu unajisi ni kile kimtokacho, siyo kiingiacho." *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hii hapa namba kumi. 86 (10)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Aah, ngoja kwanza nifanye kazi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya Sheria ya tafsiri ina maeneo manne. Lakini la kwanza ni kwamba Sheria au Kanuni lazima isomwe kwa ujumla wake. Kwa

hiyo, unaposoma kanuni hizi na hilo ni sharti la kwanza. "*Statutes must be read as a whole*."

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, natumia muda mrefu kwa sababu hili ni jambo muhimu.

Ukiangalia Ibara ya 86(10) na angalia maneno yanayotumika; maneno mawili yanatumika hapa "Marekebisho na Mabadiliko." Hayakutumika kwa mambo ya ovyo ovyo tu, yana maana! Sasa inasema hivi:

"Katika hatua hii, iwapo mtoa hoja anataka kufanya marekebisho au mabadiliko (matumizi ya maneno hayo siyo ya ovyo ovyo!) katika Muswada wa Sheria kutokana na ushauri uliotolewa ama na Kamati ama katika Kamati au wakati wa Muswada wa Sheria kusomwa kwa mara ya pili au kwa sababu nyingine yoyote. Iwapo Muswada huo ni wa Serikali atamjulisha Mwandishi Mkuu wa Sheria, na iwapo Muswada huo husika ni wa Kamati au Binafsi, atamjulisha Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria ili atayarishe na kumkabidhi Katibu ambaye atagawa kwa kila Mbunge nakala ya Muswada wa Sheria uliochapishwa upya, ukiwa na marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika. (b) Jedwali la Marekebisho au Mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulipokuwa kwenye Kamati, Mheshimiwa Waziri akasema, lakini jamani kuna tatizo hapa. Hivi tunasema kwamba Bunge litafanya hivi, mbona hakuna utaratibu kwamba

isipowezekana itakuwaje? Mimi nina mashaka, na ni lazima niseme, mimi ni Mkatoliki, lazima niseme ukweli kuhusu ninayohisi, kwamba kuna watu hawataki mchakato huu umalizike. Ninahisi hivyo na ninathibitisha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati na ndiyo msingi wa Mheshimiwa Halima Mdee alivyosema kwenye Kamati na Mheshimiwa Tundu Lissu pia alishiriki kwenye hii *argument*. Wakasema haiwezekani tukafanya *simple majority.* Kwa sababu sisi tulikuwa tume-*propose* kwamba kama imeshindikana, tupige kura, na atakayeshinda ameshinda. Wakasema hapana. Mheshimiwa Tundu Lissu akasema, Katiba inatokana na hiari. Maneno yake mwenyewe! Ni *consensus.* Kwa hiyo, ni lazima twende kwenye Kamati tuzungumze, tujadiliane mpaka tuelewane. Ni maneno yake.

**MBUNGE FULANI:** Kwenye Kamati, au kwenye Bunge?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwenye Kamati pale! Tulikuwa tunazungumza kwenye Kamati pale, kulikuwa hakuna kamera, kwa hiyo, tulipata mawazo mazuri kweli kweli! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge, wanatoka nje kwa msingi kwamba upande wa Serikali ya Zanzibar haikushirikishwa, mimi sina mashaka. Walishirikishwa, na ninazo barua zao. Kwa upande kwamba yameingizwa mambo ambayo

hayakuwa kwenye Muswada wa Asili, Kanuni zinaruhusu kufanya hivyo, na zinaruhusu kwa msingi kwamba hapa sasa, wale watoto wa Machifu wanafahamu, kwamba kwenye *Court* ya *Chief* ndiyo watu wanazungumza. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, tumeleta Muswada huu hapa ili muujadili. Lakini kuna Muswada muhimu sana, niliona kwenye maoni ya Mhariri wa gazeti moja, anasema kwamba "Kuahirisha Muswada ule, unatokana na udhaifu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali." Kama udhaifu ni kushirikisha wananchi, ni kweli. Kwa sababu tumeona kwamba wenzetu wa Zanzibar walisema kwamba wanahitaji muda zaidi kuufanyia kazi, na sisi tukawashauri Viongozi wetu wakakubali. Lakini hili la kutoka nje kwa ajili ya Muswada huu kwamba unavunja Kanuni, siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi, lakini pia nafahamu na nilihudhuria Mkutano wa Kamati ambako Mheshimiwa Shoka, nadhani aliwahi kuwa Mbunge hapa, naye alitoa maoni. Lakini kama ilivyo utaratibu wa kupiga kura kwa Mujibu wa Sheria ya kupiga kura, katika nchi hii hakuna Sheria inayomlazimisha mtu kupiga kura. Kwa hiyo, hata ukialika watu, wasipokuja, unafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili Bunge naona watu wamekuja, kuna wanafunzi, kuna wanamichezo; mimi sio mshabiki wa ngumi, mimi ni mshabiki wa *chess.* Kuna wanafunzi; hili Bunge aah, ni Bunge la viwango

na tunategemea kwamba tunapoanzisha vitu, kwa kweli viwe vitu *very serious.*

Kama kutoka nje hivi, lazima kiwe ni kitu ambacho ni *very very serious! Very very serious!* Nami nafikiri tunaweza kuzungumza kama marafiki nje, lakini hapa ndani tuzungumze tu kwa misingi kwamba kifungu hiki ni kibovu, ondoa, weka kifungu hiki. Nasi kama Serikali, tupo tayari na tuna ushahidi kwamba tumeshawahi kukubali mabadiliko ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninakushukuru kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa sehemu kubwa sana umenisaidia kufafanua yale ambayo ningetoa kama ufafanuzi kwenye yale mambo yaliyojitokeza jana. Nakushukuru sana. Wenye masikio wamesikia, sina sababu ya kurudia kipengele kwa kipengele. Kazi kubwa ya kutunga Sheria ni yenu na nchi hii hapa imewakilishwa kikamilifu, kila Jimbo, Viti vilivyoko wazi huko kila mtu anajua kama yupo *officially* wapi aliko, lakini uwakilishi upo hapa kamilifu. Kwa maana hiyo, kuna uwakilishi kutoka Zanzibar, kamilifu; uwakilishi toka Kongwa, kamilifu. Kikatiba sisi ndio wenye kazi hiyo, wadau wanashiriki tu. Lakini wenye kazi hiyo ni sisi. Tukikimbia na kutoka nje, ni sisi; tukikaa humu ndani, ni sisi. *(Makofi)*

Niwambie ndugu zangu. Yapo mambo unaweza ukafanya, halafu baada ya muda hiyo *fashion*

inakuwa wala haina maana tena. Kwa hiyo, binadamu lazima unaangalia, baada ya muda unabadilisha *fashion* kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Maana ilianza siku ya kwanza kabisa Mheshimiwa Rais alipokuja kufungua Bunge hili. Siku ya kwanza alipokuja kufungua Bunge! Katiba inasema, Bunge halitaanza isipokuwa Mheshimiwa Rais ameliitisha. Alipokuja kuliitisha Bunge hili kwa hotuba yake ya kwanza, watu wakatoka nje. Alikuwa amewakosea nini? *(Makofi)*

Kwa hiyo, inafika mahali Watanzania, (huu ni ushauri) mimi naona huko mbele tuangalie hii Sheria ya kupata Mgombea Binafsi. Utakuta baadhi yao hawatatoka. Saa hizi, mtu afanyaje? Mimi naelewa! Wapo baadhi yenu, yaani maji yapo shingoni, mfanyeje? Siyo jambo ambalo mnakubaliana nalo, hata kidogo! Lakini huko mbele mimi nina hakika, Sheria zikikaa vizuri haya mambo hayatajirudia. Maana kila mtu atajipima kwamba hivi kweli kwa hili? Hili kweli nitoke? Tena Watanzania mtu anatoka baada ya kusaini posho. Maana kwenye kumbukumbu zangu za Bunge, hakuna ambaye hajasaini. Wote wamo! *(Makofi/Kicheko)*

Sasa narudi kwa Mheshimiwa Ali Khamis Seif. Ametoa hoja muhimu, naomba Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, tuifanyie maamuzi. Ndiyo iliyobaki peke yake katika Miongozo yote. Katumia Kanuni ya 69, inayoomba kwamba mjadala huu sasa uhairishwe na akatoa sababu zake na maelezo mengi yametoka hapa, mmepata ufafanuzi mkubwa sana.

Sasa jambo hili la hoja hii ya kwamba mjadala uahirishwe huwa inatakiwa ama mimi Spika nikubali ama niikatae kama Kiongozi hapa, ama mimi niitoe kwenu nyinyi muiamue. Mimi naamua kuitoa kwenu nyinyi muiamue. Ile tabia ya akina Mheshimiwa Mkosamali waliozoea kusema kwamba mimi napendelea, Watanzania waone kwamba siyo mimi, ni nyinyi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Chombo, chombo! Washa *mic*! Washa *mic*!

**NAIBU SPIKA:** Sasa naomba sana, kuna watu wana tabia ya kuweka vipaza sauti ili kupaza sauti. Naomba sana tuache tabia hiyo! Tukumbuke katika mitambo yetu tuna uwezo wa kujua ni nani anafanya nini, nawahakikishia. Siyo tabia nzuri hata kidogo!

Kwa hiyo, naomba kuwahoji. Maana hoja ni ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif. Wale wanaoungana na hoja ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif kwamba Bunge hili sasa liahirishe mjadala huu waseme ndiyo, na wale ambao hawakubaliani na hoja ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif na wanasema kwamba Bunge liendelee na Shughuli zake kama zilivyopangwa waseme ndiyo, ndiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kura zihesabiwe! Kura zihesabiwe!

**MBUNGE FULANI:** Anapoteza muda huyo!

**NAIBU SPIKA:** Namkubalia Mheshimiwa John Mnyika. Mimi ninachowaambieni kwa hakika, jambo hili lipo vizuri, na zege halilali. Kura zihesabiwe. Katibu andaa.

Mheshimiwa Habib Mnyaa kaa chini. Nakuomba sana twende kwa utaratibu. Moja baada ya lingine. Nawaheshimu sana, lakini mkinilazimisha nifike mahali pa kuchukua hatua, narudia tena, nina uwezo mkubwa wa kuchukua hatua. Kura zihesabiwe!

Kwa vile Makatibu hawakuwa wamejiandaa tunawapa dakika mbili, tatu ili waweze kujiandaa. Lakini litakuwa ni jambo la haraka. Katibu kwa haraka! Wakati huo mkijiandaa kengele iweze kulia nje.

Namwona Mheshimiwa Mnyaa anatoka. Anayetoka nje maana yake kengele itakapolia tutafunga mlango. Tukishafunga mlango, hataingia mtu humu ndani. Katibu, sasa zoezi linaanza, naomba utulivu na usikivu wenu na Watanzania fuatilieni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, watakaosema “Ndiyo” wanaungana mkono na Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

**MBUNGE FULANI:** Kwamba!

**NAIBU SPIKA:** Kwamba Bunge liahirishwe. Sijui kama inaeleweka!

Hoja ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif ni kwamba Bunge liahirishe shughuli zake. Sio ndiYo mjadala wenyewe! Yaani Bunge liahirishe huu mjadala kwa maana ya *Order Paper* ya leo. Mnanielewa?

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**NAIBU SPIKA:** Kwamba hii *Order Paper* ya leo sasa isifanye kazi. Watakaosema "Siyo" maana yake ni kwamba wanasema kwamba tuendelee na ratiba kama ilivyopangwa. Tumeelewana hapo? Katibu Anza. *(Makofi)*

*(Waheshimiwa Wabunge Walivyopiga Kura ya Kuunga Mkono au Kutounga mkono Hoja ya Mheshimiwa Mnyika)*

| | |
|---|---|
| Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda | Siyo |
| Mhe. Samuel John Sitta | Hakuwepo |
| Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Siyo |
| Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu | Siyo |
| Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli | Hakuwepo |
| Mhe. Prof. Mark James Mwandosya | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi | Hakuwepo |
| Mhe. Stephen Masatu Wasira | Hakuwepo |
| Mhe. Prof. Jumanne A. Maghembe | Hakuwepo |
| Mhe. Shukuru Jumanne Kawambwa | Siyo |
| Mhe. Hawa Abdurahman Ghasia | Siyo |
| Mhe. Sophia Mattayo Simba | Siyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Bernard Kamillius Membe | Hakuwepo |
| Mhe. Mathias Meinrad Chikawe | Siyo |
| Mhe. George Huruma Mkuchika | Siyo |
| Mhe. Celina Ompeshi Kombani | Siyo |
| Mhe. William Vangimembe Lukuvi | Siyo |
| Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi | Hakuwepo |
| Mhe. David Mathayo David | Hakuwepo |
| Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka | Siyo |
| Mhe. Samia Hassan Suluhu | Siyo |
| Mhe. Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa | Siyo |
| Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa | Hakuwepo |
| Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka | Hakuwepo |
| Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza | Siyo |
| Mhe. Balozi Khamis J.S. Kagasheki | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe | Siyo |
| Mhe. Dkt. Fenella Ephraim Mukangara | Siyo |
| Mhe. Dkt. Abdallah Omar Kigoda | Hakuwepo |
| Mhe. William Augustao Mgimwa | Siyo |
| Mhe. Prof. Sospter Mwijarubi Muhongo | Siyo |
| Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema | Siyo |
| Mhe. Dkt. Milton Makongoro Mahanga | Siyo |
| Mhe. Adam Kighoma Malima | Siyo |
| Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri | Hakuwepo |
| Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu | Siyo |
| Mhe. Benedict Ngalama Ole-Nangoro | Siyo |
| Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa | Hakuwepo |
| Mhe. Gregory George Teu | Siyo |
| Mhe. Pereira Ame Silima | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Mahadhi Juma Maalim | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga | Hakuwepo |
| Mhe. Goodluck Joseph Ole-Medeye | Siyo |
| Mhe. Philipo Augustion Mulugo | Siyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Ummy Ally Mwalimu | Siyo |
| Mhe. Dkt. Abdulla Juma Saadalla | Siyo |
| Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge | Siyo |
| Mhe. Dkt. Seif Seleman Rashidi | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Binilith Satano Mahenge | Siyo |
| Mhe. George Boniface Simbachawene | Hakuwepo |
| Mhe. Stephen Julius Masele | Hakuwepo |
| Mhe. January Yusuf Makamba | Siyo |
| Mhe. Dkt. Charles John Tizeba | Hakuwepo |
| Mhe. Amos Gabriel Makalla | Siyo |
| Mhe. Angellah Jasmine Kairuki | Siyo |
| Mhe. Janet Zebedayo Mbene | Siyo |
| Mhe. Saada Mkuya Salum | Hakuwepo |
| Mhe. John Momose Cheyo | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Augustine Lyatonga Mrema | Hakuwepo |
| Mhe. Edward Ngoyai Lowassa | Hakuwepo |
| Mhe. Margaret Simwanza Sitta | Siyo |
| Mhe. Jenista Joakim Mhagama | Siyo |
| Mhe. James David Lembeli | Hakuwepo |
| Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa | Siyo |
| Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa | Siyo |
| Mhe. Peter Joseph Serukamba | Hakuwepo |
| Mhe. Pindi Hazara Chana | Siyo |
| Mhe. Brig. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi | Siyo |
| Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o | Hakuwepo |
| Mhe. Andrew John Chenge | Siyo |
| Mhe. Sylvester Massele Mabumba | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Selemani Jumanne Zedi | Hakuwepo |
| Mhe. Freeman A. Mbowe | Ndiyo*(Makofi)* |
| Mhe. Kabwe Zuberi Zitto | Hakuwepo |
| Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu | Ndiyo |
| Mhe. Raya Ibrahim Khamis | Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Esther Nicholas Matiko | Hakuwepo |
| Mhe. Said Amour Arfi | Hakuwepo |
| Mhe. Mchungaji Israel Yohana Natse | Ndiyo |
| Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo | Ndiyo |
| Mhe. Pauline Philipo Gekul | Ndiyo |
| Mhe. Ezekia Dibogo Wenje | Ndiyo |
| Mhe. Leticia Mageni Nyerere | Ndiyo |
| Mhe. Joseph Roman Selasini | Ndiyo |
| Mhe. Sylvester Mhoja Kasulumbayi | Ndiyo |
| Mhe. Prof. Kulikoyela K. Kahigi | Ndiyo |
| Mhe. Halima James Mdee | Ndiyo |
| Mhe. Mchungaji Peter Simon Msigwa | Ndiyo |
| Mhe. John John Mnyika | Ndiyo |
| Mhe. Salvatory Naluyaga Machemli | Ndiyo |
| Mhe. Mhonga Said Ruhwanya | Hakuwepo |
| Mhe. Lucy Philemon Owenya | Hakuwepo |
| Mhe. Christowaja Gerson Mtinda | Ndiyo |
| Mhe. Dkt. Antony Gervas Mbassa | Ndiyo |
| Mhe. Naomi Amy Mwakyoma Kaihula | Ndiyo |
| Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi | Ndiyo |
| Mhe. Mustapha Boay Akunaay | Ndiyo |
| Mhe. Meshack Jeremiah Opulukwa | Hakuwepo |
| Mhe. Highness Samson Kiwia | Ndiyo |
| Mhe. David Ernest Silinde | Ndiyo |
| Mhe. Vincent Josephat Nyerere | Ndiyo |
| Mhe. Christina Lissu Mughwai | Hakuwepo |
| Mhe. Mwanamrisho Taratibu Abama | Ndiyo |
| Mhe. Maida Hamad Abdallah | Hakuwepo |
| Mhe. Anna Margareth Abdallah | Siyo |
| Mhe. Rashid Ali Abdallah | Hakuwepo |
| Mhe. Munde Tambwe Abdallah | Hakuwepo |
| Mhe. Bahati Ali Abeid | Ndiyo *(Makofi)* |

| | |
|---|---|
| Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood | Hakuwepo |
| Mhe. Chiku Aflah Abwao | Hakuwepo |
| Mhe. Rukia Kassim Ahmed | Ndiyo |
| Mhe. Lameck Okambo Airo | Hakuwepo |
| Mhe. Abdalla Haji Ali | Ndiyo |
| Mhe. Juma Othman Ali | Hakuwepo |
| Mhe. Mbarouk Salim Ali | Ndiyo |
| Mhe. Sara Msafiri Ally | Siyo |
| Mhe. Hussein Nassor Amar | Hakuwepo |
| Mhe. Kheri Khatib Ameir | Hakuwepo |
| Mhe. Abdallah Sharia Ameir | Siyo |
| Mhe. Abdulsalaam Selemani Amer | Siyo |
| Mhe. Amina Abdallah Amour | Ndiyo |
| Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Ndiyo |
| Mhe. Iddi Mohamed Azzan | Siyo |
| Mhe. Mussa Zungu Azzan | Hakuwepo |
| Mhe. Omary Ahmad Badwel | Siyo |
| Mhe. Faida Mohamed Bakar | Hakuwepo |
| Mhe. Salum Khalfan Barwany | Ndiyo |
| Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga | Siyo |
| Mhe. Gosbert Begumisa Blandes | Siyo |
| Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba | Siyo |
| Mhe. Ester Amos Bulaya | Siyo |
| Mhe. Selemani Said Bungara | Ndiyo |
| Mhe. Felister Aloyce Bura | Hakuwepo |
| Mhe. Agripina Zaituni Buyogera | Ndiyo |
| Mhe. Saidi Ramadhani Bwanamdogo | Hakuwepo |
| Mhe. Jerome Dismas Bwanausi | Siyo |
| Mhe. Josephine Tabitha Chagulla | Siyo |
| Mhe. Kisyeri Werema Chambiri | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Cyril August Chami | Hakuwepo |
| Mhe. Mary Pius Chatanda | Siyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje | Hakuwepo |
| Mhe. Capt. John Zefania Chiligati | Siyo |
| Mhe. Diana Mkumbo Chilolo | Hakuwepo |
| Mhe. Muhammad Amour Chomboh | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Amina Andrew Clement | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Mohamed Gulam Dewji | Hakuwepo |
| Mhe. Deo Haule Filikunjombe | Hakuwepo |
| Mhe. Josephine Johnson Genzabuke | Siyo |
| Mhe. Ali Juma Haji | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Khatib Said Haji | Ndiyo |
| Mhe. Zahra Ali Hamad | Hakuwepo |
| Mhe. Hamad Ali Hamad | Hakuwepo |
| Mhe. Azza Hillal Hamad | Siyo |
| Mhe. Asaa Othman Hamad | Ndiyo |
| Mhe. Neema Mgaya Hamid | Siyo |
| Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Hakuwepo |
| Mhe. Maria Ibeshi Hewa | Hakuwepo |
| Mhe. Mansoor Shanif Hiran | Hakuwepo |
| Mhe. Agness Elias Hokororo | Hakuwepo |
| Mhe. Balozi Seif Ali Idd | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Christina Gabriel Ishengoma | Siyo |
| Mhe. Yahya Kassim Issa | Hakuwepo |
| Mhe. Waride Bakari Jabu | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Jaddy Simai Jaddy | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Selemani Saidi Jafo | Siyo |
| Mhe. Asha Mshimba Jecha | Hakuwepo |
| Mhe. Juma Sururu Juma | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Riziki Omar Juma | Hakuwepo |
| Mhe. Abuu Hamoud Jumaa | Siyo |
| Mhe. Ritta Enespher Kabati | Hakuwepo |
| Mhe. David Zacharia Kafulila | Hakuwepo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu | Siyo |
| Mhe. Haji Khatib Kai | Ndiyo |
| Mhe. Moshi Selemani Kakoso | Siyo |
| Mhe. Innocent Edward Kalogeris | Siyo |
| Mhe. Dkt. Titus Mlengeya Kamani | Siyo |
| Mhe. Vick Paschal Kamata | Hakuwepo |
| Mhe. Josephat Sinkamba Kandege | Hakuwepo |
| Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya | Hakuwepo |
| Mhe. Mariam Reuben Kasembe | Siyo |
| Mhe. Rosweeter Faustin Kasikila | Siyo |
| Mhe. Eustace Osler Katagira | Siyo |
| Mhe. Vita Rashid Mfaume Kawawa | Siyo |
| Mhe. Zainab Rashidi Kawawa | Hakuwepo |
| Mhe. Gaudence Cassian Kayombo | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Kebwe Stephen Kebwe | Siyo |
| Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa | Hakuwepo |
| Mhe. Kheir Ali Khamis | Hakuwepo |
| Mhe. Sadifa Juma Khamis | Hakuwepo |
| Mhe. Salim Hemed Khamis | Hakuwepo |
| Mhe. Yussuf Haji Khamis | Ndiyo |
| Mhe. Muhammed Seif Khatib | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Aliko Nikusuma Kibona | Hakuwepo |
| Mhe. Mendrad Lutengano Kigola | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla | Siyo |
| Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe | Siyo |
| Mhe. Modestus Dickson Kilufi | Hakuwepo |
| Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga | Ndiyo |
| Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini | Hakuwepo |
| Mhe. Mariam Nasoro Kisangi | Hakuwepo |
| Mhe. Dunstan Luka Kitandula | Siyo |
| Mhe. Susan Limbweni Aloyce Kiwanga | Ndiyo |
| Mhe. Grace Sindato Kiwelu | Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Silvestry Francis Koka | Hakuwepo |
| Mhe. Capt. John Damiano Komba | Hakuwepo |
| Mhe. Mussa Haji Kombo | Ndiyo |
| Mhe. Kombo Khamis Kombo | Hakuwepo |
| Mhe. Maulidah Anna Valerian Komu | Hakuwepo |
| Mhe. Al-Shaymaa John Kwegyir | Hakuwepo |
| Mhe. Michael Lekule Laizer | Hakuwepo |
| Mhe. Devotha Mkuwa Likokola | Siyo |
| Mhe. Dkt. Festus Bulugu Limbu | Hakuwepo |
| Mhe. Alphaxard Kangi Ndege Lugola | Hakuwepo |
| Mhe. Riziki Said Lulida | Siyo |
| Mhe. Livingstone Joseph Lusinde | Siyo |
| Mhe. John Paul Lwanji | Siyo |
| Mhe. Moses Joseph Machali | Ndiyo |
| Mhe. Betty Eliezer Machangu | Siyo |
| Mhe. Zarina Shamte Madabida | Hakuwepo |
| Mhe. Mwigulu Nchemba Madelu | Hakuwepo |
| Mhe. John Shibuda Magalle | Hakuwepo |
| Mhe. Catherine Valentine Magige | Hakuwepo |
| Mhe. Ezekiel Magolyo Maige | Hakuwepo |
| Mhe. Faki Haji Makame | Ndiyo |
| Mhe. Eng. Ramo Matala Makani | Hakuwepo |
| Mhe. Amina Nassoro Makilagi | Hakuwepo |
| Mhe. Anne Kilango Malecela | Siyo |
| Mhe. Annamarystella John Mallac | Siyo |
| Mhe. Ignas Aloyce Malocha | Siyo |
| Mhe. Dkt. David Mciwa Mallole | Hakuwepo |
| Mhe. Murtaza Ally Mangungu | Siyo |
| Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya | Siyo |
| Mhe. Abdul Jabiri Marombwa | Hakuwepo |
| Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Augustino Manyanda Masele | Siyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Donald Kelvin Max | Hakuwepo |
| Mhe. Lucy Thomas Mayenga | Siyo |
| Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka | Siyo |
| Mhe. James Francis Mbatia | Ndiyo |
| Mhe. Kuruthum Jumanne Mchuchuli | Hakuwepo |
| Mhe. Zakia Hamdani Meghji | Hakuwepo |
| Mhe. Mariam Salum Mfaki | Siyo |
| Mhe. Athumani Rashid Mfutakamba | Hakuwepo |
| Mhe. Subira Khamis Mgalu | Siyo |
| Mhe. Zabein Muhaji Mhita | Siyo |
| Mhe. Esther Lukago Minza Midimu | Siyo |
| Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi | Siyo |
| Mhe. Desderius John Mipata | Hakuwepo |
| Mhe. Mohamed Hamisi Missanga | Siyo |
| Mhe. Faith Mohamed Mitambo | Hakuwepo |
| Mhe. Margareth Agnes Mkanga | Siyo |
| Mhe. Dunstan Daniel Mkapa | Siyo |
| Mhe. Nimrod Elirehema Mkono | Hakuwepo |
| Mhe. Felix Francis Mkosamali | Ndiyo |
| Mhe. Mustafa Haidi Mkullo | Siyo |
| Mhe. Ritta L. Mlaki | Hakuwepo |
| Mhe. Martha M. Mlata | Hakuwepo |
| Mhe. Rebecca M. Mngodo | Ndiyo |
| Mhe. Herbert J. Mntangi | Siyo |
| Mhe. Mohammed Habib Mnyaa | Ndiyo |
| Mhe. Ally Keissy Mohamed | Hakuwepo |
| Mhe. Hamad Rashid Mohammed | Hakuwepo |
| Mhe. Mohammed Said Mohammed | Hakuwepo |
| Mhe. Rajab Mohammed | Hakuwepo |
| Mhe. Luhaga J. Mpina | Siyo |
| Mhe. Dkt. Haji H. Mponda | Siyo |
| Mhe. Mariam Salum Msabaha | Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Assumpter N. Mshama | Hakuwepo |
| Mhe. Peter M. Msolla | Hakuwepo |
| Mhe. Said M. Mtanda | Hakuwepo |
| Mhe. Abdul R. Mteketa | Hakuwepo |
| Mhe. Abasi Z. Mtemvu | Ndiyo |
| Mhe. Philipa G. Mturano | Hakuwepo |
| Mhe. Mtutura A. Mtutura | Hakuwepo |
| Mhe. Thuwayba Idrisa Muhamed | Ndiyo |
| Mhe. Joyce J. Mukya | Ndiyo |
| Mhe. Hasnain M. Murji | Siyo |
| Mhe. Bernardetha K. Mushashu | Siyo |
| Mhe. Mussa H. Mussa | Hakuwepo |
| Mhe. Eugen E. Mwaiposa | Siyo |
| Mhe. Victor K. Mwambalaswa | Hakuwepo |
| Mhe. Salome D. Mwambu | Siyo |
| Mhe. Mchungaji. Luckson N. Mwanjale | Siyo |
| Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa | Siyo |
| Mhe. Clara D. Mwatuka | Hakuwepo |
| Mhe. Amina M.Mwidau | Ndiyo |
| Mhe. Charles J. Mwijage | Siyo |
| Mhe. Hussein M. Mzee | Hakuwepo |
| Mhe. Joshua S. Nasari | Hakuwepo |
| Mhe. Yusup A. Nassir | Siyo |
| Mhe. Richard M. Ndassa | Siyo |
| Mhe. Philimon K. Ndesamburo | Hakuwepo |
| Mhe. Dkt. Faustine E. Ndugulile-Siyo | Hakuwepo |
| Mhe. William M. Ngeleja | Hakuwepo |
| Mhe. Stephen H. Ngonyani | Hakuwepo |
| Mhe. Cynthia H.Ngoye | Siyo |
| Mhe. Ahmed J. Ngwali | Hakuwepo |
| Mhe. Juma A. Njwayo | Siyo |
| Mhe. Juma S.Nkamia | Siyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Said J. Nkumba | Siyo |
| Mhe. Dkt. Lucy S. Nkya | Hakuwepo |
| Mhe. Albert O.Ntabaliba | Hakuwepo |
| Mhe. Deogratias A. Ntukamazina | Hakuwepo |
| Mhe. Omar R. Nundu | Siyo |
| Mhe. Abia M. Nyabakari | Hakuwepo |
| Mhe. Nyambari C. M. Nyangwine | Siyo |
| Mhe. Tauhida C. G. Nyimbo | Hakuwepo |
| Mhe. Christopher O. Ole- Sendeka | Hakuwepo |
| Mhe. Rashid Ali Omar | Ndiyo |
| Mhe. Asha Mohamed Omari | Ndiyo |
| Mhe. Nassib Suleiman Omar | Siyo |
| Mhe. Saleh Ahmed Pamba | Ndiyo |
| Mhe. Cecilia D. Paresso- | Ndiyo |
| Mhe. Ismail A. Rage | Hakuwepo |
| Mhe. Rachel M. Robert | Hakuwepo |
| Mhe. Mch. Dkt Getrude P. Rwakatare | Siyo |
| Mhe. Jasson S. Rweikiza | Siyo |
| Mhe. Mwanakhamis Kassim Said | Hakuwepo |
| Mhe. Said Suleiman Said | Ndiyo |
| Mhe. Moza Abedi Saidy | Ndiyo |
| Mhe. Magdalena H. Sakaya | Ndiyo |
| Mhe. Kidawa Hamid Saleh | Siyo |
| Mhe. Ramadhani Haji Saleh | Siyo |
| Mhe. Masoud Abdallah Salim | Ndiyo |
| Mhe. Ahmed Ali Salum | Hakuwepo |
| Mhe. Deo K. Sanga | Hakuwepo |
| Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya | Hakuwepo |
| Mhe. Ali Khamis Seif | Ndiyo |
| Mhe. Haji Juma Serewej | Hakuwepo |
| Mhe. Ahmed M. Shabiby | Hakuwepo |
| Mhe. Abdulkarim E. H. Shah | Hakuwepo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Haroub M. Shamis | Hakuwepo |
| Mhe. Henry D. Shekifu | Hakuwepo |
| Mhe. Beatrice M. Shelukindo | Hakuwepo |
| Mhe. Fakharia Khamis Shomar | Hakuwepo |
| Mhe. Namelok E. M. Sokoine | Hakuwepo |
| Mhe. Jitu V. Soni | Siyo |
| Mhe. Rose K. Sukum | Ndiyo |
| Mhe. Suleiman Suleiman | Hakuwepo |
| Mhe. Shaffin A. Sumar | Siyo |
| Mhe. Sabrina H. Sungura | Ndiyo |
| Mhe. Kaika S. Telele | Siyo |
| Mhe. Salim Hassan Abdullah Turky | Hakuwepo |
| Mhe. Martha J. Umbulla | Hakuwepo |
| Mhe. Zaynab M. Vullu | Hakuwepo |
| Mhe. Anastazia J. Wambura | Hakuwepo |
| Mhe. Godfrey W. Zambi | Siyo |
| Mhe. Said M. Zubeir | Siyo *(Makofi)* |
| Mhe. Mahmoud Mgimwa | Siyo |

**NAIBU SPIKA:** Bado. Walioingia wasimame walipo, ambao hawakuwa wamesomwa majina yao wajitaje mmoja baada ya mwingine.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Fakharia Khamis Shomar, nasema Siyooo!

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mimi naitwa Mwanahamis Kassim Said, nasema, Siyo. *(Makofi)*

**MHE. KHALFAN HILALY AESHI:** Mimi ninaitwa Khalfan Hilaly Aeshi, nasema, Siyo! *(Makofi)*

**MHE.YUSSUPH SALIM HUSSEIN:** Mimi nanaitwa Yusuph Salum Hussein, nasema, Ndiyo!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa tayari eh!

**MHE. MAHMOUD MGIMWA:** Siyo!

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**NAIBU SPIKA:** Tumekamilisha. Mheshimiwa Lembeli pata maelezo kwanza ya mwenzio, maana ndiyo mnaingia sasa hivi.

**MBUNGE FULANI:** Kama unataka Muswada undelee sema 'Siyo', kama unataka Muswada uondolewe, sema 'Ndiyo.' Kwa hiyo, wewe sema 'Siyo.'

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Lembeli!

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Siyo! *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Haya Makatibu wangu fanyeni *chap chap* ili tuweze kuendelea. Tunaweza kupata wachangiaji wawili hivi, kama hali itaruhusu.

*(Hapa kura zilihesabiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kuwa matokeo yatakayotoka,

kawaida ya upigaji kura wa namna hii, kinachohitajika ni *simple majority.* Kwa hiyo, wanaendelea kujumlisha halafu tutaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu imekamilika. Sasa naomba tumsikilize Katibu atoe matokeo. Kabla hajatoa matokeo niseme tu kwamba, baada ya matokeo haya sasa ni kazi itakayokuwa mbele yetu kama ni kuahirisha au vinginevyo, na sitapokea tena suala lingine lolote la kujaribu ku-*delay* shughuli. Katibu naomba tupatie matokeo. *(Makofi)*

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kura zilizopigwa; jumla ya Wabunge wote ni 351, ambao hawakuwepo Bungeni ni Wabunge 136; katika kura zilizopigwa ambazo zilisema ‘Ndiyo’ ni kura 59 na kura zilizosema ‘Siyo’ ni kura 156. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa matokeo hayo, Mheshimiwa Ali khamis Seif, hoja yako imekataliwa na Bunge. Kwa hiyo, kwa maamuzi ya kidemokrasia kwa mtu yeyote anayeamini demokrasia ni kwamba shughuli hii iendelee. *(Makofi)*

Kama nilivyosema, naomba sana sasa mniruhusu tuongoze hiki kikao, na mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Dkt. Mrema. Walikuwa wachangie Wabunge kumi, lakini kutokana na mambo haya sasa tutampata mchangiaji mmoja tu. Mheshimiwa Mrema, naomba uchangie sasa hivi tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrema, naomba uendelee.

Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani nakuomba umpe nafasi Mheshimiwa Mrema achangie.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika!

**NAIBU SPIKA:** Nakuomba sana Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani!

*(Hapa Mheshimiwa Freeman A. Mbowe aliendelea kusimama)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrema, kaa chini. Kiongozi wa Upinzani itakuwa ni aibu sana kama wewe ndio utakayekuwa unaongoza kutokutii mamlaka kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika…

*(Hapa Mheshimiwa Freeman A. Mbowe*

*aliendelea kusimama)*

**NAIBU SPIKA:** Nakuomba sana Kiongozi wa Upinzani ukae chini.

*(Hapa Mheshimiwa Freeman A. Mbowe aliendelea kusimama)*

**NAIBU SPIKA:** Ni vizuri Watanzania mwone jinsi ambavyo fedha zenu zinatumika vibaya.

**WABUNGE FULANI:** *Aaaah! Aaaaah! (Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba *Sergeant At Arms* mjiandae!

**MBUNGE FULANI:** *Yes, Yes!* Kabisa, hiyo itokee!

**NAIBU SPIKA:** Nikisema hivyo, namaanisha. Hivyo *Sergeant At Arms* naomba mjiandae, na nguvu yote ya Askari iliyopo katika Bunge ijiandae. Nawapa dakika tano Askari wote mjiandae kwa sababu hakuna kisichowezekana. Nakuomba tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani kwa heshima yako ukae chini.

**WABUNGE FULANI:** Aaah, aaah, aaah!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja.

**NAIBU SPIKA:** Nakuomba sana kwa mara nyingine ukae chini.

**WABUNGE FULANI:** Aaah, aaah!

*(Hapa Mheshimiwa Freeman A. Mbowe aliendelea kusimama katika kiti chake)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba Askari wote waliopo katika maeneo haya waingie ndani. *Sergeant At Arm,* tusaidiane haraka kuharakisha muda. Sasa naomba Kiongozi wa Upinzani atolewe nje ya Ukumbi wa Bunge. Askari fanyeni kazi hiyo haraka.

*(Hapa Serjeant-At-Arms waliingia ndani ya ukumbi wa Bunge kumtoa nje Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha CHADEMA Walimzunguka Mheshimiwa Freeman A. Mbowe - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kuzuia asitolewa nje na Askari)*

**MBUNGE FULANI:** Hatoki! Hatoki mtu hapa!

**MBUNGE FULANI:** Msimtoe Kiongozi! Tunataka Demokrasia! Hatutaki Kiongozi atoke!

*(Hapa fujo ilianza kati ya Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA na Askari)*

**NAIBU SPIKA:** Askari hamjaletwa humu ndani kufanya majadiliano, kazi yenu ni kuhakikisha Kiongozi wa Upinzani anatoka nje ya Ukumbi wa Bunge. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni Kanuni gani inamzuia!

*(Hapa Wabunge wa CHADEMA waliimba,*
*'Hatutaki, Kuburuzwa!')*

**NAIBU SPIKA:** Askari wote mliopo humu ndani, naomba mnisikilize!

**MBUNGE FULANI:** Hiyo ni Kanuni gani anayotumia?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda, muda!

**NAIBU SPIKA:** Sasa naagiza Askari kwa mara ya mwisho, hakikisheni Kiongozi wa Upinzani anatolewa nje, kama Askari.

*(Hapa fujo ilizidi kuongezea ndani ya*
*Ukumbi wa Bunge kati ya Askari*
*na CHADEMA wanaozuia Mheshimiwa Mbowe*
*asitolewe nje)*

**NAIBU SPIKA:** Ni nani anayewasimamia hawa?

**MBUNGE FULANI:** Askari kama mmeshindwa, tuachieni sisi wenyewe! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Askari wameshindwa, watuachie wenyewe!

*(Hapa Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi na Mheshimiwa Sylivester Kasulumbayi walipambana na Askari kuwazuia wasimtoe nje Mheshimiwa Freeman Mbowe)*

**MBUNGE FULANI:** Sasa wale wanaingia kwenye shida ile yote kumzuia Mheshimiwa Mbowe! Inahusu nini? Yule anapigana na Mheshimiwa Kasulumbayi!

**WABUNGE FULANI:** Toaa, toaa, toaa! Toa nje!

*(Hapa Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi na Mheshimiwa Kasulumbayi walitolewa nje ya Ukumbi wa Bunge)*

**WABUNGE FULANI:** Bado Mheshimiwa Mbowe! *(Kelele/Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Askari wanarudi na wanavua tai!

**MBUNGE FULANI:** Wanavua tai sasa hivi! Ayayaah! Hii kali! Ni vizuri wakaleta heshima!

*(Hapa Mheshimiwa Freeman Mbowe aliamua kuondoka ndani ya Ukumbi wa Bunge akisindikizwa na Wabunge wa CUF, CHADEMA na NCCR-MAGEUZI)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mbowe ameshakubali kwenda mwenyewe.

**MBUNGE FULANI:** He! He! Duh! Sugu umemwona alivyotolewa kama mzigo? Sugu, kabebwa vibaya sana. Maana kachukuliwa mzega mzega! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Alikuwa ana-*test* nguvu za Askari.

**MBUNGE FULANI:** Tanganyika jeki!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo utaratibu wa kukamata mhalifu!

**MBUNGE FULANI:** Naibu Spika, hoyeeee! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), atoe hoja ili tuweze kuongeza muda wa nusu saa tuendelee na majadiliano. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Jioni anataka ku-*wind up! (Makofi)*

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoona leo muda wa wananchi ulivyopotea kwa sababu ambazo

hazifahamiki na hazina maana, na kwa sababu tutakuwa hatuwatendei wananchi haki, kuahirisha hili Bunge na kutofanya kazi yeyote tangu asubuhi na hasa kwa kuwa Mheshimiwa Mrema alishatajwa kwa ajili ya kuchangia pamoja na Wabunge wengine, naomba kutoa hoja kwa Waheshimiwa Wabunge mliopo ambao mmekubali kubaki humu ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi ya wananchi, mkubali Bunge liongeze kidogo dakika thelathini ili angalau tujibane tupunguze muda wetu wa mapumziko, tuwatendee haki wananchi kuongeza muda wa dakika thelathini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono na Wabunge wote. Mheshimiwa Dkt. Mrema, nakuomba uchangie, atafuatia Mheshimiwa Anne Kilango Malecela asubuhi hii.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yangu ni mafupi. Kwanza nataka niwaeleze wananchi wa Vunjo, wapigakura wangu na Watanzania, kwanini Augustino Lyatonga Mrema hakutoka nje ya Bunge jana?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachotaka kusema, hapa nina kofia mbili tangu jana. Mimi ni Mwenyekiti wa *TCD. TCD* ni Taasisi inayojumuisha Vyama sita na wamenichagua mimi kuwa Mwenyekiti. Naangalia CCM, CHADEMA, *NCCR, TLP, UDP* na *CUF*. Mimi ndio Mwenyekiti wao, mimi ndiyo bosi wao! Naomba Watanzania waelewe, mimi ni Kiongozi, nina dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa siwezi kukimbia wajibu wangu wa kuangalia hivi Vyama. Kwa hiyo, walioamua kutoka, sawa, wametimiza wajibu wao wa kidemokrasia wanaoufahamu. Lakini mimi siyo kwamba nimebaki kwa kuwa mimi ni CCM au ni kibaraka wa CCM. Nimebaki kwa sababu kuna Chama kilicho kwenye *TCD* ambacho mimi nakiongoza. CCM wapo hapa, mimi nakimbia naenda wapi? Nakimbia kwa sababu zipi? Hilo la kwanza. Naomba Watanzania wajue lililoniweka hapa. Mimi ni Kiongozi wa Vyama sita vyenye Wabunge Bungeni CCM ikiwa mojawapo. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokutana tarehe 26 *St. Gasper TCD,* vyama hivyo sita, tulikuwa na ajenda kwenye *Steering Committee* yetu. Kuna maneno tumepanga mazuri. Mojawapo ni kwamba tulimwomba Profesa Lipumba, hebu tuandikie *write up* unavyoona hali ya kisiasa inavyoelekea kuhusu Katiba Mpya. Akatuletea *paper* hii hapa, ambayo ndiyo tulizungumza mambo muhimu ya kurekebisha katika Katiba sasa kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya matatizo yaliyosemwa hapa yalikwishaonekana kwamba kutakuwa na mgogoro. Sisi tukatafuta, tutafanyaje *if the worse comes to the worse*? Hii *paper* ni ya Ibrahimu Haruna Lipumba kaandika na tukai-*table* kwenye kikao cha tarehe 26 St. Gasper. Tukai-*adopt* hii kwamba pakitokea kitu chochote kama hii Katiba Mpya haitapatikana kabla ya mwaka 2015, tufanye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba hii *paper* niiweke Mezani ili mwone mawazo ya Profesa Lipumba - Mwenyekiti wa *CUF* anasemaje kuhusu haya mambo, na huu mchakato unavyoendelea? Hilo ni la kwanza, karatasi ipo hapa na moja ya kitu ambacho amekisema hapa ni kwamba, ili kupata Katiba ambayo ni muafaka wa kitaifa katika mambo ya utawala, uchumi na siasa inahitaji muda hasa katika Taifa lenye Muungano wa nchi mbili ambazo kwa muda mrefu umekabiliwa na kero nyingi, huwezi kupata muafaka wa kitaifa *faster faster*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ameandika hapa, amezungumzia kuhusu athari za kuvunja Muungano. Tunahitaji mjadala wa kutosha kuhusu umuhimu wa Muungano na athari za kuuvunja. Ukisoma mapendekezo ya Kamati ya Maridhiano ya Zanzibar kuhusu Muungano yaliyotolewa kabla ya Rasimu ya Katiba, ni vigumu kuamini kuwa Muungano utakuwepo ikiwa mapendekezo hayo yatakubaliwa. Mapendekezo hayo akayaorodhesha. Sasa *feed back* itakuwaje? Tukajiuliza kule *TCD,* kama patatokea

chochote, tunafanyaje? Wakasema kama haitawezekana kupatikana Katiba Mpya 2015 kwa sababu zozote zile na kutokana na vurugu zinazoonekana zitatokea, kwa hiyo, tufanyeje?

La kwanza, ni kwamba tuiombe Serikali tuangalie hii Katiba iliyopo tufanye marekebisho ambayo yatatusaidia. Kwa mfano, mwaka ujao kuna uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Watu wakauliza, kama hii Katiba itakuwa haiko tayari kabla ya Aprili, 2014, huo uchaguzi wa Vitongoji na Vijiji tutaufanyaje? Tukasema ni lazima tufanye marekebisho kwenye Katiba iliyopo. Profesa Lipumba - Mwenyekiti wa *CUF* anasema hapa aliyo-*table* kwenye hicho kikao jamani! Maana tusipoangalia hii nchi itasambaratika sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ni nzuri ya kufikiri tutapata Katiba Mpya, lakini katika mazingira haya haipatikani Katiba mpya hapa! Nchi itavurugika tu! Kwa sababu sio wote wenye nia njema! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukakubaliana kwamba hebu tuangalie yale mambo muhimu yakifanyiwa marekebisho kwenye Katiba iliyopo, yanaweza yakatuvusha mwaka 2015, tukapata muda wa kujipanga? Jambo hili ni kubwa kuliko tunavyofikiri. Tena Profesa Lipumba anasema katika nchi zenye Muungano wa Serikali mbili zenye matatizo chungu mbovu, sasa tukakubaliana kwamba, mimi kama Mwenyekiti wa *TCD* tutafute redio, televisheni na magazeti apewe nafasi aelezee hiki ambacho

anakitaka Serikali ikifanye. Hayo ndiyo yalikuwa makubaliano yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mwenyekiti, uende umwone Waziri Mkuu na umwone Mheshimiwa Rais, ndiyo kazi waliyonipa; umwone Mheshimiwa Rais tuone *feed back position* kama mambo yataharibika.

Haya mambo yanayofanyika sasa hivi, siyo tabia nzuri. Siyo mazuri haya! Mimi nawaambieni jamani! Inawezekana mna nia nzuri ya kutaka kupata Katiba, lakini nakwambia Katiba hii, kwa mazingira ninayoyaona, yatakuwa magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, name nitataka hii karatasi ya Profesa Lipumba iwekwe Mezani Watanzania wasome ni vitu gani ambavyo *TCD* tuliviona, halafu nikaambiwa sasa nimwone Mheshimiwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo, jana nisingeweza kutoka. Ningetokaje? Hiyo *appointment* na Mheshimiwa Rais nitakwenda kumweleza nini? Kwa hiyo, nilitaka kuona watu wanavyochangia, kitakacholeta vurugu katika nchi hii, vikwazo viko wapi? Kwa hiyo, naomba Watanzania, mimi sio kibaraka wa CCM, mimi ni Mtanzania Mzalendo napenda nchi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siwezi kuja hapa nikaacha Kiti changu nilichopewa na wananchi wa Vunjo; ehe! Nikikuta siku nyingine mtu amekalia, mimi nitasema nilikuwa wapi? Kwa hiyo, hatoki mtu

hapa! Kama ni mashati tutashikana huku huku ndani mpaka kieleweke! Hilo ni la kwanza lililonifanya nibaki hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waziri Mkuu *paper* iko hapa, tumpelekee Mheshimiwa Rais mwangalie *seriously* mambo haya yaliyopendekezwa hapa ili tufanye marekebisho tusonge mbele. Hii Katiba Mpya, isitutoe roho! Tujipe muda wa kuangalia mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mimi ni Mwenyekiti wa *TLP.* Naomba wenzangu waliotaka kunishika mashati jana wakitaka tutoke nje; natoka nao nje kwa lipi? Mbona hawanipendi mimi? Mimi wananipenda kwenye migogoro, kwenye kutoka nje, kwenye vurugu! Wao wanasema kwamba wao ni Kambi ya Upinzani Rasmi, mbona *TLP* sipo? Mbona hawakunishirikisha? Siyo rasmi! Mimi sipo! Kwa hiyo, siwezi kulaumiwa. Nalaumiwa nini? Nami nilijaribu kujipendekeza kwa hawa jamaa, nimeshindwa, nimechoka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 nilipinga bajeti hapa ili kuwafurahisha, nikafikiri watanipenda, kumbe nimepoteza. Mwaka 2012 nikapinga tena, nikatoa Shilingi nikafikiri watanipenda, kumbe bado wananinyanyapaa. Hata wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitakuomba radhi, dhamira yangu inanisuta; nililetewa fomu hapa nikatia saini kwamba wewe tukung'oe. Nikiangalia kosa la huyu Bwana ni lipi? Sasa mimi ninachotaka kusema hapa, kama siasa zenyewe ndiyo hizi, leo tunasema Mheshimiwa Rais asiteue mtu,

mbona alimteua Mheshimiwa Mbatia na bado ameendelea kubaki hapa? Mbona ameteua watu wengi; CHADEMA wana mtu, Profesa Baregu mbona yupo pale, mbona hawajakataa? Jamani, mbona tunamsingizia Mheshimiwa Rais? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona kukiwa na matatizo tunakwenda Ikulu tunakunywa chai na maandazi? Kama kulikuwa na maneno, kwa kuwa walinituma mimi kama Mwenyekiti wa *TCD,* kama kungekuwa na mgogoro si tungekubaliana? Kwanza, tungeitana nje *TCD,* jamani huu Muswada upo hivi; kumbe wenyewe wamepanga huko, hawajanishirikisha, hawajaniambia; eti dakika ya majeruhi ndiyo wananiambia nitoke. Sasa nitoke niende wapi? Tunaongoza nchi hii kwa utaratibu gani? *(Makofi/Kicheko)*

Ninachotaka kusema ni kwamba nawaambia Watanzania kwamba mimi nitashirikiana na Mheshimiwa Rais, kwa sababu kule Vunjo Mheshimiwa Rais alipata kura 27,000 na mimi nikapata kura 26,000. Wote walimchagua Rais wa CCM, wakijua na mimi ni *TLP*. Sasa ni lazima nifanye kazi na yeye, yeye ndio Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hawa jamaa, mimi nilikuwa na uchaguzi Kata ya Kilema Kusini, wanajua Diwani wangu amekufa, mbona walinifuata kule Kilema Kusini kupambana na mimi! Sisi ni Wapinzania, huko nyuma walikuwa wananilaumu, mbona wamenifuata pale, Mungu akanisaidia

nikawashinda, nikawagaraza na CCM! Kwa hiyo, ninachotaka kusema, sikiliza, mimi nimekuja hapa kwa ajili ya maendeleo. *Interest* yangu, ni Jimbo langu. *You scratch my back, I scratch yours*. Sasa bila kujenga mazingira mazuri na wawekezaji hao wa Chama Tawala wa CCM wenye fedha na Rais wetu, maendeleo ya watu wangu wa Vunjo yatapatikanaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu ameniuliza, lile soko la Kimataifa nimekwenda kule *TIB* tayari wanatengeneza utaratibu wa kupata Shilingi bilioni 40 kujenga soko na Mji wa kisasa pale Vunjo. Siwezi kuelezea usambazaji wa maji, hata kule Mwika Kaskazini na Mwika Kusini, Mheshimiwa Rais ameahidi, ameniambia Mrema lete *write up,* wale Wajerumani tayari wameshachangia Shilingi milioni 150 wameleta juzi. Wakaniambia, sasa ule mchango wa Rais! Nikawaambia, nitaenda kumwambia! Kwa hiyo, mimi nipo hapa kwa ajili ya kusimamia mambo ya kweli, mambo ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, ninachosema, maelezo yametolewa na Serikali hapa kuhusu jinsi walivyofanya huko Zanzibar, walivyoshirikishwa. Jana sikuwa na *information* ya kutosha, sasa ningekurupuka nitoke; leo nimepata *information* ya kutosha, kumbe watu wameshirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema, kwa mtaji huu, hii nchi inakwisha. Angalia Misri kilichotokea! Walianza kelele kama hizi za Mbaraka aondoke aondoke, maandamano, nguvu ya umma.

Kweli ameondoka. Tumemweka Mohammed Morsi, *Peoples Power.* Baada ya mwaka *Peoples Power* inarudi tena, Mohammed Morsi hafai. Ninachotaka kusema, jamani eeh, haiwezekani kuongoza nchi hii kwa nguvu. Unajua nchi hii ni ya kidemokrasia; unaona Rais wa Kwanza alikaa miaka yake 25 akaondoka; amekuja mwingine miaka kumi na ameondoka; amekuja Mheshimiwa Rais Mkapa ameondoka; amekuja Mheshimiwa Kikwete, sioni akisema kwamba ataendelea. Hii ndiyo demokrasia. Hakuna demokrasia kubwa kuliko hii ya uchaguzi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunataka nchi hii iwe kama Misri, tuendelee na hizi vurugu na wananchi wazishabikie. Kama tunataka nchi yetu iwe kama Tunisia au Libya! Ninachotaka kuwaambia Watanzania, haya yanayotokea ni fedheha, ni aibu kubwa, kwa nchi iliyozoea utulivu, kwa nchi ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatafuta nini? Ukibaki hapa Bungeni si unapinga kwa kusema na Watanzania watakusikia? Siyo kwa kutumia mabavu au kwa kutumia nguvu. Kwa hiyo, nawaambia Watanzania kwamba, nimebaki hapa kwa sababu ya majukumu yangu niliyonayo kama mzalendo wa nchi hii, mimi siyo kibaraka, mimi siyo pandikizi. Lakini na mimi siwezi kushikwa masikio nikapelekeshwa, sikubali! Nitatumia akili yangu, hekima yangu na busara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi simameni imara. Simameni imara, kwa sababu mimi nafahamu taratibu za Bunge, hiki ni kipindi changu cha tatu. Naomba wananchi wanisikilize, Serikali inapoleta Muswada, haimng'ang'anizi mtu kukubali. Serikali inatoa muda tutoe hoja, tushindane kwa hoja ndani ya Bunge. Wakati mwingine Serikali inakubali Wabunge tunapokataa jambo, inarekebisha ilichokileta. Wakati mwingine Mbunge ukiona Serikali na wenzako wengi wamesimama upande ule, unapaswa kukubali upande ambao ni wa wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wananchi waelewe kwamba Serikali hailazimishi kitu. Sheria inapotungwa ndani ya mjengo huu, wote tunaruhusiwa kutoa maoni yetu, tunachangia hoja, mpaka mwishoni tunakubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wenzetu naomba nimuunge mkono *AG* jambo alilosema, kwamba Watanzania ni vema wakaelewa kwamba wenzetu hawataki Katiba ipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba tunayoipigania sasa hivi ni Katiba ambayo tunataka ituondoe hapa tulipo. Utuondoe kwenye kuitwa ulimwengu wa tatu, utuondoe kwenye kuitwa nchi maskini, itupeleke kwenye ulimwengu wa katikati. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote sasa tusimame imara tushirikiane na Serikali ya Chama chetu cha Mapinduzi, tuunde Katiba, tuondoke hapa tulipo. Ni aibu kwamba sisi tuna rasilimali nyingi lakini tunaitwa maskini. Hakuna sababu! Ni Katiba hii tunayoitunga sasa, tunayoitengeneza, tunayoirekebisha ili tusonge mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuanza kuchangia. Naomba nirudi kwenye Kifungu cha 22 cha Sheria mama, kwenye idadi ya Wajumbe ambao wataunda Bunge Maalum la Katiba. Katika Wajumbe waliotajwa hapa ndani ya Katiba mama kuna Wabunge wa Jimbo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi, kuna Wajumbe 166 ambao watateuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiunge mkono Serikali, naomba nikubaliane na idadi. Kwa nini? Mimi nina imani kabisa na Rais wangu kwamba wale Wajumbe 166 atakuwa makini kabisa na atateua Wajumbe ambao wana vigezo. Nina imani kabisa, wala sitaki kuamini wanayozungumza Kambi ya Upinzani! Atateua Wajumbe 166 wa uhakika, wataungana na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wataungana na wenzetu wa Wawakilishi. Hao tuliopo takribani 600, vichwa vya watu

600 jamani ambavyo viko makini tutafanya kazi ambayo itazaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu kule Upare kuna nyanya zinazoitwa 'wingi si hoja.' Utahitaji nyanya 1000 ili upike nyama ya kilo mbili. Hizo nyanya ni vinyanya vidogo sana, kwetu sisi tunaita 'wingi si hoja.' Ndiyo jina la hizo nyanya. Mnaweza mkawa na Wajumbe 3,000 lakini msitengeneze kitu. Mnaweza mkawa na Wajumbe wa Bunge la Katiba 600, lakini kama kuna umakini, kama kuna *commitement*, kama kuna *seriousness* ya Wajumbe hao, tutatengeneza Katiba itakayotuvusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niunge mkono Serikali, hiyo idadi ya Wabunge 166 watakaoteuliwa na Mheshimiwa Rais wanatosha kuungana na Bunge la Jamhuri ya Muungano na Wawakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia kwenye kifungu cha 24 (4) cha Sheria mama. Hapa naomba Serikali msijifunge sana, najua mmeleta *amendment*, lakini naomba hapo niongee kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isijifunge kuwa Watumishi wa Bunge na Baraza peke yake, kuna Wajumbe wengi ambao ni Watumishi wa Serikali. Kwenye sehemu nyingi ambao nao wanaweza wakateuliwa kuwa Watumishi wa Bunge hili Maalum. Kuna Waandishi wa Sheria, kuna watalaam wa masuala ya Katiba. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali,

katika hili tuchanganye changanye ili mradi wawe ni Watumishi wa Serikali ambao wanajua taratibu zetu.

Baada ya kusema hayo, naomba kwanza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri niwape pole sana katika hii tafrani iliyotokea. Lakini nawaomba msione mko peke yenu, tuko pamoja. Mheshimiwa Waziri Mkuu pole, Waheshimiwa Wabunge poleni. Naomba tuendelee na majadiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

Waheshimiwa Wabunge, kuna miongozo ilikuwa imetoka asubuhi, mojawapo ulitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Mheshimiwa William Lukuvi kuhusiana na maneno yasiyokuwa ya kweli yaliyotolewa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

Kwa jambo lile nitoe tu onyo la jumla kwa Wabunge wote kujitahidi kukumbuka Kanuni zetu, zinasisitiza kuhusu umuhimu wa kusema kweli. Ni jambo la aibu Mbunge kumsingizia Mheshimiwa Rais wa Nchi, ambaye ndiye Kiongozi wetu Mkuu, kwa lugha za aina ile. Katika mazingira ya kawaida, jambo hili lingepelekwa katika Kamati ya Maadili, lakini nawashauri Waheshimiwa Wabunge na kuwaomba kwamba tutoe onyo kwa mara nyingine na mwenzetu wa aina hii tumpuuze tu. Kwa hiyo, hakuna haja ya

kuchukua hatua yoyote. Ninachoagiza ni kwamba sasa yeye na wengine wajikite katika kusema kweli badala ya kujikita katika kusema uongo na kudanganya Watanzania, taratibu ambazo siyo nzuri hata kidogo. *(Makofi)*

La pili, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, tunapokuwa hapa ndani, anayeongoza kikao ndiye Kiongozi wetu. Kwa hiyo, ni vizuri tukamheshimu, tukafuata maelekezo yake. Mtakubaliana nami, toka asubuhi hatujautumia vizuri muda wa Watanzania. Ni gharama kubwa sana kuliweka Bunge hata kwa siku moja, lakini leo mchezo ulioendelea hapa katikati, ilikuwa lengo lake tu ni kuhakikisha kwamba kichwa cha treni kinatoka nje ya reli. Kwa hiyo, imekuwa ni aibu kwa Kiongozi wa Upinzani kuongoza aibu hii iliyotokea, lakini na yeye kama tulivyosema, nia yetu kila wakati ni kuanza upya, Kiti kinamsamehe, hakuna neno. Kuanzia saa 11.00 jioni anaweza akaendelea na vikao na wenzakle wote, kwa sababu lengo letu ni kujenga pamoja, tutengeneze pamoja jambo ambalo ni zuri hapa mbele. Niwahakikishie Watanzania kwa mara nyingine, hakuna upendeleo wa aina yoyote unaofanywa na Kiti, hakuna. Tatizo ni mipango inayopangwa kabla, nje, kuja kuvuruga ndani. Nami wajibu wangu niliowekwa hapa na Watanzania na Waheshimiwa Wabunge hawa, ni kuhakikisha kwamba nawaongoza kwa kile ambacho kimepangwa kwa wakati huo kifanyike na ndiyo wajibu wangu, na lazima nitekeleze wajibu wangu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naomba sasa niwaombe Waheshimiwa Wabunge...

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Anna Abdallah!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa maneno yako ya busara. Mimi nadhani na wenzangu tunakubaliana na wewe. Sasa katika *Hansard* itaonekana maneno yaliyoandikwa ya kumkashifu Mheshimiwa Rais, na kwamba Mheshimiwa Rais ameteua teua tu watu ameokoteza okoteza, jambo ambalo tumeona kama siyo kweli: Je, litabaki bado kwenye *Hansard*?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hilo litahitaji muda kidogo nifanye *consultation.*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naomba sasa niwahakikishie kwamba jioni ni uchangiaji kama kawaida. Naomba mahudhurio yenu yawe mazuri, na tutaanza na Mheshimiwa Hamad Masauni na wengine watafuata.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.21 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae na majadiliano yanaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, naomba Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni awe mchangiaji wa kwanza wakati narekebisha orodha yangu hapa. Mheshimiwa Masauni tafadhali!

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii niwe mtu wa kwanza kuchangia leo jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla sijajikita moja kwa moja katika mapendekezo yangu ya kwenye Muswada huu wa Marekebisho ya Mabadiliko ya Katiba nianze kwa kusema kwamba nimefarijika sana leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana hasa kutokana na maelezo ya kina kabisa ambayo yamewasilishwa na Serikali yaliyotuthibitishia kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshirikishwa kikamilifu katika zoezi hili na kwamba maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yametiliwa maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanasheria Mkuu alisema kwamba kuna oni moja ambalo halikutiliwa maanani, mjadala wangu utaanzia hapo kwamba, katika hili suala la uwiano wa kijinsia nahisi maoni haya pia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yachukuliwe.

Nitatoa sababu baadaye kwa kina kabisa kwa nini nasema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu utaratibu huu ambao umekuwa mrefu sana wa kushirikiana Serikali mbili hizi katika masuala muhimu na mazuri ambayo yanagusa mustakabali wa Taifa letu, ni mambo ambayo yanahitaji kupongezwa na kuendelezwa kwa bidii zote, lakini kulikuwa kuna hoja nyingine hapa imejitokeza, suala zima la ushirikishwaji wa wadau kupitia Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata maswali ya kujiuliza, moja katika swali ambalo nimepata mashaka sana kulifahamu, hili neno wadau. Wadau hasa ni nani? Maana kwa mtazamo wangu, kwa suala zima hili la Katiba na unyeti wake, mdau ni kila mwananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo nimeshangaa sana kuona Kambi ya Upinzani imeshikilia tu baadhi ya Taasisi kwamba hawa ndiyo wadau, lazima hawa washirikishwe. Ningelikuwa niko pamoja nao kama wangenidhihirishia leo hii kwamba ushirikishwaji wa wananchi wote wa Jimbo langu la Kikwajuni pamoja na Taasisi zilipo ndani ya Jimbo la Kikwajuni, lakini na Watanzania wote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wangenidhihirishia kwamba, hawa wananchi wote wa Tanzania hii wangeweza kuitwa na Kamati ile ya Bunge kama kulikuwa kuna uwezekano huo. Lakini kuja tu kupiga

kelele hapa kusababisha vurugu kwa kuzungumzia wadau ambao ni wachache, inanipa mashaka sana, kwamba inawezekana pengine labda wadau hawa ambao wanaonekana kwamba hawajashirikishwa ni wadau maalum ambao mawazo yao yalikuwa yangewafurahisha wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kwa kweli limenipa mashaka sana na hili linanipa mashaka pia katika suala zima la uadilifu wa ndugu zetu hawa. Maana leo hii wangepata fursa kama ambayo amepata Mheshimiwa Rais na mamlaka ambayo amekuwa nayo Mheshimiwa Rais, sijui wange-*misuse* kiasi gani kwamba leo hii katika suala la wadau ndiyo kunaonekana kuna vitu vimejificha. Lakini Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya mamlaka yote makubwa aliyokuwa nayo, amekuwa akiliendesha zoezi hili kwa demokrasia ya hali juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawataka wananchi wa Tanzania waliangalie kwa makini sana hili jambo. Lakini kuna jambo moja ambalo nataka nisisitize sana kwamba, toka lini Mheshimiwa Tundu Lissu anakuwa ndiyo mtetezi wa haki za Wazanzibari, baada ya kutukana tulivyotukanwa kila bajeti inapokuja. Nasema kwamba Wabunge wa CCM wa Zanzibar tuko makini na hatuwezi kufanywa ngazi. Wasemaji wa wana Bunge wa Zanzibar tupo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwashauri tu hasa ndugu zangu wa *CUF* ambao wanacheza ngoma

wasiojua. Nataka niwashauri kwamba, jambo ambalo nilitegemea Waheshimiwa Wabunge wangeiga mfano angalau japo wangu mimi na Wabunge wengine wengi wanafanya hivyo, wa kutumia fursa wanapokuwa hawapo katika shughuli za kazi za Bunge, kuitisha mikutano wananchi wao wakawasiliza. Lakini bila shaka wengine wanahofia kwenda kuonana na wananchi wao, hawana *confidence* kwa sababu pengine hawakufanya kitu chochote katika Majimbo wanahofia masuala mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama wangekuwa na *confidence* pia wangekuwa na *confidence* hapa katika Ukumbi huu kuweza kusimama na kuwatetea kwa sababu wanaamini nini ambacho wananchi wao wanakijua. Kwa hiyo, nasimama kifua mbele leo nikizungumza kinagaubaga kwamba naunga mkono Muswada kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kikwajuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuna mambo ambayo nitayasisitiza na lazima yarekebishwe. Nitayazungumza hayo kwa ufasaha kabisa baadaye kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka nilizungumze, lakini kabla ya kulizungumza nataka nitoe tahadhari kwa wananchi ambao wanatuchagua ili kuwatumikia katika nafasi mbalimbali, kwamba leo hii kama unamchagua Mbunge ambaye anakimbia majukumu yake, Mbunge leo anakuwa msemaji wa Serikali ya Shirikisho, wewe

inakuhusu nini? Mbunge anakuwa msemaji sijui wa wadau, wewe Mbunge ndiyo mdau mkubwa wa Jimbo lako katika chumba hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi ambao mmechagua Wabunge ambao hawajiamini kuja kuwawakilisha muwe makini nao sana, kwamba leo majukumu yao wanawatupia watu wengine. Sisi hapa tutasimamia Sheria hii na tutahakikisha kwamba ina maslahi ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, Wanzibari na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nirudi sasa katika hiki kitabu. Nikienda moja kwa moja, halafu cha kushangaza mapendekezo yenyewe haya ni machache siyo mambo mengi, ni mambo madogo madogo tu siyo ya kuleta tafrani kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono asilimia mia moja idadi ya Wabunge *I mean* Wabunge 166 ambao wamependekezwa wachaguliwe kwa sababu uwakilishi wa wananchi upo wa kutosha, kinachohitajika ni nyongeza ya uwakilishi katika makundi maalum. Pia kupata na watu ambao wana taaluma mbalimbali waweze kusaidia ule mchakato. Hatuwezi kuwa na Bunge la Katiba kama mkutano wa hadhara ama *fete*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huu mchakato wa kuwa na watu hawa 120 ni sawa. Niseme tu nimefarijika sana na lile wazo ambalo limetolewa na Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar kwamba liongezwe

neno Rais atashauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar. Hilo nasisitiza sana liendelee kuwepo. Ingawa katika hiki kitabu naamini itakuwa ni *typing error* kwa sababu Mwanasheria alizungumza kwamba hili kila kitu kimechukuliwa na nimezungumza Mheshimiwa Waziri pale na Naibu Waziri wamesisitiza kwamba hili jambo limechukulikwa kama lilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba waende tu katika *document* ambayo wametupatia inaonekana limekosekana neno kukubaliana, liwekwe pale. Kwa hiyo, baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar. Lakini katika Wajumbe hawa 166 sioni kwa nini wasigawiwe nusu kwa nusu tu. Nusu wakatoka Zanzibar na nusu wakatoka Tanzania Bara. Kwa hiyo, hapo kwanza najaribu kuchangia katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo nataka nichangie katika hii nyongeza ya 2(a), kuna jambo hapa limezungumzwa kwamba linahitaji kuongezwa. Naomba nisilisome kwa kuokoa muda. Lakini ambalo nilitaka kusema ni nini. Ni kwamba tumegundua kuna baadhi ya Taasisi zimetajwa pale; *Institute* na taasisi ya wakulima, Vyama vya Wafanyakazi, lakini kuna wadau wengi tu hawakutajwa. Kwa mfano, mimi huwezi kuja katika Jimbo langu usiwazungumzie watu kama wafanyabiashara, wavuvi, makundi ya vijana mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu tusifike mahali tukajiwekea vikwazo kwamba jamii

fulani tu ndiyo imeorodheshwa. Tutanue wigo, tutoe fursa kwa makundi yote na vile vile tusimbane Rais. Leo nyinyi mmeshuhudia hapa, alizungumza hapa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi kwamba, Chama cha Demokrasia na Maendeleo kimepeleka majina matatu, moja katika majina yaliyopelekwa ni la Profesa Baregu na lingine la Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi Profesa Baregu kwa kuwa anasimamia misingi ya uzalendo na maslahi ya Taifa, leo chama hiki kinamwona kwamba ni tatizo. Sasa tujalie kwamba katika mapendekezo yale matatu halikuwepo jina la Profesa Baregu, tunaweza kuona kwamba katika Tume ile tungepata watu ambao wanaweza wakasababisha mambo ambayo kama tulivyoona hapa leo hii. Kwa hiyo, nataka nitoe wito kwamba Rais asibanwe, aachiwe fursa ya kuweza kuchagua ikiwezekana nje ya mapendekezo ya wale watatu ambao wametolewa akiona kwamba kuna haja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo naitilia nguvu zaidi kwa sababu ukiangalia mapendekezo mengine chini yanasema kwamba, inatakiwa izingatiwe sifa na uwezo wa mhusika, lakini pia uwiano wa kijinsia. Sasa ikitokezea kwamba kuna mapendekezo ya majina yale matatu ambayo hayana sifa ama hayakuwiana kijinsia ina maana tumembana Mheshimiwa Rais asiweze kuwa na wigo mpana wa kuweza kupata Wajumbe ambao wanaweza kusaidia Bunge letu kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niliona nipendekeze hivyo, lakini nataka ile imeishia kwenye namba tisa ya Kirumi, iendelee na namba 10 na isomeke hivi: "Ama Rais atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya mapendekezo hayo machache, nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM. Kwanza kabisa kwa kuona mbali kwamba, hili zoezi ni vizuri hata kama halikuwepo katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM, lakini akaona kwamba ashawishi chama tuweze kulikubali na leo hii wale ambao walikuwa na *agenda* ya kusema kwamba CCM hatutaki Katiba mpya, inaonekana wao ndiyo hawana haja ya Katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mambo mengi ambayo ni Rais huyu anaambiwa apunguziwe madaraka ambayo chini ya uongozi wake yamefanyika na hawa Upinzani sidhani kama wanapaswa kuyabeza. Leo hii Zanzibar kule, kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo chini ya Uongozi wa Rais huyu huyu, ndiyo mambo haya yamefanyika. Kwa hiyo, inashangaza mtu huyu huyu leo kwenda kunywa *juice* Ikulu, sawa, kusimamia uanzishwaji wa Serikali ya Kitaifa sawa, sijui kwenda kusimamia mchakato wa Katiba sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuingiza katika Tume watu wengine, nasema, inashangaza kwa kweli. Nataka niombe radhi sana, lakini inashangaza sana kwamba baadhi ya Wajumbe wa Tume ambao

wamechaguliwa wanafika mahali wanashindwa kuficha hisia za jaziba na utashi wao. Kazi yao ni kutafuta maoni ya wananchi, lakini wao ndiyo wamekuwa wasimamizi na wapigaji debe wa jambo ambalo wanalitaka wao na kushinikiza jambo wanalolitaka. Kwa hiyo, kwa yote haya yamefanyika na Mwenyekiti huyu alikuwa ana fursa ya kuweza kushinikiza, lakini amesimamia kwa uadilifu na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri mchango wangu ulikuwa ni huo tu. Nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Masauni. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Zambi. Mheshimiwa Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kukupongeza sana wewe kwa namna ambavyo leo umeendesha kikao hiki cha Bunge tangu asubuhi mpaka ulipositisha shughuli za Bunge mchana, tukaenda kupumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa sababu leo umekuwa mvumilivu wa kupita kiasi na Watanzania wameona. Wenzetu leo walikuwa

wanatafuta namna tu ili wafukuzwe au watoke ndani ya Bunge, lakini hukutaka kuwapa nafasi. Mwisho wakaona wavunje hata taratibu baada ya kukubaliana kwamba tukipiga kura hapo tutakuwa tumemaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Watanzania kura waliomba wao zipigwe. Naibu Spika akawakubalia, wakashindwa kwenye kura, wakaona haliwezekani, wanainuka tena kwa ajili ya kuleta hoja nyingine za ugomvi usiokuwa na sababu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa misingi hiyo naomba nikupongeze sana sana sana. Sanjari na hayo, naomba nimpongeze sana *AG* kwa maelezo mazuri aliyotoa, maana ametoa darasa hapa ndani. Kwa wale wanaojiita Wanasheria, lakini hawazijui sheria, nataka niamini hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpongeze Mheshimiwa Lukuvi maana naye amewathibitishia Watanzania kwamba, wenzetu waliyokuwa wanakuja kutueleza hapa ndani ni ya uongo. Unaposema Mheshimiwa Rais ukamsingizia kwamba, amechagua watu ambao hawakupelekwa na Taasisi ambazo zilihitajika zipendekeze. Halafu baadaye Serikali ikathibitisha kwamba huyu anasema uongo, wote walioteuliwa na Rais walipendekezwa na Taasisi zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo inakuwa ni aibu kwa wenzetu wa Kambi ya Upinzani na Watanzania wanapaswa wawajue watu wa namna hiyo. Hawa ndiyo wanaotaka madaraka kwa udi na uvumba. Sasa wakitaka madaraka watakuja wawachinje Watanzania bila shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaeleze Watanzania kwamba, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambao tumeaminiwa na Watanzania pamoja na Serikali yetu, tunawajali Watanzania, tunawapenda Watanzania, wala hatuna sababu ya kuwaingiza Watanzania kwenye shimo, lazima wajue kwamba na sisi ni Watanzania, ni wazalendo wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wao wasije wakajifanya kwamba, wanayoyapigania maana yake sisi tunaona wanayapelekea wananchi wetu shimoni, hapana, tuna uzalendo mkubwa, tunaipenda nchi yetu, tunawapenda watu wetu na naomba waamini kwamba tunawawakilisha na yale mabadiliko ambayo Serikali inaleta katika Muswada, kwa kweli yananuia tu katika kurekebisha au kuboresha yale mambo machache ambayo yalikuwa kwenye Muswada wenyewe ule wa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache sana, labda mawili. La kwanza ambalo lipo kwenye kifungu cha 22(a) ambacho kimeongezwa, naomba Serikali ikiangalie tena vizuri. Katika kifungu hicho kinasema kwamba, yule atakayechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda wa Bunge Maalum, baada ya

kumaliza kazi hiyo, asiruhusiwe tena kugombea Uenyekiti wa Bunge Maalum lenyewe. Sasa mimi hapo naona kwamba tunaweza tukampata Mwenyekiti wa muda mzuri na baadaye akaendesha vizuri. Tukapendezwa naye kwamba anaweza akatuendeshea Bunge vizuri, lakini unapomfunga hapa kwamba asigombee tena, nadhani Sheria zile zitakuwa hazitendi haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Sheria inatenda haki, acha watu ndiyo wakatae wenyewe, lakini tusimfunge kwenye Sheria kwamba anayechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda asigombee tena. Hilo sikubaliani nalo na naomba Serikali itafakari upya kwamba tumchague mtu kwa sababu ya *merit* zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama itatokea huyo huyo ambaye amekuwa Mwenyekiti wa muda amefanya vizuri na Wajumbe wakaamini kwamba anaweza na akagombea nafasi hiyo, basi tumpe. Maana Wabunge wenyewe wa Bunge hili ndiyo watakaoamua nani, lakini Sheria isifunge kwamba ukishakuwa Mwenyekiti wa muda, basi huko mbele asiende. Hilo naomba Serikali iliangalie upya. Sidhani kama litakuwa linatenda haki kwa kulifunga namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine dogo ambalo ningependa nilizungumze na wenzangu wengi wamelizungumza, ni suala la Wajumbe 166. Katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo tayari Mheshimiwa Rais alishaisaini, Wajumbe hawa 166

walishapitishwa na tulishakubaliana kwenye Bunge hili. Tulipokubaliana wakati ule hakukuwa na mtu yeyote ambaye alipinga Wabunge 166, wakiwepo na wenzetu wa Upinzani, hawakupinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua hata walipoomba wao kwenda kumwoma Mheshimiwa Rais, akawakubalia wakaenda Ikulu, mambo mengi waliyoyapeleka Mheshimiwa Rais, aliyakubali. Hii haikuwa moja ya ajenda waliyoipeleka, leo wanakuja na jambo lingine. Nadhani wenzetu hawana nia njema, kama walivyosema hawataki tutoke hatua moja kwenda nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wamesoma tu wameona upepo kwao sio mzuri. Kwa hiyo, wakaona sasa tuje na idadi ya Wajumbe 334 na wakifikiri hao 334 basi wote watakuwa labda wa upande wao. Nadhani hili wala Watanzania wasibabaishwe nalo na wawaone wenzetu hawa ni wanafiki, kwa sababu wakati ule tulipokuwa tunatunga Sheria ile, kama nilivyosema halikuwa-*issue* hata kidogo na walikubali kwa asilimia mia moja, leo wameona nini? Haya ndio mambo ambayo tunasema Watanzania waone, Watanzania wapime kwamba, hivi watu wa namna hii tukiwapa nchi leo, wanaweza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wako kwenye *learning process,* bado wanahitaji wajifunze labda miaka mingine 50 inayokuja. Ni kweli, wanahitaji kujifunza miaka 50 mingine inayokuja, lakini nataka niwadhirihishie Watanzania na sioni Rais katika wale

ambao wanataka Urais kupitia Kambi zao za Upinzani, hata wale tunaowasikia sijamwona Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Watanzania wanataka hii nchi iende kwenye majaribio kwamba, wamechoka sasa na amani, wanataka kuipeleka nchi kwenye majaribio, basi wahangaike na wenzetu ambao wakati wote wao wamekuwa ni kuigombanisha Serikali, iliyoko madarakani na wananchi; sasa huwezi kutawala nchi namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kama ukiwagombanisha wananchi na Serikali iliyoko madarakani, kama ikija hiyo miaka 50 inayokuja labda ndio wakatawala, hivi hao watakaokuwa wanawaangalia wao, watataka watawale bila matatizo yoyote na wenyewe watajengewa mazingira mabaya ya kutotawala. Kwa hiyo, tunawaomba Watanzania wanaopenda mema, wanaoitakia heri nchi yetu, wasikubaliane na mambo yanayoenda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nimesema sina mambo mengi, naomba niipongeze sana Tume ya Jaji Warioba kwa kukataa maboksi yale sijui kumi na ngapi, eti ya Watanzania milioni tatu ambao walipata maoni kwenye mikutano ya hadhara. Muda wa mikutano ya hadhara kuchukua maoni ulishapita na ningeshangaa sana kama Tume ingeyapokea maoni yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakwenda kwenye mikutano ya hadhara, watu wanazungumza, wanaleta ushabiki wa vyama, leo unayaleta kwamba, ni maoni ya Watanzania wanataka Serikali tatu, haiwezekani. Naipongeza sana Tume kwamba, imetenda haki kwa kukataa maoni yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, sina mambo mengi zaidi ya kuwataka Watanzania watuelewe, wafahamu kwamba, ni watu gani ambao tunataka kutawala nchi hii. Pia Watanzania watuelewe kwamba na sisi ambao ndio tumeaminiwa na Watanzania walio wengi, tunawapenda Watanzania na wengine tunawatumikia Watanzania kwa uaminifu. Tunawasemea Watanzania na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inajitahidi kuhakikisha kwamba, Watanzania hawa wanapata maisha mema kadiri ya hali ya bajeti na uchumi wa nchi unavyokua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Godfrey Zambi. Sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru sana Mungu kwa uzima na afya njema hadi nikafika siku hii ya leo. Pia nakushukuru binafsi wewe mwenyewe kwa kunipa

fursa hii ili niweze kuchangia Muswada huu wa Marekebisho ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kipekee kabisa nikupongeze kwa jinsi ambavyo umeendesha Bunge lako Tukufu asubuhi hii ya leo. Umeonesha diplomasia ya hali ya juu sana na Watanzania wamesikia, Watanzania wameona, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuridhia mchakato huu wa Katiba. Naomba niwaeleze Watanzania kwamba, Tanzania Kwanza – Uzalendo Kwanza na sisi tuko hapa kwa ajili ya kuwawakilisha wao kwa maana ya kwamba, tuko kwa ajili ya Utanzania, tuko kwa ajili ya uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa Katiba ni mgumu sana. Sisi kama wawakilishi wa wananchi tunatakiwa tubishane kwa hoja, wala sio malumbano na kama tunashinda tushinde kwa hoja, kwa afya na manufaa ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya kuokoa muda sitasoma, lakini naomba ninukuu ile Kanuni ya 86 ya Kudumu ya Bunge, Ibara ya 10, ambayo inaruhusu Mtoa Hoja kuleta mabadiliko wakati wowote na ndicho Serikali, ambacho imekifanya. Kwa hiyo, sioni kosa liko wapi na sioni tatizo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu kile cha 22 cha Sheria Mama, Kifungu kidogo cha 1(c); naomba niseme kabisa, mapendekezo ya Serikali, ninayaunga mkono kwa asilimia mia moja na moja ya kumpa Mheshimiwa Rais, mamlaka ya kuteuwa wale watu watatu ambao wamekuwa *nominated* kutoka katika Taasisi mbalimbali, ili yeye aweze kuchagua mtu mmoja katika wale watu 166. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaposema kwamba, Rais asiteue; kwanza, tukubali na tuangalie kabisa kwamba, haya majina matatu yanakuwa *nominated* na hizi taasisi mbalimbali na Rais yeye atakapoteua, anateua kutokana na yale majina matatu, kwa maana hiyo demokrasia yenye uwigo mpana kabisa hapo inakuwa imeshatumika. Kwa hiyo, sielewi kabisa ndugu zangu wanacholalamika hapo ni nini kwa sababu, hayo majina matatu yanakuwa yametoka katika hizo taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika ukurasa ule wa mwisho, hizi Taasisi mbalimbali ninazozizungumzia ziko 16. Kwa maana hiyo, kama ni Vyama vilivyosajiliwa viko zaidi ya 20. Sasa chukulia kila chama kinatoa majina matatu, sasa hiyo bado tunasema ni demokrasia na bado sielewi wala haipandi akilini kwamba, mtu anapolalamika analalamika kitu gani na wakati demokrasia ya kweli inakuwa imetumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zile siku 20 za kuongeza *apart from the 70 days,* nashauri kama

wenzangu wengi ambavyo wamesema, zisiwe *mentioned,* zile siku 20 za nyongeza kwa sababu, je, endapo hizi siku zitakuwa zimeongezeka tutafanyaje? Matokeo yake bado tutaanza kuwa na mlolongo mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ningependa kukichangia au likawa ni angalizo langu; kwenye Hotuba ya Kambi ya Upinzani, hili wamelizungumzia sana. Naomba kwenye angalizo tuangalie sana, mwaka kesho tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Uchaguzi Mkuu na muda uliobaki ni mfupi sana. Kwa hiyo, endapo *if worse goes to worst,* basi tuweze kufanya *some amendments* ili hakika tuweze kuangalia kabla ya Uchaguzi Mkuu ni vitu gani vitaingia ili uchaguzi Mkuu wa Serikali za Mitaa, uweze kufanyika kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisiwe mzungumzaji sana katika jioni hii ya leo, maana naomba sana na namwomba Mungu nijikite katika mada ambayo iko Mezani siku ya leo nisiende nje ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, naomba niwaambie Watanzania wenzangu tena kwamba, sisi tuko hapa kwa ajili ya Watanzania wote na Tanzania kwanza, uzalendo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa. Katika mchango wako nilidhani kwa niaba ya Wanambeya Mjini, utaomba radhi kwa kutung'olea vipaza sauti na kufanya vurugu kuwa sana humu. Naona mmeamua kukaa kimya watu wa Mbeya.

Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala. Atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Chomboh. Mheshimiwa Kigwangala!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niitumie fursa hii vizuri kwanza kwa kuomba dua kwa Mwenyezi Mungu, aniongoze nitoe mchango ambao una tija na ustawi katika Taifa letu. Lakini pia naomba nitumie fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niseme machache nitakayojaliwa, lakini pia nikupongeze sana kwa ujasiri na umakini uliouonesha wakati ukiendesha Kikao cha Bunge, asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati ilifika wakati yule bwana anaambiwa atoke nje, akawa hatoki, mimi nikashika Kitabu cha Kanuni. Nikasema labda nimpige Mwongozo hapa, nimwombe tu atumie busara ya kawaida amwambie Mheshimiwa Mbowe aongee, halafu tuendelee na Bunge, maana nilipata mashaka kweli, lakini nikaona umeamua kushikilia palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyokuona uko imara, nikasema nitakuunga mkono kwenye uamuzi wako. Ni

bora ulisimamia kauli yako maana baadaye heshima yako ilionekana umeilinda ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ningekushauri umruhusu Mheshimiwa Mbowe, aongee wakati ulikuwa umeshatoa agizo kwamba, akae chini akabisha na ukasema atolewe nje, ningekuwa nimekushauri vibaya kwa sababu, tungekuwa tunaendelea kulealea upuuzi wa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii haiwezi kuendelea kama tutaendelea kuulea upuuzi. Kuulealea ujinga wa namna hii kama uliofanyika hapa siku ya leo, nchi haiwezi kuendelea hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze kwa kusimamia kauli yako, kwa kusimamia uamuzi wako na nasema niko na wewe katika uamuzi wa namna hiyo siku zote kama utaendelea kufanya hivyo. Haya ndio yale, kuna mtu mmoja aliwahi kusema humu Bungeni, kufanya maamuzi na kuyasimamia maamuzi; umefanya maamuzi sahihi na ukayasimamia mpaka dakika ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonifurahisha ni kimoja. Baada ya ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, kubebwa msobemsobe hapa mpaka nje, nikaona na yule mwingine ndugu yangu Msukuma, Mheshimiwa Kasulumbayi na urefu wote ule na u-*giant* wote ule, kanyanyuliwa juu kuliko kile kikundi chote pale, nikasema kweli, Dola inafanya kazi. Nikaona na

yeye anaanza kuwaambia nishusheni nitembee mwenyewe tu nitoke nje, nikasema Dola iko kazini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndio Serikali tunayoitaka. Hiyo ndio aina ya Serikali tunayoitaka, Serikali inayosimamia maamuzi yake, Serikali inayosimamia maagizo ya Viongozi yanapotolewa. Niwapongeze sana wenzetu *Sergeants of Arm,* Askari wa humu Bungeni na wale wa nje walioingia kwa kuhakikisha amani inakuwemo ndani ya Bunge hili. Nawapongeza sana huko mliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kilichonifurahisha zaidi, baada ya kuona sasa Dola imeingia kwa nguvu kabisa, kwamba iko *serious* inawatoa nje, nikamwona Mheshimiwa Mbowe, ametepeta. Mheshimiwa Mbowe, akatepeta, akaanza mwenyewe kuongoza, moja, mbili, tatu, nikasema ameshikishwa adabu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikajifunza kitu kimoja maana Mwanafalsafa mmoja aliwahi kusema, ukikutana na watu ama ukakutana na tukio kuna mambo mawili ya kujifunza, aidha mambo mazuri ama mambo ya hovyo ya kishetani. Lakini nikajifunza jambo moja zuri kwamba, kama Serikali, ikiwa inafanya kazi yake ipasavyo, watu wataheshimu Dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwona hapa leo na macho yangu, Mheshimiwa Mbowe, akiheshimu Dola, alitoka kwa hiyari yake mwenyewe; japokuwa

alitoka kama bibi harusi, taratibu taratibu, lakini alionekana ameheshimu Dola na ameiogopa Dola. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana nilivyoona wale Askari wanaingia kwa mara ya pili, wanavua tai, nikajua shughuli imeingia hapa, nikajua shughuli inaingia hapa. Bila ya shaka macho yangu hayakuwa mbali na macho ya Mheshimiwa Mbowe, kwa sababu na yeye nafikiri aliwaona wakati wakivua tai, akajua sasa nabebwa na mimi, itakuwa aibu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aibu hii aliyoifanya Mheshimiwa Mbowe hapa, inanisikitisha sana kwa sababu, Mheshimiwa Mbowe, amepata bahati kubwa ya kuoa Daktari. Ameoa Daktari mwenye heshima kubwa sana, ambaye kwa sisi Madaktari tunaitana *colleagues,* ni *colleague* wangu. Sasa yaani sijui yule Daktari kule alipokuwa, halafu akawa akimwangalia mume wake hapa, ambaye amepewa majukumu makubwa na wakwe zangu kule Hai, mimi nimeoa kule kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbowe, amepewa majukumu makubwa kuja kuwawakilisha hapa wale Wamachame, halafu kafika hapa anafanya upuuzi kama ule. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza huyu mtu ni Kiongozi wa ngazi ya juu kabisa kwenye chama chake. Kwa tabia za kiuongozi, kwa sisi viongozi, kuna wakati ukifika umezidiwa hoja, umeonewa, lakini ukikumbuka kwamba, wewe ni kiongozi, unatakiwa uheshimu

kwamba, mimi ni kiongozi nina watu nyuma yangu, maamuzi ninayoyafanya hapa yanawaathiri wale watu, yanawaumiza wale watu. Unachukua staha ya kiuongozi, unavaa heshima yako, unakaa kwenye Kiti chako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kweli, amewaaibisha sana wakwe zangu wa kule Machame, amewaaibisha sana; wengine wamenipigia, wanasema sasa huyu inakuwaje? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia Bwanashehe huyu Mbowe, ana matatizo. Si Mchaga kama wale Wachaga wengine, *enterprising, smart,* wenye hekima na busara ambao wanaendesha dunia ya biashara katika Taifa letu. Nikasema huyu sio wa aina ile, huyu pengine ni aina ile nyingine ya kihuni, ya mtaani ya mjini huku Uswahilini na sio wa aina ile ya kule kwenye migomba, kwa sababu, kwa cheo alichonacho, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, hutegemei angeweza kufanya alichokifanya hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kikubwa kilichonishangaza ni kwamba, Tanzania ipo katika *transition period,* ipo katika kipindi cha mpito. Kwa sisi viongozi vijana kipindi hiki ni muhimu sana katika historia yetu ya uongozi wa Taifa hili kwa sababu, kibaiolojia tuna fursa ya kuishi miaka mingi katika nchi hii kuliko wazee wetu wengine waliomo humu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, tuliopata fursa hii ya kuwepo katika mchakato huu wa kuandika Katiba Mpya ya Taifa letu tunatakiwa tuwe makini zaidi kuliko hata hawa wazee wanaotuongoza leo, kwa sababu, ya *institutional memory.* Kwamba, miaka 10 ijayo, miaka 20 ijayo, kama tutapata bahati ya kuendelea kuwemo katika uongozi wa Taifa hili tutakuwa wazee na tutakuwa tukitoa ushauri kwa vijana ambao watakuwa wameingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kibaya zaidi, badala ya sisi vijana kushiriki katika mchakato huu wa kuandika Katiba Mpya, sasa hivi tunataka tupitishe Sheria ambayo itatupeleka kwenye kuandika Katiba Mpya, ili tufanye mabadiliko makubwa ya kiuongozi ambayo yataongoza uchumi wetu na kuleta maendeleo kwa watu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume chake sisi vijana tunakuwa wa kwanza kubebwa msobemsobe kama Mheshimiwa Sugu na Polisi kwenda nje, badala ya kutulia, tutoe mchango wetu, tulete *dot-com* zetu humo kwenye Katiba, ili basi mawazo yetu yawe *incorporated.* Tuwawakilishe vijana wenzetu huko nje wanaotusikiliza, sisi tunakuwa wa kwanza kufanya vurugu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kubwa sana kwa sisi viongozi vijana. Vijana wenzetu huko nje tunawanyima fursa, wazee wataanza kuwadharau vijana, watasema hawa vijana ukiwapa majukumu makubwa yanawashida. Wakifika Bungeni,

wanafanya fujo, wanafanya vurugu, badala ya kupeleka usomi wao humo Bungeni, badala ya kupeleka hekima, badala ya kujifunza, wanakwenda kufanya vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kwa kazi nzuri waliyoifanya leo. Walichokisema, kama ingekuwa ni matakwa yangu ningesema hii Sheria ipite kama ilivyo kwa sababu moja. Hoja kubwa ambayo imewafanya hawa wenzetu watoke nje, katika sura iliyopo kule nje ni kwamba, wadau hawakushirikishwa, wadau hawakushirikishwa kwenye nini? Hili ni swali lenye thamani ya bilioni moja; wadau hawakushirikishwa kwenye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatunga Sheria Bungeni, hiyo ndiyo kazi ambayo tunapewa sisi Wabunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini leo hii mtu anataka kulazimisha sisi tupate mawazo ya wadau wakati mimi nina wapiga kura wangu karibu 500,000 ambao ninawawakilisha, ambao ningepaswa kwenda kuwauliza wanataka nichangie nini kwenye Muswada huu kabla sijaja Bungeni ili nije nikiseme hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wadau ni nani hawa na wako wapi kwenye Sheria zetu, wako wapi kwenye Katiba yetu, wako wapi kwenye kanuni zetu za Bunge, hawapo sehemu yoyote ile. Ni matakwa ya Kamati husika kushirikisha wadau kadiri inavyoona ili

wapate ushauri kutoka kwa watu wengi ambao wanatarajiwa kuwa ndiyo watumiaji wakubwa wa Sheria ambayo inatungwa, lakini siyo lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaonisikia waelewe hili, siyo lazima kushirikisha wadau, kazi ya kutunga Sheria kwa mujibu wa Katiba ni ya Wabunge na ilitakiwa ifanyike hapa leo. Wenzetu hawa wangekuwa na busara za kiuongozi wangejipanga kutoa hoja hapa, wangejipanga kuleta *amendments* hapa na siyo kutoka nje ya Bunge kwa sababu kazi majukumu matatu ya Mbunge la kwanza ni kutunga Sheria, la pili ni uwakilishi, la tatu ni kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukishatoka hapa maana yake umeondoa asilimia yote mia ya Ubunge wako, kwa sababu unatakiwa uwepo hapa uwakilishe watu wako, hata kwa kusikiliza tu, uwakilishe watu wako, sasa hawa watu wametoka wamemwakilisha nani. Hawa watu waogopwe na wanyimwe kura wakati mwingine ukifika, kwa sababu hawakai Bungeni, tunafanya kazi ya Kibunge hapa, tunatunga Sheria, watu hawakai Bungeni maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba wanawasaliti watu waliowatuma hapa. Sasa maana yake kama mimi nikitoka hapa leo hii, watu takribani laki tano kutoka Nzega waje wakae kwenye kiti changu ama vipi? Ningetakiwa niwaulize Wananzega wanataka nini na hicho ndiyo nikilete hapa Bungeni sasa kuliko mimi nitoke ama nitoroke Bungeni nikafanye

mambo mengine eti kwa kisingizio kwamba wadau hawakushirikishwa, wadau wananguvu gani ya kutunga Sheria zaidi ya sisi wenyewe watunga sheria ambao tuko hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini muda mpaka hapa nilipofikia siyo rafiki sana, lakini nimesikiasikia za chini ya mti hapo nje kwamba hawa watu wanataka mchakato wa Katiba usiishe kufikia 2015. Kwa hiyo, wanatuchelewesha kwa makusudi, hawana sababu nyingine, kama wanaogopa kwamba 2015 ni mapema mno na hawajajipanga huo ni uoga wao lakini sisi tunataka ngoma iwekwe kati 2015, tuwapige tena kama tulivyowapiga 2010, ndiyo tunachokitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kusogeza mbele ratiba miaka yetu miwili iliyobaki, ngoma iwekwe kati, tucheze, atakayeshindwa ashindwe, atakayeshinda ashinde kwa sababu wao walitaka hii Katiba, Rais amewapa mchakato, mchakato umeanza wanaanza kuu-*frustrate* kwa sababu gani, *why should they frustrate the system why?*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni lazima wana yao yaliyojificha, kama hawataki hivyo leo hii tukiamua sisi ambao tuko wengi hapa Bungeni kwamba basi tuache hatutaki hiyo Katiba mpya, hatutaki turudi kwenye ile ya zamani nani ameumia? Maana yake sisi CCM hatukuwa tunataka Katiba mpya hii, waliokuwa wanataka Katiba hii ni *CUF*, CHADEMA, *NCCR* hao ndiyo waliokuwa wanapiga kelele toka mwaka 1995 mpaka leo wanapiga kelele Katiba

iandikwe upya. Sasa leo wamekuwa *granted okay, now* tunaanza mchakato wanaanza kuleta vurugu, *why?*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake wanatuchezea akili, hii ni akili kama ya shetani hata ukimficha kwenye chupa lazima atanyoosha kidole, ndiyo akili za namna hii.

**MBUNGE FULANI:** Siyo shetani, mwanaharamu.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** mwanaharamu eeh?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Ndiyo akili za namna hiyo wanataka tu wajioneshe kwamba na wao wapo, wanavurugu, wana nini, lakini huu ni ushetani. Hatuwezi kukubali mambo ya namna hii, kwa sababu kama tukiamua sisi *okay* tuachane na hii Katiba, nani anaye-*loose*. Kwa sisi viongozi vijana ambao tunataka tupate mambo mapya tunavyoingia kuchukua hii nchi, tuchukue nchi ikiwa na Katiba mpya na mambo ambayo tumeshiriki kuyatengeneza, basi tuiendeleze tu nchi yetu mbele, wao wanachokifanya hawa watu ni kutu-*frustrate* tusiandike Katiba mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tukiacha kuandika Katiba mpya maana yake nini? Maana yake tunarudi kwenye Katiba ya zamani kuna ubaya gani, kwa CCM tunasherekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema, naunga mkono hoja na nawapongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa mchango wako na kwa sababu sote tupo katika Kamati mbalimbali tuendelee kusisitiza utaratibu wetu na kukumbushana namna Kamati zetu zinavyofanya kazi. Ni kwamba wadau wanafuata Kamati, Kamati haifuati wadau.

Ndiyo maana juzi hapa tulikuwa na Sheria ya Ushirika, maeneo makubwa ya Ushirika ni korosho, pamba, tumbaku; Kamati ya Kilimo haikwenda Mtwara Kusini, wala haikwenda kwenye tumbaku, Tabora, wala haikwenda kwenye pamba, Shinyanga wala wapi; kama walikuwepo wadau waliifuata Kamati hapo ilipokuwa na ndiyo utaratibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chomboh atafuatiwa na Mheshimiwa Lwanji. Mheshimiwa Chomboh!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kusimama jioni hii. Pia nakushukuru wewe kunipa nafasi ya kuchangia katika mada iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwanza kwa masikitiko makubwa kwa ndugu zangu hasa wa Chama cha Wananchi *(CUF)* ambao wengi wao

wanatoka Zanzibar ninakotoka mimi, kwa kususia mjadala huu na kuacha kutoa maoni yao kwa kisingizio ambacho kisheria na kiutaratibu hakipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote hapa katika Bunge, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ametuthibitishia ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini pia Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba naye pia ametuthibitishia ushirikishwaji wa wadau kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio chao ndugu zangu walikuwa wanasema kwa nini Kamati haikwenda Zanzibar, lakini kilio cha msingi wangeuliza kwa nini Serikali ya Zanzibar haikushirikishwa, siyo Kamati kwenda Zanzibar, muhimu ni kushirikishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, haikwenda Kamati lakini kaenda Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri wa Sheria na akakutana na Waziri mwenzake kule na Mwanasheria mwenzake kule na wakakubaliana na wakayaleta ambayo waliyapendekeza wao kwa niaba yetu. Sisi ilikuwa leo hapa ni kushirikiana na wenzetu na kuweza kutoa mchango wetu kwa maslahi ya nchi yetu na maslahi ya Katiba hii ambayo tunaitegemea Mungu akijalia ifanikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu hawa walichokifanya kwa kweli kimenisikitisha sana kwa sababu sikutegemea kabisa, nilijua leo sisi na wao

tungeungana pamoja kuchangia mchango huu. Wamekwenda kumfuata mtu ambaye kwa kawaida yake, namzungumzia Msemaji wa Kambi ya Upinzani, huyu haijatokea hata siku moja akaipenda Zanzibar, akaupenda Muungano na anathubutu kusema hadharani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati fulani vipindi mbalimbali alikuwa akitoa maoni yake ya Kambi ya Upinzani hutumia pia maneno ya kuwajaza chuki Wanazanzibari kwa kuwakumbusha watu ambao walipatwa na maafa wakati huo toka 1964 jambo ambalo limeshapotea miaka hamsini karibu sasa hivi. Jana akajidai kujipamba kwamba Zanzibar haikushirikishwa na maneno na ndugu zangu wakajaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ndugu zangu hawa kama miezi mitatu nyuma walikuja wakaikataa Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA na wakathubutu kusema Mwenyekiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani aliyoyatoa ni ya CHADEMA siyo ya *CUF* wala Kambi ya Upinzani. Alikuja kutamka maneno, kaja kafanyafanya hivi hapa, kaondoka, sitaki kuyarudia yale aliyosema. Kumbe bahati mbaya kile kitendo alichokifanya yule Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani, ule upepo umewalewesha, wamelewa leo wamekuwa wawele, uwele ni ule kwamba hujijui, wakabwebwa na upepo hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwafanyii haki wenzetu, hatuwafanyii haki Wazanzibari wenzetu. Nataka kuwaambia ndugu zangu kule Zanzibar,

mnanisikia na mnaniona kinachofanyika hapa hii Sheria ambayo tunaifanyia marekebisho hapa ni Sheria ambayo imeshapita wakati mwingi sana na wenyewe wote walikubaliana na imeshafanya kazi na ndiyo kufika hadi ikaundwa Tume, Tume imekuja huko, imechukua maoni na ikafika ikawapelekea kwa Kamati ya Tume ya Maoni ile ambayo imetoa rasimu, rasimu inaendelea kuchambuliwa. Sasa hivi kinachooonekana hapa ni mambo madogo madogo tu ambayo mambo hayo pia kiutaratibu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo gani ambalo linataka lazima Kamati au Tume au Kamati ya Katiba iende Zanzibar kwa sababu gani. Wamealikwa na wamekuja, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria amewaalika watu na wamekuja. Wamekuja viongozi wa *ADC* kama alivyozungumza, wamekuja Chama cha Jahazi Asilia, lakini pia wawakilishi wa Tume ya Uchaguzi wamekuja wamekaa nao wiki nzima katika kubadilishana maoni yao, sasa tulikuwa tunataka nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninavyozungumza na bahati nzuri Waziri wa Sheria kule ni muasisi na mkereketwa mkubwa wa Chama cha *CUF*. Sasa hawamwamini hata huyo Mwanasheria pamoja na Waziri wa Sheria. Kitu ambacho kinanishangaza hapa hawa watu wote, wawakilishi wa Chama cha CUF na wao ndiyo waliotoa mapendekezo hayo, sasa kipi kilichojiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri bahati mbaya sana hawa, walilewa huo upepo. Kule sisi watu wa pwani, kuna samaki mmoja anaitwa kitatange, huyu kitatange ni samaki mjanja sana, yeye unapokwenda kutega mtego wa samaki tunaita dema kule baharini yeye hukaa pale karibu na mlango wa lile dema anajihifadhi, samaki wengine wanafikiri pale kuna chakula, huingia tele ndani ya dema, yeye baadaye huyo aenda zake, huu ndiyo mpango wa Tundu Lissu kwa Zanzibari.

Mheshimiwa Naibu Spika, anajidai kutusifu, akajidai kama anaona uchungu sana, matokeo yake anakuja kuwapiga chini. Nataka kuwaambia ndugu zangu, nyinyi Wabunge wenzangu, lakini pia na wale ndugu zangu Wawakilishi ambao watakuja katika Bunge hili la Katiba na wengine hao watakaokuja kuchaguliwa na Mheshimiwa Rais, huyu ndiyo yule yule Tundu Lissu, mnamjua na mnafahamu tafadhalini tujihadhari na mtu huyu. Tafadhalini sana tujihadhari na mtu huyu tutakapokuwa tumeshikamana katika Bunge letu la Katiba, tuje tuiteteeni Zanzibar kwa maslahi ya Zanzibar, tusije tukaleweshwa na upepo huo uliowalewesha wenzetu leo. Hawa najua leo wakishakuwa tayari huko watagubuka kwa maneno haya na Mungu atawasaidia mgubuke, hatujakwenda mbali bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya wajumbe hawa 166 na wanatosha kabisa na kwamba tutachaguliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akishauriana na Mheshimiwa

Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naliunga mkono hilo na kwa idadi hiyo 604 kwa mujibu wa taratibu inatosha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja zuri nataka kuwaambia ndugu zangu hasa kule Zanzibar, huu siyo mwisho wa mambo yote, hata hilo Bunge lenyewe tunapokuwa tunakaa ndani ya Bunge, Wazanzibari watakaa upande wao na Watanzania bara watakaa upande wao na hakipitishwi kifungu kama theluthi mbili ya kundi mojawapo halijakubaliana, tatizo liko wapi na hayaishii hapo, hii baadaye itakuja kwenu kupiga kura za maoni, mna ujuzi, mna uzoefu, mmeshawahi kufanya hivyo, tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachofanya hapa ni kuboresha ili huko mbele tusije tukakwama na haya mambo madogo madogo ya kisheria. Kwa hiyo, nawaombeni sana ndugu zangu, nafikiri walijikwaa, wakaogopa tena kujikuna pale tulipojikwaa, lakini naamini wamenielewa na nyinyi mnanielewa huko, hakuna kubwa na tutajitahidi kutetea nchi yetu na tutahitaji kutetea Muungano wetu na Katiba hii ifanikiwe na tuweze kuikamilisha kwa wakati ambao umepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwambieni tena wala msiwe na hofu wala msiwe na wasiwasi kinachoendelea hapa, hao ndugu zetu walilewa, upepo uliwapanda, lakini Mungu atawasaidia na atawaondoshea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Lwanji atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Mheshimiwa Lwanji!

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze kwa msimamo wako wa leo kama ambavyo wamefanya wenzangu. Nimpongeze pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, leo naona kweli nafasi hii anaimudu vizuri sana, kweli ametufundisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpongeze Mheshimiwa Lukuvi na Mwanasheria Mkuu kama nilivyosema kwa kuanika uongo wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye hoja hii. Bila kumsahau mzee wetu Mheshimiwa Mrema, kwa kweli amenifundisha ukomavu wa kisiasa, ni mzee mahiri, naona katika ulingo wa kisiasa bado yumo na tunamwomba aendelee kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyotokea leo asubuhi hapa hatuwezi kuyakwepa, inabidi tuyazungumze kwa sababu yaliyotokea kwa kweli kwa wengine, tuliona kama ni uasi, ni uasi wa dhahiri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukafikiria watu tuliokwenda shule kabisa, tumesoma shule na wengi hapa mpaka Chuo Kikuu, *degree* mbili mbili, wengine sijui mpaka *PhD,* huko wanakataa matokeo dhahiri ya kidemokrasia, imenishangaza sana. Hapa tumepita mchakato wote, toka jana asubuhi hapa jioni wametoka, lakini asubuhi hapa wametaka walichokitaka wamepewa, sauti zile ilikuwa ni dhahiri kabisa zile za siyo za kwetu zile za mwanzo, zilikuwa ni nyingi kuliko zao, lakini hata hivyo ukawapa nafasi wakasema tunataka tuhesabu kura, wamepata kura 59 dhidi ya kura 156, lakini bado wanakataa, sasa ni darasa lipi wanalowapa wananchi ndugu zangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi nyuma, watu tuwe tunasoma historia kwa sababu ukiwa na matukio kama haya au ukaanzisha vitimbi kama hivyo si kwamba utashika dola. Jonas Savimbi alililia dola miaka zaidi ya 20 lakini hakupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakiumbuka kule Angola, Jonas Savimbi na Chama chake cha *UNITA*, *(Union For Total Independence of Angola)* alijaribu sana kuchukua madaraka alishindwa, akajaribu kutumia njia ya kidemokrasia, lakini napo alikataa matokeo, alikataa matokeo dhahiri kabisa. Yeye alikuwa na Sera yake ambaye wananchi wa Angola walikataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani huko tunakoelekea, tunaomba Serikali yetu iwe makini.

Natoa *scenario* tu hiyo ya Angola na nyingine hiyo ya Msumbiji, ya *RENAMO,* sasa hivi vyama ni lazima tuwe makini tunaelekea wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwe makini, tukio hili lililotokea sikulipenda sana kwa sababu maagizo yako ni kama yalikuwa yanacheleweshwa cheleweshwa kutekelezwa, hayakutekelezwa *immediately,* sasa mhimili huu wa Bunge ni lazima uheshimiwe, tuuheshimu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wewe unatoa maagizo hapa, halafu watu badala ya kutekeleza wana-*negotiate* haiwezekani. Tatizo ni nini hapa, nadhani uliangalie, ulichunguze suala hili hata baada ya *reinforcement* ya hawa Mapolisi na watu wa usalama kuja lakini hakukuwa na kitu kilichofanyika haraka sasa ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, inanikumbusha tukio moja, niliwahi kupanda ngazi siku moja nakwenda Ofisi ya Spika, ngazi ile ya kwanza sasa pale kuna, lakini siwezi kumtaja wala simfahamu kwa jina, labda kama nitakuwa nimemponza huyu, naomba radhi, lakini huwa kuna Mapolisi pale, nilikuwa nimeambatana na Mbunge mmoja wa Chama cha Upinzani, ni Mchungaji sasa naona anapigiwa saluti, mimi nilipopita pale sikupigiwa saluti.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwamba nataka saluti, lakini ilinifundisha kitu kimoja nikasema hivi, ni kwa nini, kwa sababu naona kama kuna kaunyenyekevu

kasikokuwa kanaeleweka, huu utiifutiifu huu wanaopewa watu wanaofanya fujo, ndiyo unaniogopesha. Sasa kama hawa watu hawalipwi vizuri, naomba sana ofisini yako iimarishwe, waweze kulipwa vizuri, watekeleze haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kama tukio hili lingetokea au tukio lolote la kutaka kuvunja amani Jaji yuko pale angeamrisha mara moja mtu angekamatwa au Hakimu au mtu wa Serikali, lakini maagizo yako yalicheleweshwa. Sitaki niendelee hapo, ila ilinisikitisha kidogo na ilinikera kwa kweli, hakukuwa na sababu ya muda mrefu hapo kulumbana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI, lakini kabla ya hapo nilikuwa Makamu Mwenyekiti kwenye hii Kamati ambayo imewasilisha Muswada huu, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Pindi Chana, nimefanya naye kazi kwa uadilifu, ni kijana mdogo kwangu, lakini hata siku moja sijawahi kuona chembe ya uwongo kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya aliyozuliwa jana amezungumza uongo, basi nilishangaa kabisa, lakini kitu nilichojifunza katika ile Kamati, kutokana na huyo bwana aliyezusha huu uwongo wote hapa, ni kwamba, kuna watu ambao wana *capricious minds,* ni watu vigeugeu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sikushangaa nilivyoona malumbano ya jana yalivyokuwa

yanafanyika hapa, kwa sababu namwelewa, huyu mwenzangu ni jirani yangu kwa Majimbo, mimi natoka Manyoni Magharibi yeye anatoka Ikungi, ni majirani. Sasa nashindwa kuelewa mwenzangu alikunywa maziwa gani hayo, maana nashindwa kuelewa. Hatuwezi tukazungumza uwongo dhahiri wa kuchafuana wakati inaeleweka kabisa kwamba wananchi wao wamejiandaa kwa ajili ya mabadiliko ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wamekwenda kule, wametembea wameona hali halisi kwamba wananchi wamejiandaa kuleta mabadiliko hayo kwa amani na utulivu. Nadhani kwa hilo wameona kwamba wafanye fujo, kwa kifupi ni kwamba hawataki mabadiliko ya Katiba, huo ndiyo ukweli wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nchi hii inaheshimika, juzi hapa dada yetu Mheshimiwa Mhagama alimtambulisha Balozi wa Marekani *Alfons Leonard*, mtu mwenye heshima zake alikuja hapa kutuaga, ingekuwa ni nchi inayodharulika, ni watu wa fujo fujo, sidhani kama watu wakubwa kama hawa wangeweza kuja hapa katika Bunge lako Tukufu haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *on the right cause* na sisi si vibaraka wa Marekani, lakini wanatuweka kwamba tuko katika Mataifa karibu yote; tuna majeshi Darfur, DRC, tumesaidia nchi nyingi, sasa leo Muswada huu utugawe na utuvuruge na tuingie vitani, hatuwezi kwenda Misri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali chonde chonde huu utaratibu wa kusubiri matukio mpaka hali ya hewa inachafuka na nini, halafu tunabembelezana na nini hapana! Naomba kabisa kuanzia Mikoani, kuanzia hapa, kama wameleta fujo watu hawa wadhibitiwe ili Muswada huu uweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Chomboh, ndugu yangu ni kwamba, watu wa namna hiyo wako ndani ya Bunge hili, ni watu wa hatari. Kweli tusiwaache ndugu zangu wakaleta matatizo, amani ya nchi hii tutaipoteza na watoto wetu watakwenda wapi? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hilo lizingatiwe, mifano imetolewa ya machafu, nchi ya Misri, Libya, tumesikia watu wengi wamechangia hilo na sasa hivi huko wanakopigana hakuna amani, lakini tusingekuwa makini mpaka sasa kama tusingelikuwa makini kulinda demokrasia na mafanikio yetu, nachelea kusema kabisa kwamba *we are not special,* tutaelekea huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii ili Muswada huu upite, katika vifungu vile vilivyokuwa vimeainishwa kuanzia kile kifungu cha 22, 24, 27 mpaka 28 pamoja na Jedwali la Marekebisho la Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Masauni ameweka vizuri sana hapa vipengele vyenyewe ni vichache, tulitarajia Muswada huu jana tu ungeweza

kupitishwa, lakini nashangaa mambo yalivyokuja kuzuka kwa sababu ya uzushi wa mtu mmoja yametufikisha hapa. Naomba sana ndugu zangu tuwe tunapita pita tusome historia za nchi mbalimbali, nchi ya Ujerumani ilianza hivi hivi na yule Adolf Hitler alikuwa mwongo sana, alikuwa mahiri kwa propaganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama tutaacha mambo yaende hivyo, bila kuyakerebisha, hakika hatutaweza kukwepa majanga yanayotokea kwa wenzetu sasa hivi. Njia moja kubwa waliyofanya ni uchochezi wa hapa na pale, kugeuza maneno, kufika kwenye Kamati pale ni sehemu ya kuchukulia *information*, alichukua *information* pale na hakai, nilikuwa kule, hakai yeye ni muda mfupi tu akishabaini *information* za kutosha ameshatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sishangai waliposema wakati wanapitisha Muswada huu yeye alikuwa Mwanza na ni kweli alikuwa Mwanza katika kuvuruga mambo haya haya ya Mabaraza ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sitaki kuzungumza sana, lakini naiomba Serikali iwe makini na hasa katika Muswada huu huku tunakoelekea katika kuhitimisha jambo hili. Nilikotoka huko wananchi wamejipanga vizuri tu, japo tunageuziwa kwamba CCM ndiyo imepanga na hivi, hapana wao wamefika kwangu na helikopta, wamefika pale wamewafundisha watu nini cha kusema. Ni kweli kabisa wamewafundisha kwamba bwana semeni hivi

hasa kwenye kile kipengele cha sita cha kuhusu suala la Muungano, wamepita wanawaambia kabisa bwana ni Serikali tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa katika kile kifungu cha 28 nafikiri ambapo wajumbe tumepewa nafasi za kutosha ya kuchangia kadiri tutakavyoweza, kusema lolote lakini huwezi kushtakiwa Mahakamani wala huwezi kuulizwa na mtu yoyote. Sasa haraka hii ni ya nini, kama wana mambo ya kusema wasubiri, Bunge la Katiba litakuja, waje waeleza mambo yao yote ili tuweze kuhitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lwanji. Kabla Mheshimiwa Lusinde hajaendelea kuchangia, kidogo kwa faida yenu Waheshimiwa Wabunge ambao mnaendelea kuchangia na mnaosikilizwa na wananchi pia, mezani kwangu ninazo nakala za mawasiliano yalikuwa yanaendelea hapo mwanzo kabla ya Muswada huu kufikishwa katika mikono ya Katibu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliiandikia Serikali ya Zanzibar na Waziri wa Katiba na Sheria wa Zanzibar, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakar; akamwandikia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Makamu wa Rais na *communication* ikaja kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naenda kwa kifupi sana. *(Makofi)*

Kwamba Muswada huu, *an Act to Amend the Constitution Review Act* niliupata juzi tarehe 26 Mei, 2013. Baada ya kuupata nilimpelekea nakala *AG* ili aupitie na leo asubuhi tumekutana pamoja kwa kubadilishana mawazo. Maoni yetu kwa pamoja na baada ya kujadiliani ndani ya Serikali ni ifuatavyo:-

Kwa ujumla marekebisho yote si mabaya sana kwa kuathiri haki na fursa kwa Zanzibar. Hakuna kifungu cha mabadiliko ambacho *substantially,* ame-*quote* kimebadilisha maudhui ya kifungu kile cha zamani au Muswada wote kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Hata hivyo, vifungu vitatu tu ndiyo vinapaswa kuangaliwa kwa undani sana, kwani hivi kidogo vinaweza kuleta matatizo, akavitaja vifungu vyenyewe vitatu na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Zanzibar akauleta Muswada, akaiandikia Serikali huku, lakini ninayo *communication* ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali sasa akimwandikia Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa barua namba *AG.CC/C*.10/5 ya tarehe 31 Mei, 2013.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Fredrick Werema, anamwandikia Mheshimiwa Balozi Seif Iddi, anasema hivi:

Mheshimiwa Makamu wa Rais, nakiri kupokea mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (*A bill for an Act to Amend the*

*Constitution Review Act)*. Mapendekezo hayo yatazingatiwa katika ukamilishaji wa Muswada huo. Kwa heshima na unyenyekevu nakushukuru sana. *(Makofi)*

Haikuishia hapo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali akamwandikia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, akamwandikia ifuatavyo:-

Nimeyapitia mapendekezo katika Muswada wa Sheria inayokusudiwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba Zanzibar. Kwa kifupi, pendekezo la kwanza linahusu marekebisho katika ibara ya tatu ya Muswada, kifungu cha 22(1)(c).

Pendekezo hili limezingatiwa na kifungu hicho kimefanyiwa marekebisho ipasavyo. Inategemewa kwamba, Marais watatumia hekima katika kushauriana na kufikia uamuzi kuhusu uamuzi huo pasipo kulazimishwa kisheria kufanya makubaliano. Kwa hiyo, pendekezo la kwanza la Zanzibar limekubaliwa. *(Makofi)*

Pendekezo la pili, linahusu marekebisho katika ibara ya 3 ya Muswada, kifungu kipya cha 22(2)(b) kinachohusu mambo ambayo Rais atayazingatia katika kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum.

Pendekezo hili pia limezingatiwa isipokuwa ni vyema kifungu hiki kikabaki kilivyo kwa maneno usawa jinsia, neno tu usawa wa jinsia *(gender balance)* na ni

kwa sababu usawa wa jinsia haimaanishi lazima iwe 50 kwa 50. Yaani siyo lazima iwe *equality*, inaweza ikawa ni *equity*.

Pendekezo la tatu, linahusu ibara ya (6) ya Muswada kifungu 28(3), kinachohusu muda wa Baraza la Katiba, pendekezo hili pia limezingatiwa kuwa siku 90 zilizopendekezwa na Zanzibar, zijumishwe katika Muswada ili kuepuka suala la kuomba muda kuongezwa. Kwa hiyo, aliyesikiliza vizuri, mapendekezo yote matatu yalizingatiwa.

Cha muhimu zaidi kilichofanya nisimame Waheshimiwa Wabunge, leo tarehe 5 Septemba, ipo barua ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar rasmi iliyoandikwa na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais, akimwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Kayanza Pinda, inayohusu kushirikishwa kwa Zanzibar katika matayarisho ya Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, naisoma ilivyo. Barua hiyo inasema hivi:

"Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, napenda kukuarifu rasmi kwamba, Zanzibar imearifiwa na kushirikishwa kikamilifu katika hatua zote muhimu za mchakato wa maandalizi kuhusu Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba *(A Bill for an Act to Amend the Constitution Review Act)* ikiwa ni pamoja na Muswada kuhusu uteuzi wa Wajumbe wa Bunge la Katiba na Idadi yao.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haina pingamizi juu ya suala hili na tunaomba kusisitiza kwamba majadiliano juu ya Muswada huu yanaweza kuendelea kama yalivyopangwa ili kuwezesha mabadiliko hayo ya kurekebisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yaweze kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Amemalizia kwa kusema kwamba, hili ndilo tamko la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wale wote wenye kumbukumbu sahihi mnafahamu Serikali ya Zanzibar ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Chama cha Mapinduzi na CUF. Kwa hiyo, kwa rafiki zangu ambao labda walikuwa hawana mawasiliano, ni vizuri wajue hivyo.

Mheshimiwa Livingstone Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa John Komba. Mheshimiwa Lusinde!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijasimama hapa kuzungumza, nilikuwa nasali kimoyo moyo ili Mwenyezi Mungu anisaidie kadiri atakavyoweza kupunguza ukali wa maneno yangu, kwa sababu kwa kweli hii nchi ni yetu wote na wako wana CCM kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge wanakerwa na unyonge wetu na ustaarabu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu wanapotukanwa, viongozi wetu wanapodhalilishwa, sisi tunasema tunaenda kwa kufuata kanuni na ustaarabu, kuna wana CCM tunawavunja moyo sana.

Wanaofikiria kwamba jamaa zetu hawa ni hodari sana, ni watu waelewa sana, kumbe hawa jamaa hamna kitu hakuna hata shimo la choo cha shule walichowahi kujenga hawa jamaa, ni maneno tu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamewapongeza sana, lakini nataka niwaambie kwamba, ukitaka kuwa msemaji mzuri lazima ujifunze kusikiliza vizuri. Leo tumepata faida kubwa sana Waheshimiwa Wabunge, toka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali namna alivyoendesha darasa na kama na sisi kidogo tunaanza kupata elimu ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ametumia lugha ya upole sana, sijui Mkurya wa wapi huyu kutumia lugha ya upole sana ya kutufundisha tuelewe tunapojadili maana yake nini, kwa nini wananchi walichagua Wabunge? Maana yake ni kwamba, jengo hili lisingetosha watu wote wa Mtera kuja hapa, ndiyo wakasema aende Lusinde kutuwakilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe wenzetu hawaelewi hilo, wanataka muda wote wananchi wa Hai, wananchi wa Ubungo wote wawe wanakuja au tukitaka kutunga kitu tuwafuate, wakati wananchi walishachagua watu, wakasema hawa ndiyo makini, waende wakatuwakilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na mchango wa Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema. Unajua kwa wenzetu Wapinzani wanaendesha siasa kishabiki kama Simba na Yanga vile, kwamba Kaseja

alikuwa golikipa mzuri wakati akichezea Yanga, alipoenda Simba hafai na wao ndiyo walivyo, Lusinde nilipokuwa CHADEMA nilikuwa nafaa, unajua hata lugha kali ninazozitumia Walimu wangu ni wao wenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niko CCM, siku hizi napata matibabu, naelekea kupona wanasema natukana, Walimu wao. Wakati ule nilikuwa nikiwashambulia CCM, nikiwatukana, wanasukuma mpaka gari langu akina Mnyika, lakini leo nawaonja kidogo tu, tena wala siyo maneno makali kama yale ya zamani waliyonifundisha, kwa sababu napata tiba taratibu, wanalalamika, oooh! Wanatukana, wanatukana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mwanasiasa mzuri akiwa CHADEMA tu, akitoka CHADEMA siyo mzuri. Sijui ni Tanzania gani wanayotaka kutuandalia wenzetu hawa, lakini niseme kwa wazazi, ukiwa na mtoto anakuomba pipi, unamwambia sina hela analia, ndiyo unaenda kumnunulia, ndiyo tabia zake akiwa mtu mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto akiomba pipi ukimwambia sina hela akilia, tandika. Akikulazimisha na wewe ukakubali, ndiyo akiwa kiongozi anakuwa msusaji kama wanavyosusa hawa jamaa. Hizi ni tabia za tangu utoto, hawajazianzia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yanayofanyika ni mambo ya ajabu sana, staili wanayotumia sasa, leo

nataka niwakumbushe wana CCM na wananchi mnaotusikiliza, wamegundua kwamba kasi ya kutekeleza ilani ya uchaguzi ni kubwa, hawa siyo wajinga, wamegundua barabara zinajengwa, wameona safari hii na maji yanapatikana, wameona minara ya simu inapelekwa, wameona namna Kikwete anavyochapa kazi, watasema nini 2015 Katiba, Katiba basi! Hawa watu siyo wajinga tulishawaweka kwenye kona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwakumbushe, walichokifanya leo CHADEMA siyo jambo kubwa sana la kulijadili, ni kama vile Tyson alivyomng'ata Holyfield. Baada ya kuzidiwa na makonde, hawa wametung'ata leo, wameona mkong'oto mkubwa, hawana kitu cha kwenda kuwaambia Watanzania, maana kila ukipita sehemu unakuta kazi za Serikali zinatekelezwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakatumia staili ya *traffic*. Bwana ukimkuta *traffic* mla rushwa; atakagua *brake* zipo, *fire extinguisher*, atawasha taa zipo, mwisho atasema mbona hujachana nywele. Sasa unajiuliza kuchana nywele kuna uhusiano gani na kuendesha gari! Ndicho ambacho wanakitumia hawa. Hizi ni siasa za kitoto, siasa ndogo, wala siyo siasa kubwa. Nani asiyejua siku zote Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Zanzibar kwamba Zanzibar wanapendelewa. Ndicho wanachosema kila siku, tunawalea sana, wanapendelewa sana. Sasa leo tena wanasema Zanzibar wamepunjwa. Hizi siasa za niteme nisiteme, uchimumunye wala uchiteme, ndiyo siasa wanazotumia hawa wenzangu. Sukari usipomumunya

wala usipotema itayeyuka tu mdomoni, hata utakapoachama haitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijielekeze kwenye Kifungu cha 22 cha Sheria, kuhusu Rais kuteua watu 166. Hebu tutumie sasa elimu ya chekechea, maana wengine sekondari labda ada iligomba. Hivi nani kati yetu sisi Wabunge, maana mimi nina *mandate* za kura za watu wa Mtera peke yao na ndivyo ulivyo Engineer Chiza, ndivyo ulivyo Mheshimiwa Naibu Spika, wewe una *mandate* ya kura za Kongwa. Sasa nani atakayetuteulia hawa watu wawe Wabunge kama siyo Rais mwenye *mandate* ya kura za nchi nzima? Jamani mbona mnatia aibu, kitu kiko wazi, tunaye mtu mmoja tu aliyepigiwa kura na vitongoji na nchi nzima, naye ni Jakaya Mrisho Kikwete. Ndiyo maana tukasema wao watapendekeza, watakapopendekeza Rais atateua, maana Rais ndiye anayewakilisha. Sasa leo wanataka kumwondoa Rais kwenye majukumu haya kwa hoja nyepesi kwamba, Rais ni Mwenyekiti wa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka mnisikilize kwa makini, mimi ni miongoni mwa watu wenye tafakuri kubwa, nataka niwaambieni hapa, wengine hamjui siri yangu. Mimi ni mwanasiasa mkubwa na nilianzia huko CHADEMA na nimewafundisha wengine siasa, wengine hawajawahi kunisikia tu, mimi nimekuwa nikifanya siasa, nikiitwa jeshi la mtu mmoja, natangaza Mkutano mimi na nakuja kuhutubia mwaka 1995. Kwa hiyo, kuna watu huwa wananichukulia kwa wapesi tu! Hawa watu

wanataka kutumia siasa nyepesi, kwamba Rais kwa kuwa ni Mwenyekiti wa CCM asipewe fursa ya kuteua.

Nataka niwakumbushe tu, Rais wa China ndiye Katibu Mkuu wa Chama kinachotawala China; lakini mara mbili wagombea wa CHADEMA wamekuwa Viongozi wa Chama cha CHADEMA. Mbowe wakati anagombea Urais alikuwa Mwenyekiti wa CHADEMA, kwake ilikuwa sawa, angetenda haki, kwa sababu yeye ni mteule wa Mungu siyo Kikwete. Dokta Slaa ni Katibu Mkuu wa CHADEMA, kwake ingekuwa sawa, lakini siyo kwa Mkwere Jakaya. Huu ni ubinafsi wa aina gani? Hivi wenzetu hawa wakishika nchi Wana-CCM watawafanyaje hawa? Mpaka wakati mwingine najiuliza hivi Viongozi wa CHADEAMA wakipanda mahindi yanaota na rangi gani kama siyo ya kijani jamani; mbona hawafyeki yale mahindi? Wakimwaga mpunga wenzetu shambani unaota kwa rangi gani? Wanafurahia, wakija humu wanajisikia kichefuchefu ni mambo ya ajabu sana.

Leo tuna Rais wa South Africa, Jacob Zuma, ndiyo Kiongozi wa *ANC,* ajabu ni nini kwa Jakaya mpaka kila siku kuzungumzia jambo hili kama jambo kubwa, mambo ya ajabu sana. Anatutolea takwimu hapa, ukiisoma Rasimu ambayo wao wanaishabikia, Rasimu inataka kupunguzwa kwa Wabunge kutoka idadi iliyopo mpaka Wabunge 75, wakapiga makofi. Leo wanalazimisha Bunge Maalum liwe na Wabunge karibu 700 au 800; akili ya wapi hiyo jamani? Gharama hizo tutazitoa wapi za kuendesha Bunge hilo? Hawaangalii gharama, kuendesha Bunge ni gharama. Leo hawa

Wabunge wanaoongezwa 166 wanasema wachache, ukijumlisha pamoja na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi unapata idadi ya Wabunge 604. Wanasema wachache, chukulia mfano sijui Bangladeshi, Bangladeshi ndiyo nchi maskini kuliko zote Duniani, ukaitolee mfano eti walikaa wakatunga Katiba!

Sasa na mimi nataka niwatolee mfano, maana wenzangu wanajifanya wamesoma sana, wa nchi iliyoendelea kuliko sisi Duniani na ikatutawala lakini haina Katiba ya kuandikwa, Uingereza. Uingereza hawana Katiba. Hivi jamani katika hali tulinayo hata Wazungu wanatucheka kwamba, wenzetu wameshaenda mwezini zaidi ya mara kumi, wameshaimarisha uchumi wao kwa kiwango kikubwa, wameimarisha michezo kwa kiwango kikubwa, sisi tunabishania kuandika Katiba! *(Makofi)*

Hivi kweli hawa ndiyo wanasema wakitawala wao kutakuwa na maendeleo? Maendeleo kipaumbele Katiba; hivi ndugu zangu kweli tutaandika Katiba yenye ubora kuliko *Quran* na Bibilia? Kama hatuwezi kufuata Bibilia na *Quran* tutafuata Katiba wanayotushawishi hawa? Vitu vya ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka niseme hapa kuwa, kwenye Jimbo la Mtera, Katiba siyo kipaumbele; kipaumbele ni maji, kipaumbele ni barabara, kipaumbele ni zahanati, kipaumbele ni mambo ya uchumi. Tusitake kuwadanganya Watanzania kwamba, tukitengeneza Katiba mpya baiskeli zitakuwa

hazipati pancha, mvua itanyesha, haya ni mambo ya uongo kabisa. Mnayatoa wapi haya? Munataka kuwatumainisha Watanzania kwa vitu ambavyo havina maana. Kama huwezi kujiheshimu mwenyewe, kama huwezi kuwa mwadilifu wewe mwenyewe, kama huwezi kuwa mchapa kazi wewe mwenyewe, Katiba itasaidia nini? Tusidanganyane hapa, kila mtu akisimama Taifa muhimu, sijui jambo muhimu; hili siyo jambo muhimu kuliko maji afya na siyo muhimu kuliko Watanzania kupata njaa. Tunataka kukuza mambo tu hapa! *(Kicheko)*

Kuna vitabu vya maana na vikubwa kama Bibilia na *Quran* na hatufuati. Ninataka nikwambie Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mkristu wa kuzaliwa. Kwenye Bibilia hayajaandikwa mambo yote, nina hakika hata kwenye *Quran* hayajaandikwa mambo yote, maana yangeandikwa yote hakuna mtu ambaye angekibeba hicho kitabu. Wenzetu wanatulazimisha kwenye Katiba tuandike kila kitu, tuweke kila mtu, Katiba ya wapi hiyo? *(Makofi)*

Nenda kasome Bibilia na *Quran,* huwezi kukuta mahali Mwenyezi Mungu anaagiza kupitia Vitabu Vitakatifu kwamba, nyumba za ibada ziwekwe feni na *AC*. Wapi imeandikwa? Mbona kwenye misikiti mmeweka? Mbona kwenye makanisa mmeweka? Hawa watu wanatoa wapi vitu vya namna hii? Tumewavumilia tumechoka, nataka niwaambie tutafika mahali hili Taifa tutaliyumbisha, tutalipeleka kubaya sana. Wapo wanaotaka kuwaaminisha watu kwamba wao ni watakatifu sana, wakati siyo kweli.

Tumeona Katibu Mkuu wa Chama fulani akijikopesha shilingi milioni 40 za chama chake za ruzuku. Chama wamegeuza *SACCOS*, uadilifu hakuna, lakini wakisimama hapa wataongea kwa mbwembwe, fisadi, sijui nini na kuzunguka zunguka. Wao wenyewe ndiyo wenye madeni makubwa kwenye Asasi za Serikali, wanafanya biashara. Kwa hiyo, hii Katiba tusitake kuwadanganya Watanzania kwamba, utakuwa mwarobani wa matatizo ya Watanzania; hapana! Sana sana tunaweza tukajikuta tumewaongezea mzigo, ndiyo maana pale mwanzo niliwaambieni na mpaka leo bado nasema, pesa tunazotumia kwa ajili ya kuandika Katiba mpya, zingetosha kuwaletea Watanzania huduma nyingi muhimu. Mheshimiwa Rais, amekubali amesema hiyo hoja ya wenzetu wasije wakasema tumeitupa, wasije wakasema hatuko pamoja nao, acha tuijadili, leo Kikwete mbaya.

Juzi, Mheshimiwa Kikwete, aliwaalika Ikulu Wenyeviti wa Vyama akiwepo Mheshimiwa Mbowe, kwenda kusalimiana na Obama. Mbowe alikuwa wa kwanza kufika. Pale Kikwete hakuwa Mwenyekiti wa CCM maana alikuwepo Obama, kila mtu alikuwa anataka kupiga naye picha, mimi mwenyewe nilikosa bahati tu. Leo kwenye kuteua tena majina ambayo yamepelekwa na wao, Kikwete asishiriki. Hivi tukimwondoa Rais tukubaliane hapa, kwamba Rais asishiriki mchakato kabisa. Mambo yakiharibika tutamwuliza nani? Tutamwuliza nani na mtu

anayehusika na nchi hii raia namba moja ni Rais wa nchi hii?

Leo tumeshuhudia Mbunge anampiga ngumi askari; vitu vya aibu kabisa! Vitu vya aibu vimefanyika nje pale, Mbunge kapiga ngumi polisi, halafu ikija kutokea Polisi amemvunja mguu Mbunge, mtaanza ng'we ng'we, oooh Wabunge wamepigwa, hapana!

Polisi chukueni hatua, nataka niwaambie Dunia nzima mnayoina, iliharibiwa na wabishi. Wabishi ndiyo waliharibu Dunia, kabla ya wao kuwepo hapa Duniani, Dunia ilikuwa safi. Mtu anafuatwa bwana umekosea twende kituoni, siendi! Wale ndiyo waliosababisha Polisi wakawa na virungu. Akigongwa viwili naenda, kwa sababu ya ubishi. Hata ujenzi wa barabara ukiona kuna tuta, siyo ujenzi wa barabara bora ni kwa sababu ya madereva wabishi, anaambiwa nenda kilomita sitini yeye anazidisha mia mbili, wanasema weka tuta kwa sababu nalo ni bishi atapunguza.

Kwa hiyo, wabishi ndiyo wamevuruga Dunia mnayoina leo, kila wakigeuka wanaona umeme unawashwa, kila wakigeuka wanaona bei za umeme zinashushwa, kila wakigeuka wanaona CCM tunatekeleza wanajiuliza 2015 watasema nini? Watasema nini?

Kwa hiyo, sasa wanageuza ionekane kwamba, hoja ya msingi kuliko vyote katika nchi ya Tanzania ni Katiba. Kitu ambacho siyo kweli kabisa, zipo hoja za msingi nyingi. Tusitumie muda wa Watanzania bure na

isije ikaonekana kuna kikundi fulani cha watu wanaojiona bora, maana hata ukifuatilia kilichotokea leo ni aibu. Wamepanga tangu jana, twende pale tukakatae, tufanye fujo na sasa hivi tusitoke nje, tugomee mle mle ndani ili waahirishe Bunge. Yaani hawa watu ndani ya wiki mbili zilizopita taarifa zao zilikuwa zinaandikwa ukurasa wa nne, wa tano, wa sita, leo wakataka kulazimisha ziende *front page* kwa staili hii. Mambo ya ajabu sana yamefanyika hapa.

Nataka niwaambie hata ukiutazama urafiki wenyewe ni urafiki wa mashaka, ni kama ndoa ya mkeka. Maana yake *CUF* wametumia dakika moja na nusu tu kuwashawishi CHADEMA kutoka. Kambi Rasmi ya Upinzani hata wewe huwezi kuielewa ni ipi. Hawa wangeongoza Serikali ipo siku wangesusa, wakati wao ndiyo wanaoongoza Serikali, maana hata huwezi kuelewa wanataka nini! Leo nataka nitumie fursa hii kuwafundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili mabadiliko ya Katiba lakini tuwape hata historia fupi za wanasiasa wengine mtujue. Huwezi kushinda kama una hoja lukuki kama walizonazo hawa. Mandela pale South Africa alishinda kwa sababu alikuwa na hoja moja tu ya Ubaguzi, basi. Alizungumzia ubaguzi maisha yake yote, mpaka watu wakamwelewa, lakini angechanganya maji, ubaguzi, lami, angeshindwa asingepata Urais kama wanavyoshindwa hawa. Hawa wana hoja nyingi, uanasiasa wao ninauita ni wa hali ya hewa; leo meli ikizama hoja ni meli, meli imezama tuahirishe

Bunge tujadili meli. Wanataka kuwaaminisha Watanzania wakitawala wao hata ajali hazitakuwepo.

Watu wa ajabu sana hawa, wakisikia ya meli yamepita, basi limeanguka, wanageuka, barabara wanajenga vibaya mabasi yanaanguka. Ninataka niwapongeze sana Serikali, Mawaziri mmejitahidi kuwabana wabadhirifu kwenye Wizara zao. Sasa hivi mabomu hamna, maana hawa walitegemea kuishi kwa mabomu, wanaenda kilimo pale kuna mabomu gani ya mbolea, wakienda elimu kuna mabomu gani, wakienda maji kuna mabomu gani, hamna, ndiyo maana unaona wanaokoteza sasa; hoja za kuokoteza, Katiba, Katiba, hakuna tena mabomu yale. *(Makofi)*

Ilikuwa ikipita siku mbili utawasikia nimeshapata bomu nakuja kulipua bomu, siasa za *unywanywa unywanywa* hivi, za *udandala dandala* ndiyo wanataka kupatia nchi hao! Sasa leo nataka niseme kwamba, watafute hoja za msingi na wafanye kwa vitendo. Ukifika mahali useme hii shule mbovu uoneshe ya kwako nzuri. Sasa wewe kazi yako ni kusema tu mbovu halafu mwishoni kikao kimefungwa, ndiyo imekuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo tulipitishe, tuwaundie hiyo Katiba mpya wanayoitaka. Wasifikiri kwamba, Wabunge wote wa CCM tunaunga mkono Katiba mpya, lakini unakubaliana na wenzako. Mimi ni miongoni mwa watu ambao hawaoni umuhimu wa jambo hili na nawaambia wazi hapa na hata Jimboni kwangu sidhani kama utampata mpiga kura wa Mtera,

jamani robo tatu ya Watanzania wanalala chini hata magodoro wengine hawana. Leo mnazungumzia kuongeza idadi ya Wabunge, mnazungumzia kuongeza idadi ya matumizi ya Katiba; hivi hatuwaonei huruma wapiga kura?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka kwenye familia maskini, ni miongozi mwa Wabunge wachache sana humu ndani, waliotoka kwenye umaskini uliotopea. Kuna watu wanakula mlo mmoja na kuna wengine hawaupati, tuwazungumzie hao, tunazungumzia Katiba. Tunatumia zaidi ya trilioni kadhaa kwa ajili kujadili vitu vya kitoto kabisa. Hebu tuzungumzie vitu vya msingi na tukitaka kumaliza wanatupa muda ili waendelee kula posho tujadili mambo ya Katiba. Ni lini tutawashughulikia Watanzania maskini? Lini tutawakumbuka akina mama wanaokufa kwa kukosa Zahanati? Lini tutawakumbuka watu wanaougua magonjwa ya *typhoid* kwa kukosa maji? Tumeng'ang'ania Katiba; hivi kweli tukienda kwenye kila Jimbo, tukatafuta watu ambao hawataki maji, hawataki barabara, wanataka Katiba tutawapata? Jimbo la nani hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu ninaowaongoza mimi wana shida wanataka zishughulikiwe. Hili jambo ni *by the way* kwa sababu wenzetu wanataka na Rais kasema tuwasikilize na ndiyo maana tunageuka kuwaunga mkono. Sasa leo tena wanatuchelewesha, tukitaka kusogea mbele wanatafuta sababu, hivi umewahi kufanya safari na mtu ambaye hataki kwenda, atakusumbua. Ukifanya safari na mtu

ambaye hataki hiyo safari atakusumbua, kila ukimwambia ongeza mwendo yeye atapunguza na hata kwenye ndoa, ikitokea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, ahsante sana. Hapo kwenye ndoa ndiyo palikuwa penyewe hapo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, umeniweka pabaya, maana nilikuwa nianze mimi ndiyo afike Lusinde, sasa Lusinde kamaliza kila kitu. Kwanza, nampongeza sana dada yangu Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati, kwa kazi kubwa na nzuri na ya mfano aliyoifanya. Kwa faida tu ya Bunge hili, niseme kuwa, zile akili nimempa mimi kwa sababu mimi ni mwalimu wake. Humu ndani nimezalisha Wabunge wengi; Mheshimiwa Pindi Chana nimemfundisha, Mheshimiwa Mahamudu Mgimwa mwanafunzi wangu, Mheshimiwa Lusinde mwanafunzi wangu na Mheshimiwa Ritta Kabati mwanafunzi wangu. Nimewafundisha wengi humu ndani, kwa hiyo, hiyo akili ni yangu, endelea mama, safi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nakupongeza sana, kwanza, nikusalimie *Asalaam Aleykum*?

**WABUNGE FULANI:** *Waaleykum salaam!*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Umefanya kazi nzuri, umeuonesha umma kwamba, unaweza kulidhibiti Bunge, huna uwoga, ni mstarabu, ni mkweli na mtekelezaji wa ilani zako. Ahsante sana. *(Makofi)*

Ombi langu kwako, naomba barua uliyoisoma maana hii ndiyo ajenda kubwa iliyofanya watoke humu, ipelekwe kwenye vyombo vya habari, isomwe na watu, itangazwe kwenye TV na Redio kusudi Wananchi wasidanganywe na hawa. Barua hii imeandikwa vizuri na umetusomea sisi na tunaomba umma wasomewe kupitia vyombo vya habari. Pia, utupe sisi Wabunge tupeleke Majimboni kwetu, ili tukawasomee Wananchi wetu waliotupa kura. *(Makofi)*

Tatu, nataka nivipongeze vyombo vya habari, safari hii vimejua ukweli ni upi na uhuni ni upi. Ukiangalia vyombo vyote kuanzia Magazeti, Redio, TV na hata *BBC* nimesikiliza, hata *Deutsche Welle* nimesikiliza, hawajawapa kipaumbele haya waliyoyafanya kwa sababu wameona ni upuuzi mtupu. *(Makofi)*

Waandishi wa habari, nchi hii tunaijenga sote, sisi na ninyi, wakiharibu hawa, tukiharibikiwa tunaharibikiwa sote. Kwa hiyo, ukweli mliounesha leo endeleeni kuwafundisha Watanzania namna ya kukaa ndani ya Bunge na kutoa mawazo ndani ya Bunge.

Siku moja Mheshimiwa Khatibu wa *CUF,* ashakum si matusi, alisema hapa, nimesema ashakum si matusi; Bwana Mbowe alikuja hapa kajamba jamba akaondoka, amekuja Bwana Tundu Lissu kajamba jamba kaondoka. Sasa leo Mbowe sijui kafanya nani kamwondoa na yeye! (*Kicheko*)

Sasa sijui kafanyaje huko? Kinachowanya *CUF* watoke hapa sikielewi kabisa. Hii ndoa iliyofungwa leo siielewi kabisa. Ndoa gani hii? Juzi juzi waliambiwa tu hapa *ooh* ninyi ni Waliberali, ikawa tafrani humu ndani. Leo *oooh* tayari wameshafunga ndoa! *CUF* rudini humu ndani msifuate mambo ya kuiga, hao wana yao.

Wanazungumza habari kwamba, Sauti ya Umma, Nguvu ya Umma, *Peoples Power*, lakini sisi tulioko humu ndiyo Umma wenyewe na Umma huu umegawanyika sehemu mbili; Umma wa Upinzani na Umma wa Chama Tawala. Hivi Umma ulio mwingi humu ndani ni upi?

**WABUNGE FULANI:** Chama Tawala.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Sasa wanachukuaje nafasi yetu sisi wakasema eti tunausemea Umma? Tunaotakiwa kuusemea Umma ni sisi tuliopewa ridhaa ya kutawala. *(Makofi)*

Leo wanatunyang'anya nafasi yetu wanachukua wao, siyo haki. Sasa nawaomba Watanzania walielewe hili. Umma ambao Chama kinao ni Chama cha Mapinduzi, ndicho kinachotawala asilimia 78 na

Rais wetu asilimia 62. Zaidi ya hapo, Umma huo Umma gani? Tunaotakiwa kusema umma ni sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Vilevile nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amefanya kazi nzuri sana na labda niseme wanaotafuta nafasi yako, nafikiri nafasi hiyo imeshajaaa. Nafasi hii ya Uanasheria Mkuu imeshajaa, haipo. Pia nafasi ya Mheshimiwa Lukuvi nayo imejaa, haipo tena. *(Makofi)*

Mnafanya kazi nzuri ya kuuelimisha Umma, fanyeni hivyo kila siku, lakini nataka niwaambieni, Naibu Spika nilishamwambia, si nilimwambia *asalaam aleykum*? Naibu Spika, uendelee kubaki hapo na uendelee kutuongoza na pengine sijui uendelee kupanda, *I don't know,* lakini nakuomba endelea kulidhibiti Bunge kama ambavyo umeendelea sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sina maneno mengi, lakini naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Capt. John Komba. Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida. Mheshimiwa Stella Manyanya!

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pili, nachukua nafasi hii kuipongeza Tume, kwa kazi

ambayo wamekwisha kuianza na ninaamini itaendelea vizuri mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa pole kwa sekeseke la mchana na nakupa hongera kwa ujasiri mkubwa ulivyoendesha kikao chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubali na sisi kama Watanzania, lakini Chama Tawala ndiyo tuna dhamana kubwa kwa Watanzania ya kuhakikisha kuwa, nchi hii inaendelea kubaki kuwa kisima cha amani, kuishi katika umoja na utengamano. Kwa kweli tusitenganishwe na hali yoyote ile ambayo inaashiria uchu au kiu au tamaa zetu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kujiuliza kwa mambo ambayo yanapitishwa leo, kwa sisi ambao ni wawakilishi na tumeagizwa kufanya kazi hii, tena kwa kiwango, kwa utaratibu maalum na ndiyo maana hata tukajitungia Kanuni zetu. Leo sisi tunaposhindwa kuonesha mfano wa kutii mamlaka tulizojiwekea sisi wenyewe; kwa mfano, kutii Kiti cha Mheshimiwa Spika, tena anayeanza kutokutii ni Kiongozi mkubwa, nadhani hatutoi taswira nzuri kwa Watanzania wenzetu hasa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini dhamira ya kuleta marekebisho haya ni njema na inalenga kuona nchi yetu inaendelea kuwa na mshikamano katika kufikia malengo tuliyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili la umuhimu wa Rais kuteua. Hatumaanishi kwamba Rais ateue, kwamba, hakuna watu watakaoweza kusaidia na kumpa taarifa mbalimbali juu ya wale wanaoteuliwa na hayo ndiyo yanayofanyika kila siku. Sasa mtu anaposema asiteue, akashindwa kuwa na imani na chombo kikubwa kama hicho, Rais, halafu akasema tufanye kama anavyotaka yeye kwa mfano ambao tunauona kabisa. Kwa mfano, kwenye uteuzi wa mwanzo, mimi naona busara kubwa ilitumika, kwa sababu yawezekana Tume kama ingetokea kwamba wakati wa uteuzi angeteuliwa Mheshimiwa Tundu Lissu, yawezekana hata leo hiyo Rasimu ingekuwa haijatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa busara hizo hizo, kwa kutuangalia namna tunavyotenda kazi zetu humu Bungeni, jinsi tunavyojiheshimu na kujithamini, watu wanakupima bila wewe mwenyewe kuona, wanasema kuna *invisible eyes and hands. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Rais ni dhamana na ndiyo maana watu tunatumia fedha nyingi na muda mwingi kumteua Kiongozi kama huyu, ni Alama ya Taifa. Sasa mtu anaposema hana imani na Rais ambaye ameteuliwa na watu wengi, kwa vyovyote vile huyo siyo mwanademokrasia wa kweli na kwa misingi hiyo basi, wenye kufahamu maana wataisimamia maana na wasiofahamu maana watatoka nje na sisi tutaendelea na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *actually,* mimi hata ile mchana ulipoongeza nusu saa, nilifikiria kwamba kwa jinsi ambavyo tunatumia fedha ya walipa kodi, pengine tungeendelea na mjadala mpaka jioni hata tusile, lakini tuhakikishe Muswada huu unapita, lakini basi hata ile nusu saa ilitosha.

Nimeletewa taarifa na simu mbalimbali kutoka kwa Wananchi, wanakupongeza na wanashukuru kwa jinsi ambavyo Wabunge wa CCM walikuwa makini kwa utulivu katika kuona kwamba, wanajiepusha na migogoro isiyo ya lazima. Ona sasa hivi tumepata hasara, kile kipaza sauti pale kimeshavunjwa na Mbunge mkubwa kabisa anayeheshimika. Mheshimiwa Sugu, amevunja kipaza sauti. Mambo ambayo wanafanya watoto anayafanya yeye kwenye Bunge; kweli hii ni sahihi? Siyo sahihi hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niende kwenye idadi ya Wabunge ambao watakuwa kwenye Bunge Maalum. Mimi naamini kuwa, idadi iliyopendekezwa ni kubwa, ukubwa wa pua siyo wingi wa kamasi. Kwa hiyo, haina haja ya kusema lazima tuwe na watu wengi, halafu tukakaa humo tukashindwa hata kuchangia, kwa sababu tutakuwa wengi na mwingine atatoka hajachangia hata kitu kimoja, hiyo itakuwa siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, najaribu kuangalia, mara nyingi tumekuwa tukichangia humu Bungeni tunasema kwamba, Mikoa inaanzishwa kienyeji, Wabunge tunaongezeka idadi yetu inakuwa

kubwa, ni gharama, lakini leo tunasema aah huko tuwe wengi!

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi linakuja; katika sura hii *suppose* tunaamua tuongeze idadi zaidi ya 166, ambao wamependekezwa hapa; je, ina maana tutakuwa tumewachukua Watanzania wote na wameingia kwenye Bunge Maalum? Ina maana kwamba, tuna uhakika wale watakaokuwa wamewakilisha, watawakilisha matakwa ya kila mtu? Siyo kweli hata kidogo na ndiyo maana hata sisi tunakuja hapa tunachangia vingine hata visivyowafurahisha waliotutuma, lakini ndiyo tuliotumwa kwa ajili ya kuwawakilisha. Kwa hiyo, mimi nadhani idadi hiyo inatosha ili kupata michango yenye afya na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni... aaah macho hayaoni vizuri sijui wameniroga hawa, lakini Sumbawanga watanilinda! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na sifa za ambao wanahitaji kugombea ili kuweza kuchaguliwa kuwa Wenyeviti na Makamu. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na sifa maalum na si kila mtu anaweza kuwa na cheo kikubwa kama hicho kinachochukua masilahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona pia nizungumzie suala ambalo limekuwa likijitokeza, *no,* kabla ya hilo, nimeona katika ibara ya pili, kumeongezewa kifungu kinachozungumzia kuingiza ushiriki wa Shirikisho la

Wafanyakazi. Hilo ni jambo jema sana, Wafanyakazi wanatengeneza sehemu kubwa ya rasilimali watu, inayolipa kodi na inayochangia mchango mkubwa wa maendeleao katika nchi yetu. Kwa hiyo, watu hawa kuingizwa katika nafasi hii ya uwakilishi ni muhimu sana. Hiyo naipongeza sana katika marekebisho yanayoletwa. *(Makofi)*

La mwisho, naomba nisisitize juu ya suala la kusema kwamba, kuna watu nimeona hata kabla hatujaanza hili Bunge, wanasema *suppose* Katiba hiyo tunayoihitaji haijapita hali itakuwaje? Labda pengine tuongezewe miaka mitatu hivi, tuendelee na Bunge hili, halafu uchaguzi tufanye mwaka 2017 au 2018; hapana, huo ni ulafi na uroho wa madaraka, haiwezekani. Tukishaanza hizi tabia za kutaka kujiongezea ongezea muda, hatutendi haki na siyo demokrasia ya kweli. *(Makofi)*

Muhimu sana Kifungu hiki hata kama kitaenda kwenye Muswada unaotegemewa kuletwa wa upigaji wa kura za maoni, nashauri haya maneno yangu yachukuliwe kama sehemu ya kusimamia kifungu hiki. Kwamba, kama Katiba itakuwa haijapita, hiyo tunayoitarajia, basi Katiba iliyopo itaendelea kuishi kwa muda wote na uchaguzi wa mwaka 2015 ufanyike kama kawaida. Hata 2014, kama tutavutana kienyeji enyeji, tunajua Katiba ipo tunaendelea na uchaguzi. Zaidi ya hapo ni kutaka kutafuta mbinu za kuwalazimisha Wananchi waweze kufanya maamuzi yasiyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili swali langu ni hili; kwa nini sisi Wabunge tunapenda kujichukulia sisi ndiyo tuna uelewa mkubwa sana kuliko Wananchi, yaani hatutaki hata kuwasikiliza wao? Mimi nimeona katika kampeni zilizoendeshwa hivi karibuni na ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Watu wamekwenda wamefanya mkutano kama kawaida, hata kule kwetu Mkoani Rukwa walikuja na mkutano ule walihudhuria watu wengi tu, Wana-CCM, *TLP*, CHADEMA wenyewe na watu wengine. Pale hakukuwa na utoaji wa maoni maalum, ilikuwa ni suala tu la kuhutubia na kueleza kwamba, jamani twende hivi, fanyeni hivi, yaani tunawalazimisha Wananchi kuchukua yale tunayoyataka sisi. Wakati tulisema wazi kwamba, katika utengenezaji wa Katiba hii, Wananchi wawe huru kueleza yale wanayoyaamini, lakini sisi tunaamua kufanya *interference*. Afadhali wangekuwa wamejifungia kwenye ukumbi wanaongea na wanachama wao, tusingewaingilia, lakini waliongea kwenye mkutano wa wazi na watu mbalimbali, tena hata siyo taasisi inayohusika. *(Makofi)*

Sasa swali langu labda kwa wale ambao wanasimamia misingi ya Sheria zilizopo; katika kuangalia Sheria yetu tuliyoitunga tulisema kwamba, mtu yeyote atakayefanya shughuli za kukusanya na kuratibu maoni ya Wananchi kinyume na Sheria hii, kuna adhabu zimetolewa hapa, ikiwa ni faini pamoja na kufungwa. Ninadhani kwa kukazia Sheria hii, isitoshe tu kukataa hayo maoni, bali pia wachukuliwe hatua. Hatua ichukuliwe wafikishwe Mahakamani na ikibidi

wafungwe au walipe faini. Hatuwezi kuendelea kuendekeza tabia hizi za kuleta vurugu na uchochezi zisizo na maana katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Jambo kubwa ambalo napenda kuwapongeza Wananchi wa Tanzania, sasa wametuelewa, wanafahamu mbivu na mbichi, wanafahamu ukweli ni upi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie kuwa, Wananchi wako *very serious* kuona wanatengeneza Katiba ambayo itakidhi mahitaji yao. Tena wanachangia michango ambayo hata wewe ambaye unakaa humu Bungeni ukiisikia huwezi kuamini, utasema hata mimi sitoshi kuliko huyu Mwananchi alivyochangia. Mfano mdogo tu, wakasema kwamba, hivi tunaposema tuwe na mgombea binafsi, sawa, lakini atadhibitiwa na nani? Huyu aliyeko kwenye Chama atadhibitiwa na Chama chake, huyu mgombea binafsi atadhibitiwa na nani? Kwa hiyo, unakuta wanatoa mijadala kama hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naamni kuna Wananchi ambao wana upeo na uelewa mkubwa, wao hawajapata nafasi ya kukaa humu Bungeni, lakini kama tutachukua nafasi zetu kuwasikiliza na kupata michango yao, tutaweza kutengeneza kitu ambacho kina tija kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Sisi tupo kwa ajili ya Watanzania na tutaendelea kutimiza wajibu wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na ambaye ametujalia kutuweka hapa, tukiwa Viongozi tulioteuliwa na Wananchi kuwaongoza huko waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna methali inasema: "Ada ya mja hunena, muungwana ni vitendo". Vitendo vya binadamu vinaonekana kwa tabia yake na mambo yake anayoyafanya, utamwona kabisa huyu ni mtu wa aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe shukrani zangu na pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uvumilivu, hekima na busara alizozionesha na kuhakikisha kwamba, Katiba hii inaletwa hapa na wenzetu Kambi ya Upinzani walituambia tunaitaka Katiba mara moja. Akatumia busara zake, akatumia hekima zake na akatumia utulivu aliokuwa nao, kutaka kuongoza hii Katiba iende kwa usalama na amani. *(Makofi)*

Wao walifikiria kuwa hii Katiba Mheshimiwa Rais ataikataa ili walete vurugu zingine. Mheshimiwa Rais, alikaa na Viongozi, Wazee, Vijana, wakampa ushauri uliotukuka, akaileta Katiba mezani kwetu. Imeletwa Katiba tu, wakaleta vijana kutoka *UDOM* kutia fujo hapa, kwa neno kuwa nchi hii itakuwa haitawaliki.

Wewe unayesema nchi haitawaliki, tukikupa hii nchi utafanya nini; ina maana utamwaga damu nchi hii itakuwa kama Somaria? Nchi hii itakuwa Misri, halafu Wananchi wetu wataishi wapi, wanawake na watoto ambao tunaitegemea amani hii ili waweze kuilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Pemba kulitokea vurugu, wanaume wote walikimbia wakawaacha wanawake na watoto majumbani wanahangaika na ushahidi huu tunao. Wanaume unaowaona hawa, wakifanya vurugu wanakimbia. Wanawake wanakumbatia watoto, kuwatunza na kuhakikisha amani na usalama wa watoto wao na vikongwe unakuwa chini yao. Sisi hii hali hatuitaki na wala tusiikubali tuikemee. Wanawake wote Tanzania tuikemee hii hali ya vurugu, siyo hali njema itatuletea athari. Watu wanaangalia masilahi binafsi, hawaangalii Tanzania tunaipeleka wapi na ndiyo maana kwa siku ya leo umeonesha ujasiri mkubwa sana, lazima nikupongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasifiwa Tanzania kwa amani na ndiyo maana leo watu wamekaa sokoni wanafanya shughuli zao, wana maduka wanafanya shughuli zao, watalii wanakuja wanafanya shughuli zao, lakini wao kwa makusudi, wakailenga Arusha. Arusha hapatawaliki, lakini ni makusudi ya kuhakikisha nchi ionekane haitawaliki. Wana ajenda zao za kuhakikisha pale Arusha hapatawaliki; mbona jirani yao pale panatawalika na ndiyo wanakotoka pale

hawafanyi fujo? Hizi ni ajenda za makusudi za kudhoofisha nchi yetu isiweze kuendelea. *(Makofi)*

Mimi kwa kweli siku ya leo nimejisikia huzuni sana, unapokuwa Kiongozi unatakiwa uoneshe uadilifu, lakini kama Kiongozi jicho lako halina uadilifu, ninapata mashaka; hivi Tanzania hii tuikabidhi katika mazingira gani? Lazima tuwe na msimamo wa pamoja kwa Watanzania wote kwa pamoja, tuisimamie Katiba iende kama ilivyo katika maadili yaliyo mazuri na yaliyoboreshwa ili angalau amani tuiendeleze na hata huyo anayekuja amani yetu iweze kwenda tena.

Watu wanapanga mipango ya kusema tukae hapa Bungeni mpaka 2017 au 2018 kwa masilahi binafsi. Je, Wananchi wetu walioko kule watakuwa wanafanya nini; watakuwa wanahangaika. Mimi nikupongeze na Kiti chako kitumie kwa ukamilifu na kwa uadilifu ili twende vizuri na Katiba hii ipitishwe, Rasmu hizi zipitishwe, Wananchi waone kuwa sisi tumekaa hapa kusimamia amani na kuhakikisha utulivu wetu utatufikisha katika usalama zaidi kuliko kitu kingine chochote.

Ninasimama hapa zaidi ya kumwomba Mwenyezi Mungu, ailete amani ndani ya nchi hii, atuongoze katika uadilifu, utulivu na tuwe na hekima katika maamuzi yetu na tusipindishe Sheria zetu ili ziende katika msimamo, Wananchi watuamini kuwa tuko hapa kuwatendea haki na wanawake na watoto wapate utulivu ndani ya majumba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa vile ninaiombea amani zaidi na nikimtakia heri Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, awe na amani zaidi, alete hekima zake na Mwenyezi Mungu atamjalia. Nitatoa mfano mmoja ndani *Quran. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mtu ambaye hakuwa na imani ya Uislam, ikawa kila siku anakwenda katika mlango wa Nabii Muhammad anajisaidia pale. Yule bwana kwa uaminifu wake, kwa utulivu wake na hekima yake, ikawa anakwenda kutoa kile kinyesi anakitupa. Hamtukani yule mtu na wala hamfanyii jeuri yoyote. Alifanya hivyo yule mtu karibu ya miezi sita, kila siku anakwenda kujisaidia anafanya, Nabii Muhammad alikuwa anatoa kile kinyesi, anakwenda kukitupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitokea siku moja yule bwana hakwenda kujisaidia. Nabii Muhammad akawauliza wafuasi, akasema mbona leo nyumbani kwangu sijaona kinyesi kulikoni na alikuwa anamfahamu vizuri sana yule mtu aliyekuwa anakwenda kumwaga kinyesi pale; akaambiwa yule mtu anaumwa. Alichofanya aliondoka mpaka nyumbani kwake kwenda kumtaka hali; *asalaam aleykum bwana*. Akajibu *alaykum salaam*. Nabii Muhammad akasema nimeona tatizo, toka juzi, jana, wala leo, sijaona kinyesi katika mlango wangu kulikoni? Akasema mimi nimepata mashaka kama wewe unaugua. Yule bwana kwa aibu aliyoiona, kwa matendo yake aliyoyafanya ya kifedhuli, alijirudi

mwenye. Nasi kufuate mifano bora, tuwe wavumilivu kwa wenzetu wanaotaka kufanya maovu, tusiyarudie maovu yao, tuendelee na msimamo wetu ambao ni bora ili tuiweke hii nchi iwe katika amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili na mimi nichangie katika Muswada muhimu sana wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Kama kawaida yangu, kwa sababu sina matatizo na marekebisho yaliyoletwa na Serikali, ninaomba kusema ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa maelezo ya kina sana asubuhi ya leo. Kila Mtanzania aliyekuwa anamsikiliza, kufuatia upotoshwaji uliotokea leo na jana, Watanzania watakuwa wamemwelewa vizuri sana. Naomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa William Lukuvi, kwa maelezo ya kina kuhusu majina ya Wajumbe, mmoja mmoja kwa idadi iliyopelekwa Wajumbe watatu, Mheshimiwa Rais akachagua Mjumbe mmoja kama walivyopendekeza wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kama inawezekana kwa idhini ya Serikali, maana mtu baki huwezi kuchukua *document* ya Serikali ukawa

unatembea nayo, lakini kwa idhini ya Serikali kama inawezekana ili kuondoa hili wingu ambalo limetandazwa huko nje huko; majina hayo na maeneo wanayotoka, yaandikwe kwenye vyombo vya habari. Nia hapo Watanzania wajue. Tukifanya hivyo, ninafikiri Watanzania watakuwa wametuelewa nani mkweli na nani mwongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia uniruhusu nikupongeze wewe kwa dhati kabisa, leo umesimama kidete. Kama ilivyo ada, ninaomba uniruhusu nisome Kanuni za Kudumu za Bunge, Ibara ya 31, inayohusu Dua. Siyo sehemu yote lakini sehemu ndogo tu inasomeka hivi: *"Ewe MWENYEZI MUNGU Mtukufu, Muumba Mbingu na Dunia, utuongezee hekima na busara sisi Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utupe uwezo wa kujadili kwa dhati, mambo yaliyoletwa mbele yetu leo, ili tufanye maamuzi sahihi na yenye manufaa kwa watu wote na ustawi wa nchi yetu. Tukamalizia na Amina." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, leo Mungu amekupa hekima vizuri sana na ndiyo maana kikao hiki umekiongoza vizuri, bila jazba, kwa manufaa ya Watanzania. Nilitegemea kutokana na Dua hiyo, wenzetu nao kwa sababu waliitikia *Amina,* jambo lililokuwa Mezani kwetu tungelijadili kwa dhati, ili tupate maamuzi sahihi na yenye manufaa kwa Watanzania. Sina uhakika wenzetu hawa hii ndiyo busara, hii ndiyo hekima ya kutokujadili kitu kilicholetwa mbele yetu leo halafu wanatoka nje! Mimi ninawasihi sana, halafu

bahati nzuri wengine tunaheshimiana sana na hata huko nje wengine wanaheshimika sana, lakini kwa vitendo hivi kwa kweli havina siha kwa Taifa na kwa Watanzania. *(Makofi)*

Naomba tuwe na uvumilivu, tuvumiliane na tuondoe jazba. Tukifanya hivyo tutaacha *legacy* kwa nchi yetu. Marekebisho ya Katiba tunayoyafanya, yatatupelekea kutengeneza Katiba nzuri, kwa miaka 50 ijayo. Kama hatutakuwa pamoja, kila mtu akafanya ya kwake, sisi humu ndani tungelikuwa pamoja kwenye hili, tukajadili, tukakubaliana, tukatoka pamoja; tukianza kugombana sisi humu ndani, kinachofuatia ni Wananchi kutotuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema asubuhi; hakilali kitu hapa, *Aluta Continua,* hii lazima ipite na kama ni kesho sisi tutapitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kukubali kwa sababu wao wana ajenda zao, wacheleweshe cheleweshe tu, kama alivyosema Mgogo pale, Bwana Mdogo Lusinde. Kwamba, labda wameshaona sasa hali ya hewa huko imeshawachafukia, lakini Wananchi wa Sumve, leo hii ukimwuliza mtu mmoja mmoja, kwa ujumla wao, kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde, kwa kweli wanahitaji sana huduma za jamii. Wanahitaji, maji, umeme, barabara na shule. Ukiwapelekea suala la Serikali tatu, watakuuliza Serikali tatu ndiyo nini, kwani hii Serikali iliyopo imekosa nini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana wenzetu, hata yale maneno yao na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa uvumilivu wa maneno yao wanayoyatumia. Ingelikuwa ni nchi nyingine, unaposimama mahali unatamka wazi unataka nchi hii isitawalike, nafikiri huu ni uhaini. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, ni kama jalala anameza yote, yawe mazuri, yawe mabaya, anavumilia na ni mvumilivu hana jazba. Angelikuwa ana jazba kwenye kusema tu hili neno, unapotamka nataka nchi hii isitawalike, inatafsiri pana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaelekea kwa vurugu hizi, labda wanataka sasa yatimie yale ambayo wanayataka kwamba, nchi isitawalike. Wanaanzia wapi? Wanaanzisha vurugu humu Bungeni. Leo asubuhi yalipotokea haya, nilikuwa nimesimama hapa, nikawa ninajiuliza hivi hili ni Bunge la Kenya, la India, hivi ninaota au ni kweli! Ikabidi nihame hapa nikahamia pale karibu na Mheshimiwa Jenista Mhagama; nikamwuliza hivi yanayotokea ni kweli; hili ni Bunge la kwetu? Akanijibu ni Bunge la kwetu. Kwa ukosefu wa adabu na tunajua lazima tuheshimu Kiti, Kiti kinanyooshewa kidole na Mbunge, unasema leo hutoki humu. Leo hutoki humu, tumefika hapo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kile kitendo cha kung'oa ile *microphone* pale ni kwa sababu zile nyaya ni ngumu; vinginevyo, alitaka ang'oe ile *mic* akurushie wewe. Nilishawahi kutahadharisha na leo ninatahadharisha tena, watu hawa tuwaangalie sana, wanaweza wakaingia na vitu vya ajabu humu halafu

Bunge lako likapata matatizo. Narudia, usalama ni kitu cha msingi sana popote pale, siyo humu ndani ya Bunge, siyo vijijini na siyo kwenye majumba yetu; popote pale usalama ni kitu cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea na utaratibu huu, Bunge lako Tukufu halitakuwa tena Bunge Tukufu, litakuwa Bunge la Wakorofi. Wabunge wa CCM hatutaki tuitwe Wabunge wakorofi. Sisi ni Wabunge Watukufu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunajadili mambo yetu kwa hoja, kama lipo tatizo tunasema hapa tunaiomba Serikali irekebishe iwe hivi, lakini siyo kusimama kama walivyosimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kuwa, kitendo cha leo, Bunge letu limevunjiwa hadhi na kama upo utaratibu kupitia Kamati yako ya Maadili ya Bunge, tusiachie tendo hili. Tukiacha tendo hili litaendelea tena na mambo haya yanafanyika kwa sababu tunawalea, eti demokrasia. Je, hii ni demokrasia? Ninaomba sana, marekebisho haya sina tatizo nayo hata kidogo. Kwa sababu mwanzo tulisema mahali fulani, sasa ni lazima turekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa. Mheshimiwa Said Nkumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Adam Malima, kama mchangiaji wa mwisho. Mheshimiwa Said Nkumba!

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nichukue fursa hii, kwanza, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vilevile ninaomba nianze kwa kuunga mkono Muswada huu, ambao uko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tukumbushane; mkiwa safarini kwenye basi, basi likifika *stand* wapo wanaoshuka na wapo watakaoendelea na safari. Wenzetu wameshuka ingawa hawajalipa nauli, tuwasamehe tuendelee na safari yetu. Katiba hii siyo Katiba ya Vyama vya Siasa, Katiba hii ni ya Watanzania na sisi tuko hapa kuwawakilisha Watanzania. Ninaomba niendelee kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuendelee kusonga mbele katika jambo hili muhimu kwa masilahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alishasema mwanzo, siku moja alisema Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuapa ni vizuri angalau tukaangaliwa kama tuko timamu. Mimi hili jambo lilinichanganya kidogo, lakini leo hii ninaanza kulikubali kwamba, ni vuzuri baada ya Waheshimiwa Wabunge kuchaguliwa, wanapoingia humu ndani wapimwe akili zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hainiingii akilini, kwa Mbunge kuingia katika jumba hili takatifu, kufanya vitendo ambavyo hata mtoto akiingia humu, kutokana na hadhi iliyopo ya jumba hili hawezi kufanya. Tulimshuhudia Mheshimiwa Tundu Lissu, akivunja meza

ile kwa kupiga mikono, halafu humu ndani huwa hatutumii nyundo, tunatumia mikono tu hii. Mikono inavunja meza hii. Mheshimiwa Sugu, ameamua kuondoa kabisa kipaza sauti. Hivi haya mambo kweli ni ya watu ambao wako timamu? Mimi ninafikiri kama kweli tunao uwezo hebu tuanze na hawa. Hospitali ya Mirembe ipo karibu hapa, twende tukawaone Madaktari tuanze na sisi wengine tutafuata. Hali hii siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kusema ni kwamba, kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA walisema kwamba, wakishika madaraka ndani ya siku 100, watakuwa na Katiba mpya. Leo hii, Mheshimiwa Rais, baada ya kuapishwa alisema kwamba, katika kipindi cha uongozi wake kutakuwa na mchakato wa kuhakikisha Watanzania wanapata Katiba kwa muda mrefu na siyo siku zile 100. Mchakato umeanza zaidi ya hizo siku 100 walizozisema, vitimbi hivi vinaanza kufanya haya ambayo yamejitokeza. Mimi ninasema, huku ni kuwadhihaki Watanzania.

Nimesikia hapa watu walikuwa wanaimba tunataka haki zetu. Waliomo humu kwa uchache wao wana haki zao, lakini waliomo humu kwa wingi wao, Wabunge wa CCM na sisi haki zetu lazima ziheshimike vilevile. Haki za Wabunge wa Chama Tawala na kwa sababu ya wingi tulionao, ambao umejidhihirisha katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, umejidhihirisha katika Udiwani, umejidhihirisha katika Ubunge na umejidhihirisha katika Urais na hata maoni ya Mabaraza ya Katiba, ambayo yamekuwa

yanaendelea huko, umedhihirika kabisa kwamba Watanzania bado wanakiamini hiki Chama cha Mapinduzi, lazima tuendelee kuheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kuheshimu wenzetu wajue, sijui wanasoma Biblia au Misahafu, kama hawasomi ninataka niendelee kuwakumbusha; sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Ninachojifunza kutoka kwao, wenzetu wanapaza sauti kwa hoja dhaifu. Sasa sisi tuendelee kujenga hoja zetu za nguvu, ili tuendelee kuwajenga Watanzania waendelee kutuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hoja ambayo leo na jana imekuwa ikisemwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameisema ni kwamba, Mheshimiwa Rais asiteue wale Wajumbe 166, kwa maelezo hayo kwamba, Mheshimiwa Rais yeye ni Kiongozi wa Serikali na ni Kiongozi wa Chama. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu, utampata wapi Rais ambaye siyo Kiongozi wa Chama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niseme kwamba, Mheshimiwa Rais, atakuwa anafanya jambo hili kubwa kama walivyosema wenzangu, kwa sababu yeye ni Mkuu wa nchi na ndiyo sababu madaraka haya makubwa anayachukua kwa niaba yetu sisi sote. Kama walivyosema wenzangu kwamba, majina yatatoka kwetu sisi wenyewe huku, tunampelekea Mheshimiwa Rais, kwa nafasi aliyopewa kwa mujibu wa Katiba anafanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais huyu huyu ambaye leo na jana wanamdhihaki hapa, mambo yakiharibika hapa wanakwenda Ikulu, kwa huyo huyo wanayemdhihaki. Hawa wananikumbusha yuko ndege mmoja anayeitwa ngurumbizi. Huyu ngurumbizi ukienda jioni maeneo ambayo wanakwenda kulala unawaona wengi wamekaa kwenye kichaka wanafurahia na maneno yao ya kufurahi na kupigapiga mabawa na kadhalika ni ya kusema kwamba, haya ni maeneo yetu, hapa hatuhapami na tunapapenda sana. Usiku wakiingia kulala mambo yanayoharibika mle usiku mzima, asubuhi viota vyao vimechafuka vinanuka wanasimama wanapiga mayowe ya kusema hapa haturudi tena! Ngurumbizi watakwenda huko kuchunga jioni utawaona wamerudi tena hapohapo walipokataa kurudi!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niseme kwamba, viti vile vimekaa wazi, kama siyo ngurumbizi hawa tutawaona, hivi tukae hata kama si Bunge la kesho lakini Bunge lijalo tuone kama hawatakalia vile viti; ngurumbizi hawaaminiki wala hawaeleweki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, huu utaratibu wanaousema kwamba, wadau hawakushirikishwa na kadhalika, kama walivyosema wenzangu; mimi nimeingia Bungeni hapa mwaka 2000. Katika historia nimekuta kwamba, suala la kuita wadau kushiriki katika suala zima la kutunga sheria mbalimbali lilianza mwaka

1995. Sasa nataka niulize; hivi hawa wanataka kutuambia kwamba zile sheria zote tulizozitunga kuanzia mwaka 1995 kurudi nyuma ambazo hazikushirikisha wadau mbalimbali zote ni batili tuzifute? Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, utaratibu huu wa kuwashirikisha ni kupanua wigo zaidi, kuwashirikisha wenzetu wadau mbalimbali waweze kutoa maoni yao ili tuweze kuwa na mambo ambayo ni ya Kitaifa zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu, kama walivyosema wenzangu, jambo hili kwanza limekwishachukua gharama kubwa; na ninataka Watanzania waelewe; hivi mnavyofika mahali ambapo Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa Katiba alishapewa mamlaka, akateua Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Tume hii imeshachukua gharama kubwa sana na Watanzania wameshirikishwa kwa namna nyingi kwenye Mabaraza, wameshirikishwa katika kutoa maoni, mambo yote haya yana gharama kubwa sana, ambayo yote haya ni gharama za mlipa kodi Mtanzania. Leo tunapokaribia mwisho, wanatokea watu wanasema mambo yote haya hayafai, aidha tuahishe au tuache kabisa! Huku kwa kweli ni kuwaibia walipa kodi wa Tanzania fedha zao ambazo zinaonekana hazitakuwa zimetumika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa niaba ya Wananchi wa Sikonge na nimesimama hapa ndugu zangu kwa heshima kubwa na unyenyekevu mkubwa, kuwaomba Watanzania, kwa hili lililotokea

leo waanze kuwa wanatufahamu vizuri kwamba, ni nani ambaye kila wakati ni mtulivu katika kujenga hoja na ni nani kila wakati anajitahidi sana kuepusha shari.

Mimi naangalia sana hapa ndani, hivi inapofika mahali Naibu Spika leo ulikuwa unaoneshwa kidole, lakini hata ukiangalia mazingira yenyewe humu ndani, Wabunge walio wengi ni wa Chama Tawala; sasa wote tukiamua kuwa na busara kama walizonazo wao hivi leo hapa pangekalika? Kungekuwa hakuna cha Naibu Spika wala cha *Sergeant-At-Arms,* wote tungepotea kadiri ya uwezo wetu.

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba, Watanzania wote tunahitaji utulivu. Nimemsikia mama yangu wa Kusini anasema wanawake wawe mstari wa mbele, hakuna, hata wanaume tunahitaji utulivu katika mambo yote, bila utulivu hakuna chochote, hakuna maendeleo wala hakuna ndoa. Nataka niseme kabisa kwamba, Watanzania tunahitaji utulivu usiku na mchana ili tuendelee kuishi vizuri na tuendelee kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Juma Nkumba. Mheshimiwa Adam Malima!

**MHE. ADAM K. MALIMA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

naomba nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitamke kwamba, katika miaka yangu minane ambayo nimekaa katika Jumba hili, sijawahi kuona aibu ya kuwa Mbunge kama siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niseme dhahiri kabisa kwa dhati ya moyo wangu kwamba, wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ni rafiki yangu wa karibu sana. Sisi Wagogo na Wazaramo tuna mambo yetu na hata mila zetu zinafanana kidogo, lakini nakuomba sana nikwambie kwa dhati ya moyo wangu kwamba, utulivu uliouonesha leo ni wa mfano, kwa sababu hawa wamezoea kukuchezea na hata mara ya mwisho lilipotokea vagi humu ndani, ulikuwa umekaa kwenye Kiti. Sasa ndugu zangu Watanzania, twende tukielewana, hili siyo jambo la bahati mbaya ni la makusudi, walikuwa wanakusudia kukidhalilisha Kiti na hakuna kitu ulichofanya cha heshima kwa Bunge hili kama baada ya kuwatoa na sisi tukaendelea na shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie suala la ndugu zangu hawa, Mheshimiwa Rais alipokuja kufungua Bunge hili alipoingia wao walitoka na walipotoka hoja yao ilikuwa hawamtambui Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa ndiyo Rais wa Jamhuri ya Muungano. Naomba niulize na wenzangu mniambie kwamba lini walitamka kumtambua lakini chai wakaenda kumimina!

**MBUNGE FULANI:** Na *juice!*

**MHE. ADAM K. MALIMA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Na *juice!* Baada ya kutoka kwenye chai, naomba niwasomee *Hansard,* maana sisi ni Wabunge, tunafanya vitu vyetu kwa kumbukumbu. Naomba niwasomee *Hansard.*

*Bismillahi!* Nanukuu: "Mheshimiwa Spika, naomba katika kuhitimisha maoni yangu kusisitiza kwa mara nyingine tena, Tundu Lissu huyo anaendelea, mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais katika kuletwa kwa Muswada huu, baada ya kunywa chai, kwa pamoja na Jedwali la Marekebisho lililoambatanishwa miezi miwili tu baada ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kupitishwa na Bunge lako Tukufu na kupata kibali cha Rais, naomba nisisitize tena kwamba, katika jambo hili muhimu kwa Taifa letu, Mheshimiwa Rais amekuwa msikivu kwelikweli kwani amejiweka juu *ya the partisanship and factionalism of party politics* na ameangalia masilahi mapana ya Taifa letu. Ni wajibu wetu sasa kuwathibitishia Watanzania kwamba, kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais na usikivu wake na uongozi wake katika jambo hili, haukuwa wa bure. Anasema Tundu Lissu! *(Kicheko)*

Naendelea; Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inafarijika kwamba Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge, Kamati ya Mheshimiwa Pindi Chana, ya Bunge lako Tukufu imeridhia na kukubali mapendekezo yote ya Muswada huu na

Jedwali la Marekebisho ya Serikali. Kwa sababu zote hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni siyo tu inaunga mkono Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba 2011, bali pia inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali *the narrowness of our political party affiliation*, tuungane na Mheshimiwa Rais katika kulipatia Taifa letu utaratibu wa kutengeneza Katiba mpya wenye mwafaka wa Kitaifa. Nimemaliza kunukuu na huyu ni Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Leo Rais hawezi kuteua watu 166 wa kutosha kuingia humu, sisi pamoja na Baraza la Wawakilishi kwa sababu Rais huyu ni wa Chama cha Mapinduzi! Aah, sasa wakati ule alikuwa ni Rais wa Chama gani? Waswahili wanasema mtu ukimwona anabadilika badilika basi ana vitu viwili; ama ni mnafiki au ni mgonjwa na kwenye hatari ya kuwa mnafiki, Mtume wa Mwenyezi Mungu *S.A.W.* alisema, mnafiki ana sifa tatu dhahiri kabisa hazimtoki; akisema hasemi kweli; ya pili, akiaminiwa hana dhamana umemkabidhi kitu peleka hafikishi; ya tatu, akitoa ahadi hatimizi, ndiyo hao! Sasa tunataka tukae, tumalizane, tukasirikiane na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako hili Tukufu leo tumetia aibu kwa Watanzania, lakini kwa bahati nzuri Watanzania wamewaona. Nami nimepata *message* nyingi, maana sisi wengine tunasema tunatoka kwenye Majimbo, kama mimi nimetoka kwenye Jimbo ambalo lina *CUF* wawili au watatu, CHADEMA mimi sina, lakini nina *CUF* wawili au watatu. Nikienda kwenye ziara

zangu nikiwakuta *CUF* nawaambia huko mliko siko, sasa leo wenyewe wamenitumia *message* wamesema, Mheshimiwa kweli tumekiri kwamba ndugu zetu wale hata sisi tuna mashaka nao.

Ndugu zetu hawa miezi miwili tu iliyopita, yaani tarehe 30 Mei, 2013, amezungumzia Mheshimiwa Komba na mimi nataka niseme kutokana na *Hansard,* anasema hivi; kwanza Masoud huyu, anasema, Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa naomba niseme, Taarifa ya Wenje ina mambo yafuatayo; Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *CUF* kutokana na itikadi zake za mlengo wa kiliberali ambazo miongoni mwa misingi yake mikuu ni pamoja na kupigania haki za ndoa ya jinsia moja, usagaji na ushoga. Sisi CCM tukasema aah, *shame, shame!*

Mheshimiwa Masoud anaendelea; Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya hayakubaliki kutolewa ndani ya Bunge. Maneno haya hayana ukweli, huu ni uzushi, huu ni uongo, huu ni uhuni, huu ni uzandiki. Anaendelea tena anasema, Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Chama cha Wananchi *CUF*, tutachukua hatua inayostahili dhidi ya Bunge na dhidi ya CHADEMA. Ndiyo hii hatua yenyewe waliyoichukua leo? Aah, maana mambo mengine turejee tu humu humu wala tusiende mbali; ndiyo hii hatua yenyewe? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachobishaniwa ni nini? Mambo manne makuu ndiyo yamejitokeza na Watanzania mnisikilize. Moja, walikuwa

wanazungumzia mamlaka ya Rais, wana mashaka na mamlaka ya Rais leo. Wanasema Rais akiteua anaweza akateua jamaa zake Wakwere, Wazaramo na kadhalika akajaza 166. Sasa ule wasiwasi wao siyo wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ni mfano wao wenyewe, maana wageuke nyuma waangalie, wangepata wao nafasi hiyo ingekuwa mamsapu, dada, binamu na kadhalika! Mfano wao upo! *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Mkwe!

**MHE. ADAM K. MALIMA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mkwe!

**MBUNGE FULANI:** Mwanawe!

**MHE. ADAM K. MALIMA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Nyumba ndogo! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana twende tukiwatazama mfano wao. Kwa hiyo, wanamtilia mashaka Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete siyo kwa mfano wa Jakaya Mrisho Kikwete na Chama chake; kwa mfano wa kwao wenyewe. Kwa hiyo, naomba kwa hili la kwanza la mamlaka ya Rais, tusiwe na wasiwasi nalo. Hili la watu 166 na uwakilishi wao ndiyo la pili linalowatia wasiwasi, ajabu *Minalrahmani,* maana jamani tukubaliane, hii Kamati ya Rasimu ya Katiba imetengeneza Rasimu ambayo sisi wengine Wana-CCM hatuipendi hata kidogo na Kamati ile imeteuliwa na Mwenyekiti wetu wa Taifa, lakini tumesema kwa

sababu *it is part of the democratic process,* twende nayo mpaka tufike mwisho tuone. Sisi hatuna raha nayo sana hii Kamati, tuseme ule ukweli kabisa, wanatuvuruga. Baadhi ya Wanakamati wa hii Kamati ya Rasimu, kwangu Mkuranga wamekuja, Mkoa wa Pwani wamekuja, wanawaambia watu huko mnakosema Serikali tatu ninyi hamna akili na kadhalika; sasa unauliza ninyi mnasema mmekuja kuchukua maoni au mmekuja kuleta ya kwenu? Lakini tumekubali na tunakwenda nayo.

Sasa leo na sisi CCM tuanze kusema aah, unajua Kamati hii sijui nini, hapana! *It is part of the process* tuliyojichagulia sisi wenyewe. Ile nyingine ya theluthi mbili na kadhalika na yenyewe tumesema kwa nia njema. Juzi Mheshimiwa Halima Mdee, alikuwa hapa wakati tunazungumzia suala la Ushirika, kaleta *Schedule of Amendment* karatasi karibu 200, tukapitia moja hadi nyingine, mbona hawakutoka? Katika hili kuna jambo, tujiweke kwenye nafasi ya kuanza kubaini yale mambo na kuwaambia Watanzania hawa muwaangalie, wapo katika zile sifa tatu na hawa wenzetu wa upande huu ni wa kuwasikitikia maana kilichowafanya kutoka kile kipengele cha ushirikishwaji wa Zanzibar, basi! Hawa leo wametutia aibu sisi Wazanzibari wenzao kupita kiasi.

*CUF* mlipokuwa mnaongoza Upinzani, mliwabeba na hawa, Mheshimiwa Zitto alikuwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Slaa alikuwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Grace Kiwelu alikuwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mhonga alikuwa Waziri Kivuli, lakini walivyopata wao

walisema ninyi hamna akili hamfai! Hivi kweli leo mtu kama Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na uwezo wake wote anaweza kuwa siyo Waziri wa Upinzani, anakuwa Waziri Mheshimiwa Peter Msigwa? *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Au Sugu!

**MHE. ADAM K. MALIMA – NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Au Sugu! Aah, *Subhanallah!* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha ajabu, Mheshimiwa Tundu Lissu akisimama hapa miaka yote yeye ni kuwatukana tu Wazanzibari, kawapenda lini? Sasa hii basi!

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Dini ya Kiislamu kuna kitu kinaitwa Ndoa ya Muta. Mtume *S.A.W.* mwanzoni kabisa ilikuwa wanapokwenda vitani wakishinda, kwa sababu wale maadui wanaume wote wanakuwa wamekufa vitani, wale wanaume wametoka wakati ule hakuna ndege na kadhalika, wanakaa miezi sita au mwaka hawajaonana na wake zao. Wakifika pale wanasema sasa Mzee, hawa akina mama ambao tumeshaua waume zao tufanyeje? Anasema basi muwaoe japo muwafanyie stara ya kipande cha nguo na kadhalika, lakini muwape muda baada ya wiki achaneni nao. Baada ya muda katika historia ya Uislamu, baada ya pale Mtume *S.A.W.* akaamua ile ndoa basi. Sasa jana nikatumiwa *message* nikaambiwa hicho kilichotokea leo ni Ndoa ya Muta! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kusema ni kwamba, hii si Ndoa ya Muta maana Ndoa ya Muta ni yule mshindi ndiyo anaoa. Sisi leo tumewagaragaza wao, lakini ndoa imekuwa ni ya wenyewe kwa wenyewe waliogaragazwa. Sasa hii haiwezi kuwa Ndoa ya Muta, hiki ni kitu kingine. Nilitaka niwaambie tu walionitumia *message* kwamba, hii siyo Ndoa ya Muta ni kitu kingine maana wamegaragazwa wao wakabebana wakaondoka wao. Kilichonishangaza na kunifedhehesha ni kumwona Mheshimiwa Khatib katoka kule juu, Mheshimiwa Mbowe anakuja kudhibitiwa eti na yeye anakuja kumkingia kifua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Adam Malima, ndiye mchangiaji wetu wa mwisho siyo tu jioni ya leo bali ni kwa shughuli iliyopo Mezani.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Katiba litakuwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge na watu 166 kutoka Taasisi mbalimbali za

Kidini, Kiraia, Vyuo Vikuu na kadhalika. Mimi nakubali mia kwa mia Rais kuteua Wajumbe hawa, hasa kwa kuwa Taasisi hizi zitapendekeza watu watatu kwa Rais. Pia nakubaliana na idadi ya Wajumbe kuwa wanatosha kuwawakilisha Watanzania katika kujadili Rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji Mkuu wa Upinzani amesema kuwa, tayari CCM ina asilimia 72 ya Wajumbe (Wabunge na Wawakilishi) na hivyo kupewa nafasi ya kuteua Wajumbe 166, itawasaidia kupitisha Rasimu kama wanavyotaka wao. Hii siyo hoja, kwani Wawakilishi na Wabunge wanachaguliwa na Wananchi. Pia Taasisi ndizo zinazopendekeza Wajumbe watatu na Rais anachagua mmoja tu katika Wajumbe hao watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi uliotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) kuwa, Taasisi ndizo zilizopendekeza majina matatu kwa ajili ya uteuzi wa Mjumbe mmoja, zimewatoa wasiwasi Watanzania kuwa hakuna uchakachuaji. Zuri zaidi ni kuwa, majina yaliyoteuliwa ni yale yaliyopendekezwa na Taasisi, hivyo ni hakika kuwa palikuwa na uadilifu mkubwa katika kuteua majina ya Wajumbe kutoka Taasisi.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuwa na Wabunge wa

kuteuliwa kufikia idadi ya 166. Ila kwa matukio yaliyotokea Bungeni jana na leo ni bora kipindi cha Bunge Maalum ulinzi ukaimarishwa. Inawezekana kabisa vurugu kutokea kipindi cha Bunge Maalum la Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ijulikane na kutambulika kwamba, Mheshimiwa Rais ni chaguo la Watanzania, tusikubali adhalilishwe na wahuni wachache. Sheria ilishatungwa kuwa atateua Wabunge kutoka kwenye orodha atakayopelekewa na hilo liendelee kubakia hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 22 tunahitaji Katiba Mpya kabla ya 2015, Wananchi walio wengi wapate fursa ya kuisoma na kuielewa, ili Uchaguzi Mkuu uwe katika misingi imara ya uwazi, haki na usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati na kwa kuendelea na Mpango wa Katiba Mpya. Pamoja na Serikali kuwa msikivu kwa kukubaliana na mapendekezo ya Wabunge katika kurekebisha baadhi ya vifungu vya sheria kwa masilahi ya Watanzania, pamoja na kelele za Wapinzani, nia na madhumuni yao ni kutafuta kuungwa mkono na

baadhi ya Wananchi wasioelewa vizuri maana ya Rasimu ya Katiba; watembee nchi nzima kwa kuwashawishi Wananchi ili kuwavuruga wasielewe nia nzuri ya Serikali yetu katika kupata mawaza ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iendelee na Muswada huu bila kupoteza muda ili Watanzania waweze kupata Katiba hiyo mpya kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza sana Waziri na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na Kamati ya Bunge, kwa hatua nzuri waliyochukua kwa tahadhari kubwa katika mchakato huu kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya ya Katiba yanatoa usawa wa kijinsia, Kifungu 2 (B), ya Wajumbe wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha (4) kipya, nashauri watumishi siyo lazima wote watoke katika Bunge au Baraza la Wawakilishi. Kama tunaweza kupata wengine nje ya Taasisi hizo, wenye uwezo wa

kisheria, waliobobea na wenye maadili mema na yanayokubalika, wateuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 24 cha Muswada Mama na Kifungu cha 24(4) kipya, kwa hivi sasa hatuna *Deputy Clerk* ingawa ikama inatoa nafasi hiyo. Je, wakati huo ukifika tutakuwa tumeshaajiri? Tujiridhishe basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 27(5)(3), utaratibu wa kuendesha mjadala katika Bunge Maalum utaainishwa katika kanuni. Hivi itachukua muda gani kutengeneza hizo Kanuni ili ziweze kuwahi kutumika kwa wakati mwafaka? Je, tutazipitisha Bungeni? Bunge hili linayo mamlaka hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 28(6)(3) na (4), ni vyema muda wa kuongezwa wa siku 20 inawezekana ukawa mfupi au mrefu, ni bora kutoa muda wa kutosha wa kukamilisha majadiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 27, Kifungu kipya cha (3), kinachohusu *Standing Orders* zitakazotumika katika Bunge la Katiba; zitatengenezwa lini? Tutawahi?

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, napenda kuelezea masikitiko yangu kuhusu tabia ya baadhi ya Wabunge, hasa wa Kambi

ya Upinzani, kutumia jukwaa la kujieleza Bungeni kwa kutoa matamshi ya uongo, ya uchochezi, hivyo yanadhalilisha heshima ya Bunge lako Tukufu. Kiti kitumie Kanuni za Kudumu za Bunge kuhakikisha taratibu zinafuatwa, ama sivyo Bunge hili Tukufu litageuzwa ukumbi wa vioja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa na hoja hafifu za kisheria zilizotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambazo zinatoa hukumu kwa kuzingatia kipengele kimoja tu cha Muswada badala ya kutumia tafsiri oanishi, ambayo msomi mzuri wa Sheria hana budi kuitumia anapoangalia vipengele vya Sheria au Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nitumie fursa hii kumkumbusha mwanafunzi wangu wa sheria wa zamani kuhusu ufafanuzi alioutoa Jaji Henchy wa *Supreme Court* ya Ireland mwaka 1982 katika kesi ya *DPP vs O'Shea (1982) IR 384* kuwa: *"Any single constitutional provision is but a component in an ensemble of interconnected and interacting provisions which must be brought into play as part of a larger composition".* Tafsiri yake ni kuwa; "Kipengele chochote kile cha Katiba ni sehemu katika mkusanyiko wa vipengele vinavyoungana na kuingiliana kimaudhui, ambavyo lazima vizingatiwe kama sehemu ya tungo moja."

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi wangu huyo wa zamani akijikumbusha nukuu hiyo, atarejea kwenye msimamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa wajumbe 166 katika Bunge la Katiba, naunga mkono taasisi ziteue majina matatu, kisha orodha ikabidhiwe kwa Mheshimiwa Rais ambapo yeye Mheshimiwa Rais atateua jina moja kati ya yale majina matatu ya kila taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upigaji kura katika Katiba, naunga mkono marekebisho yaliyotolewa na Serikali Bungeni kwamba endapo kura zitapigwa zaidi ya mara mbili lakini ikatokea haikupatikana $^2/_3$ ya kura kwa pande mbili za Muungano, basi kura zitapigwa kwa mara nyingine kwa mfumo wa *simple majority* (wingi wa kawaida).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kupiga kura kwa *simple majority* kwani hakuna madhara yoyote katika uwakilishi wa wananchi wa pande zote mbili za Muungano kwani mwisho itatengenezwa *draft* ya mwisho ya Rasimu ya Katiba ambayo itaenda kupigiwa kura na Watanzania wote ambapo ndipo kwenye ushiriki mpana wa wananchi kutoka pande zote mbili za Muungano. Nashauri Watanzania waelimishwe zaidi kwamba wajibu wa Bunge ni kutunga sheria. Aidha, katika mchakato huu wa Katiba Mpya, wananchi ndiyo watapiga kura kupitisha Rasimu ya mwisho ya Katika na hatimaye kupatikana kwa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukomo wa Bunge Maalum la Katiba, Ibara ya 28(1) na (2), naunga mkono Mheshimiwa Rais kuitisha Kikao cha Bunge Maalum kwani baada ya Kikao cha Bunge la Katiba kuahirishwa na kumaliza kazi yake na kufungwa, litakuwa limepoteza sifa ya Wajumbe kuendelea kuwa Wabunge. Hivyo, lazima pawepo na fursa ya kushughulikia endapo litatokea jambo la kuleta ufanisi. Aidha, katika sheria yoyote lazima pawepo na mwanya wa rufaa wa kushughulikia jambo husika. Hivyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais kuitisha Kikao cha Bunge la Katiba ili kuleta ufanisi na ubora katika kuhakikisha tunapata Katiba Mpya inayokidhi matakwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu iko katika mchakato wa kupata Katiba Mpya ya nchi. Kimsingi, Muswada huu una lengo la kufanyia marekebisho ya msingi Sheria Mama ili kuhakikisha kwamba Bunge Maalum la Katiba linaundwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuusoma Muswada, utaona umejikita katika kutoa njia ya namna ya kuwapata Wajumbe 166 ambapo Mheshimiwa Rais ndiye atawateua Wajumbe hawa kutoka miongoni mwa watatu watakaokuwa

wamependekezwa na taasisi na makundi yenye usajili wa kisheria. Jambo hili naliafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja linaloshangaza zaidi ni kuona baadhi ya Wabunge wa Bunge hili hasa kutoka CHADEMA wanapinga Mheshimiwa Rais kuwateua Wajumbe utafikiri wanateuliwa kwa utashi wa Rais binafsi. Kinachoonekana hapa ni sarakasi za kisiasa za kujaribu tu kuchelewesha mchakato wa kupata Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba CHADEMA na mgombea wao wa Urais - Dkt. Willbrod Slaa, wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2010 walikuwa wakijinadi kwa wapigakura kwamba wangewapatia Watanzania Katiba Mpya ndani ya siku mia (100) baada ya kuchaguliwa. Dkt. Slaa ni Katibu Mkuu wa CHADEMA na kama angepewa ridhaa ya kuwa Rais, ni dhahiri kuwa ndiye angekuwa msimamizi wa mchakato wa kupata Katiba Mpya ambayo kimsingi inaonekana kuwa alikuwa nayo tayari mfukoni mwake, ambayo kimsingi isingekuwa imejumuisha maoni ya wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Watanzania kwa wingi wa kura walimpatia Mheshimiwa Rais na Chama cha CCM na mara baada ya kuapishwa kuwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alilihutubia Taifa kueleza dhamira ya uongozi wake wa kuwapatia Watanzania Katiba Mpya na leo hii tuko hapa tukitekeleza hatua kwa hatua azma hiyo ya Mkuu wa

nchi, naomba Bunge lisonge mbele katika azma ya kupitisha Muswada huu. Hivyo basi, kifungu cha 22 cha Muswada huu na marekebisho yote yanayopendekezwa, nayaunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo pia taratibu zinazopendekezwa za namna ya kumpata Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, Katibu na Naibu wa Bunge hili na Watumishi watakaoajiriwa kwa muda kulitumikia Bunge Maalum, marekebisho yote haya nayaunga mkono.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono Muswada huu kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji wa Kambi Upinzani amesema wadau pekee walioshirikishwa kutoa maoni yao juu ya Muswada huu ni Watanzania Bara tu. Kwa hili, mimi sikubaliani nalo. Kwanza wadau si watungaji sheria, ila ni Wabunge. Hata hivyo, Wazanzibari wameshirikishwa kikamilifu kwa ushahidi wa Barua ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar – Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, iliyosomwa leo tarehe 5 Septemba, 2013 katika kikao cha jioni cha Bunge hili. Huo ni ushahidi tosha wa kuonesha ushiriki wa Wazanzibari. Sasa kuna baadhi ya Wabunge wanasema Zanzibar haikushirikishwa na kufanya fujo na kutoka nje ya ukumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naunga mkono Mheshimiwa Rais kuwa ni mteuzi wa Wajumbe wa Bunge Maalum kwa wale wasiokuwa Wabunge wala Wawakilishi. Maana Mheshimiwa Rais ndiye atakayeweza kufanya uadilifu katika uchaguzi huo, maana yeye ndiye aliyefanya uchaguzi wa Wajumbe wa Tume na watu wameridhika. Sasa kimezidi nini katika uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge Maalum? Wajumbe 166 ni idadi tosha kwa ajili ya kuongezea Wajumbe wote wa Wajumbe wa Bunge Maalum. Hakuna haja ya kuongeza idadi kubwa kuzidi 604 kwa pamoja.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nishukuru kupata nafasi hii kuchangia japo kwa maandishi Muswada uliokuwepo mbele yetu. Nitangulize kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme na niwaambie Wabunge wenzangu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi wote wa Tanzania Bara na Zanzibar kwamba Bunge hili halipo hapa kutunga sheria na kupitisha sheria ambayo Katiba tunayotaka kuiunda itailinda au kuiondoa madarakani CCM kama wenzetu wengine wanavyotaka. Bunge hili haliko hapa kutunga sheria ili Katiba tunayotaka kuiunda ambayo itakuwa na masilahi ya kikundi fulani kwenda Ikulu au Chama fulani kiendelee kubaki Ikulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili kazi yake ni kutunga sheria zitakazowezesha nchi yetu kutunga

Katiba itakayolifanya Taifa hili linasonga mbele kwa miaka mingine zaidi ya 50 Taifa likiwa wamoja, lina imani, mshikamano na kasi ya maendeleo tunayohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kuwakumbusha Watanzania na Wabunge wenzangu kuwa wako watu walikataa kukubali matokeo ya uchaguzi wa 2010 ambayo yamempa Rais Kikwete madaraka ya Kuunda Dola na Chama chake cha CCM. Kuna watu walitoka nje ya Bunge wakati Mheshimiwa Rais alipolihutubia Bunge hili kwa mara ya kwanza. Watu hao walisema nchi hii haitawaliki na wakati wa awali wa maandalizi ya Mchakato wa Kutunga Sheria juu ya Uundaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba walitoka nje ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, hata haya yaliyotokea jana kwa Wabunge kutoka nje ya Bunge hili ni mwendelezo wa mambo yale yale. Niiombe na niipe angalizo Serikali kuwa makini katika jambo hili jema ambalo Serikali na Watanzania tunataka lifanyike na nchi iendelee kutawalika na amani iendelee kubaki. Hatua zote zinazotakiwa kuchukuliwa na Serikali zitumike ili Watanzania tuendelee kuwa wamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami baada ya utangulizi huu, niunge mkono mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 22 cha Sheria Mama ili kuongeza maneno ya Rais ili aweze kuteua majina hayo kwa niaba ya Watanzania wanaotaka kuunda Katiba ya masilahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, niendelee kuipongeza Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kazi hii kubwa ambayo tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nirudie tena kusema naunga mkono hoja. Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wajumbe 166 nakubaliana nalo na nakubaliana kwamba uteuzi ufanywe na Rais kwa kuzingatia mabadiliko ambayo yameletwa na Serikali na makundi mbalimbali kama yalivyoainishwa katika Muswada na majina yapelekwe kwake ateue. Wajumbe 166 ukiongeza na idadi ya Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wanatosha ukizingatia gharama na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kazi nzuri na kuweza kusimama kidete katika kuhakikisha mabadiliko haya yanaletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, lazima wachaguliwe kwa sifa na

vigezo vitakavyowekwa kwenye kanuni badala ya kuchagua tu. Tunahitaji watu makini katika nafasi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Katiba itakuwa haijapita, basi Katiba ya zamani itumike na ifanyiwe marekebisho. Nashauri uchaguzi ufanyike 2015, kuna watu wanapenda muda uongezwe kwa matakwa yao. Watakaoongezwa, pia uwiano wa kijinsia uangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nichangie kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuchangia leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yetu kwa kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa 2013. Pia naipongeza Kamati ya Katiba na Sheria kwa kuchambua vizuri mabadiliko yaliyopendekezwa na Serikali kwa kujadili na kukaa na wadau; lakini pia kuona mahali pengine kwenye sheria ambapo panahitaji marekebisho. Naunga mkono hoja katika kipengele cha 22 (a) na pia (b), (2)(a) na (2)(b).

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza namna uteuzi huo utakavyofanywa na suala la *gender* limezingatiwa, uwezo na uzoefu umetajwa. Naomba nishauri kwamba, yale makundi madogo yote pia yapate fursa. Mfano, vikundi vya Dini, Wahindu, Kalasinga, Ismailia, Bohora na kadhalika. Pia wawakilishi wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wapewe

kipaumbele, idadi yao iongezeke na kwa upande wa walemavu, yaangaliwe makundi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa 24(4), nashauri wengi wa hao watumishi watoke Bungeni na Baraza la Wawakilishi. Wengine watoke Wizara ya Sheria ili pia sisi Wabunge tupate msaada wa kisheia na tafsiri za sheria. Pia tupate wataalam wa tafsiri (Wakalimani).

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 26 nawapongeza kuona hilo na uchambuzi mliofanya na kupendekeza mahali ambapo hakuna uelewa, hatupati theluthi mbili ya mapendekezo, basi, kwa kawaida ipigwe *simple majority* kwa upande wa Bara na Visiwani katika vipengele ambavyo hatukubaliani. Pia ningeshauri Bunge la Katiba lifanywe nje ya Dar es Salaam. Kwani Dar es Saaam pale Wabunge hatutakuwa na umakini wa kutosha kutokana na mazingira ya Dar es Salaam. Kazi hii inatakiwa ifanywe kwa umakini sana, ni dira ya miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba elimu juu ya Rasimu itolewe ya kukamilika kwa Wananchi na pia taratibu na kanuni zote zinazotumika. Leo hii Wananchi wengi hawajui taratibu, kanuni na njia tuliyoamua kuchagua kupata Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba Mwenyezi Mungu atupe busara na hekima ili tupate Katiba yenye mafanikio kwa Taifa letu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu muhimu sana kwa Taifa letu. Naridhia marekebisho ya vifungu 22(3)(b) na 2(a), 24(4), 27(5)(2) na (3), na 28(6)(3); pamoja na jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali isimamie vyema mchakato huu wa Mabadiliko ya Katiba. Sheria ianze kutumika mara moja kwa wale wanaotaka kutuvurugia mchakato huu muhimu ili tuhitimishe mchakato mzima kutufikisha kupata Katiba Mpya ya nchi yetu itakayotuongoza kwa miaka 50 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii, na nasikitika, hivi ni kwa nini wenzetu wa upande wa pili wanasusia kujadili Muswada huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu hawa wana nia ya kujipatia umaarufu wa kisiasa. Kwa nini nasema hivyo? Wenzetu hawa (Upinzani) wameshiriki katika mchakato huu tangu mwanzo hadi hapa ulipofikia, wamekuwapo katika mijadala mingi wakikusanya maoni. Kikubwa zaidi, Kamati ya Katiba na Sheria, wengi wao ni Wanasheria na wengi wa Wanasheria hawa ndani ya Kamati hii ni Wabunge wa CHADEMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge hawa wameshiriki kikamilifu katika mchakato mzima huu wa kukusanya maoni ya Katiba kutoka maeneo na kwa watu mbalimbali. Sasa je, kinachoshangaza, leo wanasema kwamba Wazanzibari hawakupata nafasi ya kutoa maoni hapa ndani ya Bunge, walikuwa wapi kutoa maoni haya ndani ya Kamati ya Katiba na Sheria? Kwamba, Wazanzibari hawajatoa maoni kuhusu Katiba na Wabunge hawa walishiriki mchakato mzima na kuridhia mapendekezo yote yaliyotolewa ndani ya Kamati, ilhali wakijua kabisa utaratibu wote ulifuatwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Bunge la Wawakilishi wote kuwa Wajumbe wa Bunge hilo la Katiba, na naendelea kuunga mkono Wajumbe wale 166 kutoka Asasi mbalimbali watakaoteuliwa kwa mujibu wa sheria. Ndani ya Katiba hii kuna visheriasheria humu, ni sheria zipi zinazotungwa na Wabunge nusu, badala ya Bunge Zima?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee suala la Uteuzi wa Mamlaka ya Mheshimiwa Rais katika uteuzi wa Wajumbe wa Bunge Maalum wasiokuwa Wabunge au Wawakilishi. Mimi naunga mkono hoja hii, na naunga mkono mamlaka yote aliyopewa Mheshimiwa Rais ya kufanya uteuzi wa Wajumbe hao wote 166.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshatumia pesa nyingi kukusanya maoni ya Katiba, na ndugu zetu

hawa wameshiriki kwa kiwango kikubwa. Tunaelekea kwenye hitimisho la suala hili kwa ujumla, wenzetu sasa wanaanza kuvuruga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo wangu, huu ni mpango wa kuvuruga uchaguzi mzima wa mwaka 2015, ama kwa kuichelewesha Katiba Mpya ama kwa kusababisha isipatikane Katiba nzuri itakayowafaa Watanzania wote kwa ujumla. Vitendo hivi vinatupa angalizo kwa ujumla kwamba kumbe wenzetu hawana nia ya kupata Katiba Mpya, badala yake ni vurugu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kukupongeza sana wewe kwa kuliendesha Bunge letu kwa njia ya kidemokrasia na uelewa mkubwa wa majukumu yako kama Naibu Spika. Aidha, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu, kwani marekebisho yaliyoletwa yatafanya mchakato mzima wa kuandaa Katiba Mpya usonge mbele (uendelee).

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mzanzibari, nimezaliwa Zanzibar, nimelelewa na kukulia Zanzibar na hadi lao ninaishi Zanzibar (siishi Tanga wala Dar es Salaam wala eneo lingine lolote la Tanzania Bara).

Hivyo basi, Wapinzani waliposema kwamba Wazanzibari kwa maana pia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hawakushirikishwa katika kutoa maoni juu ya Muswada huu, nilishtuka na kuona kama hiyo ni kweli, basi siyo jambo sahihi kwa sababu jambo linalojadiliwa linahusu sehemu zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru na kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Muungano kwa kutoa elimu ya kutosha na kueleza kuwa SMZ wameshirikishwa na kutoa maoni yao tena kwa maandishi, na baadhi ya wadau pia wameshiriki katika majadiliano ya Kamati. Kwa mantiki hiyo, Wapinzani hawakuwa na sababu tena ya kutoka nje ya Bunge, kwani walilosema kuwa Zanzibar hawakushirikishwa, ndiyo sababu ya wao kutoka nje, halikuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na marekebisho yaliyofanywa katika kifungu 22(1)(c) ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba 2013 kwa kumtaka Rais kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar kuteua Wajumbe kutoka kila kundi lililopeleka kwake orodha ya watu watatu, Rais ndiye ateue, siyo vinginevyo; na wala uteuzi wake usihojiwe na mtu yeyote yule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais ni Kiongozi Mkuu ndani ya nchi, Watanzania wamemwamini na kumchagua kwa kura nyingi kuliko mgombea mwingine yeyote. Tuendelee kumwamini na wala asidhalilishwe na mtu yeyote eti kwa kumtaka atoe

sababu kwa nini amemteua fulani na siyo fulani. Idadi ya Wajumbe kutoka makundi mbalimbali ibakie ile ile tuliyokubaliana katika Bunge hili, nayo ni 166, wasiongezwe wala kupunguzwa, usawa wa kijinsia ukizingatiwa. Wanawake wapo wengi tu wenye elimu na uwezo mkubwa, nao wateuliwe wachape kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetumia busara ya hali ya juu kwa kuleta marekebisho ya kifungu 26 cha Sheria mama, kwa kusema kwamba endapo theluthi mbili katika uungaji mkono wa Katiba haikupatikana kwa mara mbili baina ya Wajumbe kutoka Zanzibar (2/3 ya Wajumbe kutoka Zanzibar) na 2/3 ya jumla ya Wajumbe kutoka Bara, basi utaratibu wa uamuzi wa masuala hayo uwe ni kwa wingi wa kura za jumla ya Wajumbe kutoka Zanzibar, na wingi wa kura kutoka Tanzania Bara. Jambo hili ni muhimu kwa kupeleka mbele mchakato wa kupatikana Katiba Mpya. Vinginevyo, Wajumbe wanaweza wakapingana na mara zote uamuzi usipatikane. Ninapongeza kwa busara hii. Wanaopinga kipengele hiki, hawana nia ya njema ya kutengeneza/kuandaa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi kabisa ikiwa katika muda wa siku 70 (zilizowekwa na sheria), Bunge Maalum la Katiba likiwa halijamaliza muda wake, basi lisiwekewe ukomo wa siku za kuongeza ili kumaliza kazi yake. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, wakubaliane na Marais wa Muungano na Zanzibar, wapewe muda wa kutosha kukamilisha shughuli za Bunge hilo Maalum kwa madhumuni ya kupata Katiba Mpya inayotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwamba Mheshimiwa Rais apewe mamlaka ya kufanya uteuzi wa Wajumbe 166 wa Bunge Maalum kama ilivyopendekezwa katika Sheria Mama, yaani Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2013 katika Kifungu cha 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kifungu 22 (a) kinachopendekezwa cha kumpata Makamu Mwenyekiti. Nakubaliana na mapendekezo.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa pole Mheshimiwa Waziri kwa majukumu. Mimi nataka kujua, kwa nini Sheria hii haitaji Makao Makuu ya Bunge Maalum ya Katiba yatakuwa wapi; yaani Mikutano ya Bunge Maalum kisheria itakuwa wapi katika nchi yetu?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kesho asubuhi baada ya maswali, tutaendelea na hatua zinazofuata za kushughulikia jambo lililo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, nitawaomba sana kwa ajili ya shughuli hizo, mahudhurio ni muhimu sana. Nitawaomba Waheshimiwa Wabunge baada ya maswali tusitoketoke ili tuweze kuutendea haki Muswada wetu.

Naomba niwatambue Waheshimiwa Madiwani wa Mbeya Vijijini, naomba msimame pale mlipo. Karibuni sana, Waheshimiwa Madiwani wa Mbeya Vijijini. Mbunge wenu Mheshimiwa Luckson Mwanjale, anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. Tupelekeeni salamu huko Mbeya, japo bahati mbaya leo Mbunge jirani yenu mmojawapo amefanya aibu kubwa hapa Bungeni, kwa kuvunja vipaza sauti, kwa kuchana sare ya Askari wetu wa Polisi wa Bunge, kana kwamba haitoshi kwa kumpiga kichwa Polisi nje ya Ukumbi wa Bunge. Mbeya haipo hivyo, tunajua Watu wa Mbeya ni wema, tupelekeeni salamu kwa wananchi kwamba, tunawaelewa Watu wa Mbeya ni wema sana, hii ni bahati mbaya tu na ni shetani tu. Ahsanteni sana na karibuni sana, mnaweza kuketi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri Watanzania wakafahamu na baadhi ya Wabunge wakafahamu kwamba, siyo wote wanaosoma Kanuni, ni wakati gani Kiongozi wa Upinzani kikanuni anaweza akasimama na kupewa nafasi, ni wakati mmoja tu kwenye Kanuni zetu, ni wakati wa mswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiyo kikanuni imeandikwa hivyo na anapewa nafasi ya kwanza. Siku zote mmeona wakati wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hatujawahi kuanza vinginevyo, ndiyo maagizo ya Kanuni. Wakati mwingine wowote ni utaratibu kama Wabunge wengine na kwa kuheshimiana, Kiti huwa kina utaratibu, lakini sasa imekuwa kama ndiyo sheria wakati siyo sheria. Kwa hiyo, inafika mahali mtu mwenyewe anaamini kabisa kwamba ni haki yake wakati jambo hilo halipo hivyo kwenye Kanuni.

Someni Kanuni na ni vizuri tuelewane, maana binadamu ukishaamini jambo fulani ni haki yako wakati siyo haki yako, basi unajiweka katika mazingira ambayo unadhani umenyimwa haki kumbe haki hiyo huna. Kwa hiyo, tunaomba kama wengine wote na tunafanya taratibu zetu kwa taratibu zilezile kama wengine wote, tutaendelea kuheshimiana na kuona ni namna gani katika kuheshimiwa huvunji haki ya mtu mwingine. Wakati ule ilikuwa ni haki ya Mheshimiwa Mrema kuzungumza, haikuwa haki ya yeye kuzungumza, lakini akaona kama Mheshimiwa Mrema hana haki hiyo isipokuwa yeye ana haki zaidi, wakati katika Bunge hili sisi Wabunge wote tuna haki zilizo sawa. *(Makofi)*

Sasa kwa hatua hii, baada ya Mheshimiwa Mrema kubaki Bungeni, kaka yangu yuko pale nyuma na baba yangu pia, akawa amenikumbusha kitu fulani, labda niseme kidogo, lakini katika kusema nia yangu siyo kumuudhi mtu yeyote.

Mheshimiwa Mrema akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na akiwa Naibu Waziri Mkuu, miaka 20, 21 au 22 iliyopita, kwa kumbukumbu yangu, alikuwa akifanya kazi zake vizuri sana wakati huo na alikuwa na sifa kubwa sana katika nchi. Mimi wakati huo nilikuwa nasoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maana watu wanafikiri wamesoma pale peke yao, kila siku Nkrumah pale wanakwenda wao wakifikiri wao peke yao ndiyo waliosoma pale lakini wako wengi humu.

Sasa miaka hiyo mimi nikiwa pale kama mwanafunzi, Mheshimiwa Mrema, akawa ameitwa na Jumuiya ya Wanafunzi na ilikuwa ni mkutano mgumu sana kwake. Swali moja alilopewa na Wanafunzi na Maprofesa waliokuwa pale lilikuwa kwamba; nini siri ya mafanikio yako? Kwa nini wewe unavuma wakati Mawaziri wenzako wengine hawavumi kama unavyovuma wewe? Mheshimiwa Mrema alijibu na mimi nakumbuka mpaka leo, ningeweza kuiga hata sauti yake lakini haifai. Akasema kwamba, yeye ni mtu anayejiamini, anafanya mambo kwa kujiamini na leo tumethibitisha hapa na jana pia.

Yeye aliteuliwa katika nafasi nilizozitaja na Mheshimiwa Rais Mwinyi. Akasema, mimi baada ya kuteuliwa na Rais Mwinyi na kupewa hizi nafasi, nimetoka nimekwenda kufanya kazi Tanzania nzima. Wapo baadhi ya Mawaziri wenzangu hata wakiteuliwa kuwa Mawaziri, hawaendi kufanya kazi bali kazi yao ni kuzunguka kwenye *corridor* za Ikulu, Rais akipita kwenda huku, shikamoo Mzee, akipita kwenda kule, shikamoo Mzee! Kwa hiyo, Bwanamkubwa anafikiri hawa wanachapa kazi, kumbe kazi yao kubwa ni shikamoo Mzee! Huyo ndiye Augustino Lyatonga Mrema wa miaka 22 iliyopita. Kwa hiyo, wapo Viongozi walifikiri kwamba, wakimwamrisha Mheshimiwa Mrema atawaambia shikamoo Mzee; hakuna hiyo, huyo ni Augustino Lyatonga Mrema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo, naomba niwashukuru sana kwa ushirikiano wenu. Naomba sasa

niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 6 Septemba, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*